Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA SITA

**Kikao cha Sita - Tarehe 16 Juni, 2004**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**DUA**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 49

**Kituo cha Dakawa**

**MHE. BAKARI M. MBONDE** aliuliza: -

Kwa kuwa Kituo cha Dakawa kina historia muhimu kwa ukombozi wa Afrika Kusini na kwa heshima ya Watanzania: -

(a) Je, Chama cha Ukombozi wa Afrika Kusini *(ANC)* kilikabidhi kituo hicho kwa nani?

(b) Je, kwa nini aliyekabidhiwa kituo hicho amekitelekeza kiasi kwamba kinaonekana kimechakaa na hivyo kutoenzi zawadi hiyo muhimu ya Chama cha *ANC* kwa Watanzania?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kukiimarisha na kukiboresha kituo hicho?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe maelezo mafupi ya Kituo cha Maendeleo cha Dakawa kabla sijamjibu swali lake Mheshimiwa Bakari Mbonde, Mbunge wa Rufiji.

Kituo cha Maendeleo Dakawa kipo katika Kata ya Magole, Tarafa ya Magole, Wilaya ya Kilosa. Kina eneo la hekta 2,800 za ardhi ya kilimo na ufugaji, nyumba za makazi 82 zenye familia 116, pamoja na majengo na mitambo mbalimbali. Kuna Chuo cha Ufundi *(VETA)* ambacho kinasimamiwa na Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, Shule ya Sekondari kidato cha tano na sita ambayo inasimamiwa na Wizara ya Elimu n Utamaduni na eneo hili pia lina Shule ya Msingi inayosimamiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa. Vile vile, ipo zahanati inayosimamiwa na Uongozi wa Kituo. Miundombinu ya maji safi na maji taka, mitambo ya maji taka, barabara, umeme na majengo pamoja na utunzaji wa makaburi ya wapiganaji vinashughulikiwa na uongozi wa kituo ambapo Mtendaji Mkuu ni Mkurugenzi wa Kituo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bakari Muhema Mbonde, Mbunge wa Rufiji, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, Kituo cha Maendeleo Dakawa kilikabidhiwa kwa Serikali ya Tanzania Septemba, 1992 na hayati Oliver Tambo, ambaye alikabidhi kwa niaba ya *ANC* kama ishara ya urafiki na udugu kati ya Tanzania na Chama cha *ANC* cha Afrika Kusini kuwa Taasisi ya Ukumbusho. Kituo hiki kinasimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa ajili ya uratibu na mahusiano, ipo Kamati ya uendeshaji inayojumuisha Makatibu Wakuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Kilimo na Chakula, Elimu na Utamaduni, Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu na Afya. Kituo kimeendelea kutoa huduma zote ambazo zilikuwepo kulingana na uwezo uliopo.

(c) Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa kituo hakipotezi maana na historia katika suala la ukombozi wa Bara la Afrika hususan Afrika Kusini, Serikali pamoja na uhaba wa fedha imeendelea kukihudumia kituo. Mwaka 2003 Serikali iliunda Kamati Maalum, kuangalia jinsi gani ya kukiimarisha na kuboresha huduma. Kamati imetoa mapendekezo yake Serikalini na yanaendelea kufanyiwa kazi. Nia ya Serikali ni kuboresha huduma zilizopo katika kituo hiki na kuzifanya ziweze kutolewa kwa ubora unaostahili.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali itaendelea kuboresha huduma za kituo hiki kwa bajeti ya kila mwaka na kwa misaada ya wafadhili ambao watajitokeza kuunga mkono jitihada hizo ili kuona kinapata mafanikio makubwa kwa faida ya wadau wote.

**MHE. BAKARI M. MBONDE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Sasa hivi kuna kampeni kwamba kila Taasisi iliyopo maeneo fulani imilikishwe katika eneo hilo. Je, isingekuwa vizuri Taasisi hiyo ikaendeshwa kwa utaratibu ule wa Shirika la Elimu Kibaha? *(Makofi)*

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani kudhibiti au kuzuia uporaji wa ardhi katika eneo hili la Dakawa ambao unafanywa hivi sasa? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI:** Mheshimiwa Spika, wazo la kukifanya kituo hiki kiendeshwe kama ilivyo *Kibaha Education Center* ni wazo zuri na ni miongoni mwa mapendekezo ambayo yametolewa na ile Kamati iliyoundwa mwaka 2003. Lakini kama nilivyosema, mapendekezo haya yamewasilishwa na hivi sasa yanafanyiwa uchambuzi ili angalau tupate muafaka na ikiwezekana kama wazo hilo litakubalika, lazima tutaleta hapa Bungeni ili kituo hicho kitungiwe sheria kama ilivyo *Kibaha Education Center.* Kwa hiyo, wazo nimelipokea, lakini tusubiri bado kazi hii inakamilishwa vizuri na Serikali.

Mheshimiwa Spika, juu ya kuvamia eneo, ni kweli baadhi ya Wananchi wamekuwa wanalima na wanafanya shughuli zao katika eneo hili. Eneo hili ni kubwa sana, haliko *fenced* na jitihada mbalimbali zinafanywa. Lakini yapo mapendekezo kadhaa ya kuzuia eneo hili lisiendelee kuporwa, nayo yako katika hiyo Kamati na wakati muafaka utakapofika, tutampa Mheshimiwa Mbunge ili aweze kujua mikakati mbalimbali ambayo itakubaliwa na Serikali kwa ajili ya kuzuia uvamizi huu usiendelee tena.

Na. 50

**Mikopo kwa Akina Mama na Vijana**

**MHE. JAMES P. MUSALIKA** aliuliza: -

Kwa kuwa Halmashauri za Wilaya, Miji na Manispaa na Jiji kwa muda mrefu zimekuwa zikitoa mikopo kwa vikundi mbalimbali vya akina mama na vijana na kwamba mikopo hiyo imekuwa na manufaa kwa jamii ya Kitanzania:-

(a) Je, Halmashauri ya Wilaya ya Geita ilitoa fedha kiasi gani (kwa takwimu) kwa vikundi vya akina mama na vijana katika miaka ya fedha ya 2002/2003 na 2003/2004?

(b) Je, Halmashauri hizo zinapaswa kisheria kutoa fedha kiasi gani na kwa asilimia ngapi ya bajeti yake kwa ajili ya mikopo ya vikundi hivyo?

(c) Je, ni hatua gani zinazostahili kuchukuliwa na ni nani wa kuchukua hatua hizo iwapo Halmashauri hizo zinashindwa kutoa/kutenga fedha kwa ajili ya mikopo hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa James Musalika, Mbunge wa Jimbo la Nyang'hwale, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, wakati nikijibu swali Na. 1717 la Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mbunge wa Viti Maalum, tarehe 02 Julai, 2002 katika Mkutano wa Nane wa Bunge lako Tukufu, nililieleza Bunge lako Tukufu kwamba, mwaka 1995 Serikali ilitangaza nia ya kutaka kuboresha hali ya vijana pamoja na wanawake kiuchumi. Hivyo, wakati huo Serikali ilichukua jukumu la kuziagiza Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini kutenga asilimia 10 ya mapato ya Halmashauri kila mwaka ili fedha hizo ziweze kutumika kuwakopesha wanawake na vijana ili waweze kuendesha miradi ya kujiongezea kipato. Fedha zilizotengwa na Halmashauri ya Wilaya ya Geita kwa mwaka 2002/2003 na 2003/2004 ni Sh.8,000,000/= kama ifuatavyo:-

- Mwaka 2002/2003 Halmashauri ya Geita ilitenga Sh.5,000,000/= na mwaka 2003/2004 Halmashauri hiyo ilitenga Sh.3,000,000/=. Hata hivyo, fedha zilizopokelewa kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto zilikuwa ni jumla ya Sh.12,400,000/=. Vile vile, kulikuwepo na mapato mengine yaliyotokana na mikopo iliyokuwa imetolewa siku za nyuma yenye jumla ya Sh.39,600,000/=.

- Vikundi vilivyonufaika na mikopo hiyo ni kama ifuatavyo: Mwaka 2002/2003 vikundi 57 vyenye wanachama 285. Mwaka 2003/2004 vikundi 64 vyenye wanachama 320. Kama nilivyosema, jumla ya fedha zote zilizokopeshwa ni Sh.39,600,000/=. Fedha hizi ni nyingi lakini hii imetokana na maelezo niliyoyatoa kwamba, kuna mchango wa Wizara, lakini vile vile kuna fedha zilizorejeshwa kutokana na mikopo ya siku za nyuma.

(b) Mheshimiwa Spika, Halmashauri zinatakiwa kuchangia kiwango hicho cha asilimia 10 ya mapato yake kwenda katika mfuko huo kila mwaka ili fedha hizo ziweze kukopesha vikundi vya akina mama na vijana na hivyo kuwasaidia kuwapunguzia umaskini kutokana na shughuli za kiuchumi watakazokuwa wanazifanya.

(c) Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu (a), agizo la Serikali la kuzitaka Halmashauri kuchangia asilimia 10 ya mapato yake katika Mfuko wa Wanawake na Vijana, lengo lake ni kuzisaidia Halmashauri kupunguza hali ya umaskini wa Wananchi wake. Agizo hili ni sehemu ya bajeti iliyopitishwa na inayopitishwa na Halmashauri kila mwaka na utekelezaji wa bajeti hiyo husimamiwa na Halmashauri yenyewe kupitia Baraza la Madiwani na Kamati zake, ambapo kwa bahati nzuri na sisi Wabunge ni Wajumbe. Kutokana na msingi huu, Baraza la Madiwani ndiyo lenye jukumu la kwanza la kuhakikisha bajeti yake inatekelezwa kikamilifu kwa mujibu wa kifungu cha 43(5) cha Sheria Namba 9 ya mwaka 1982 ya fedha za Serikali na kumuwajibisha Mtendaji Mkuu wake pale anaposhindwa kufanya hivyo bila sababu za kuridhisha.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake katika swali hili, lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa yeye mwenyewe amekiri kwamba pesa inayotolewa ni kidogo sana, zile za Halmashauri pamoja na Wizara zile mbili, Wizara ya Kazi, Maendeleo ya

Vijana na Michezo pamoja na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwenye mikopo hii ya vijana na akina mama mithili ya mpita njia anavyotoa senti kidogo kwa omba omba maskini mtaani na kwa kuwa pesa hii huwa inakwisha wakati wanavikundi wanafuatilia maandalizi yake ikiwemo nauli, ujazaji wa fomu, kufungua akaunti na pesa ya kujikimu, wanapoanza mradi pesa inakuwa imekwisha. Je, Serikali itatamka hapa kwamba Wizara zinazohusika pamoja na Halmashauri watekeleze agizo hili la kuviwezesha vikundi hivi? *(Makofi)*

(b) Kwa kuwa sababu zilizotajwa kwenye swali langu la kwanza la nyongeza ni kwamba pesa hii huwa inaisha kabla mradi haujaanza na kwa kuwa mikopo hii sasa haiwezi kulipika, je, Serikali iko tayari kusamehe madeni yote haya ili tuanze upya kujipanga vizuri kama ambavyo Waziri wa Fedha anasamehe madeni ya Serikali Kuu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, Serikali ilibuni utaratibu huu baada ya kuombwa na Waheshimiwa Wabunge kwa nia nzuri sana. Juhudi zinazofanywa na Serikali Kuu ni kweli zinaweza kuonekana ni ndogo, lakini huo ndiyo uwezo wa Serikali Kuu kwa sasa kwa maana ya mchango wake. Lakini iko rai pale ambayo nafikiri ni nzuri kwamba, pengine utaratibu unaotumika hadi mtu anapopata mkopo ungeangaliwa ili usiwe mrefu kiasi cha kufanya fedha hiyo kupoteza maana yake. Hili tutalizingatia na tutatoa maagizo kuweza kusahihisha jambo hilo mara moja.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni kusamehe. Hii si mara ya kwanza rai hii inatolewa, lakini mara zote tumekuwa tunasema fedha hizi zilikopwa, ni fedha ya umma, ni vizuri zikalipwa. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, hata Nyang’hwale wamejitahidi sana. Katika fedha hizi ambazo nasema wamekopeshwa, hadi sasa tayari wamekwishalipa kiasi cha Shilingi milioni 20. Sasa haiwezekani mmoja tukakubali arejeshe mwingine tumsamehe. Wote ni lazima wawajibike kikamilifu. *(Makofi)*

**MHE. MARIAM SALUM MFAKI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Serikali Kuu sasa inatoa ruzuku kwa ajili ya kufidia mapato ya Halmashauri yaliyokuwa yakikusanywa. Je, Serikali Kuu iko tayari kutoa *10 percent* ya ruzuku hiyo na kuingiza katika mfuko huo wa akina mama na vijana? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, wazo ni zuri, lakini kwa kweli tunachofanya ni kwamba, tunazunguka pale pale kwenye tatizo ambalo bado hatujalipatia ufumbuzi. Kwa hiyo, hata kama Serikali utaiomba itoe *10 percent* ya fedha za ruzuku ambayo hivi sasa tunatoa, maana yake tuta-*minus similar 10 percent* kutoka kwenye mapato ambayo Halmashauri ingepata. Ndiyo maana nasema tunachofanya ni mzunguko. Nadhani rai kubwa hapa ni uwezo tu wa Serikali bado ni mdogo, punde tukipata uwezo jambo hili nadhani kila mmoja analitakia mema.

Na. 51

**Ukarabati wa Hospitali ya Wilaya ya Korogwe**

**MHE. JOEL N. BENDERA** aliuliza: -

Kwa kuwa kwa muda mrefu kumekuwepo na ahadi ya Serikali ya kuikarabati na kuiboresha Hospitali ya Wilaya ya Korogwe (Magunga) kuwa ya kisasa hasa ikizingatiwa kuwa ilijengwa mwaka 1954; na kwa kuwa wodi hazitoshi kulingana na idadi ya wagonjwa na hivyo kufanya wagonjwa wa kifua kikuu kuchanganywa na wagonjwa wengine wa kawaida na vifaa vingi ni vikuukuu, hakuna chumba cha kuhifadhia maiti; na kwa kuwa hospitali hiyo pia inawahudumia mara kwa mara wagonjwa wengi wanaopata ajali katika barabara kuu ya Dar es Salaam, Arusha, Tanga na Arusha kwenda Tanga, Arusha kwenda Morogoro, Mbeya, Dodoma na kadhalika:-

(a) Kwa kuzingatia matokeo mbalimbali ya ajali na huduma zinazotolewa na hospitali hiyo. Je, sasa ni wakati muafaka kwa Serikali kutimiza ahadi yake ya kuikarabati na kuiboresha hospitali hiyo iliyoko katikati hasa ikizingatiwa malalamiko mengi ya majeruhi wanaopata ajali wanaopelekwa katika hospitali hiyo kwa kupata huduma hafifu?

(b) Kwa kuzingatia kuwa Mji wa Korogwe sasa umepata hadhi ya Mji *(Town Council)* na uwezo wa kifedha wa Halmashauri yetu, je, Serikali haioni kwamba hicho pia ni kigezo kikubwa cha kusaidiana na nguvu za Wananchi ili kuikarabati na kuiboresha hospitali hiyo muhimu inayotegemewa na Watanzania wote wanaopita kwenye barabara kuu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joel N. Bendera, Mbunge wa Korogwe Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Wilaya ya Korogwe ilijengwa mwaka 1952 ikiwa na majengo yafuatayo: Wodi 4 za kulaza wagonjwa, ikiwemo wodi ya magonjwa ya kuambukiza, zenye uwezo wa kulaza wagonjwa 122, jengo la upasuaji, jengo la kufulia, jengo la utaalam lenye sehemu ya mapokezi, chumba cha *X-ray*, maabara na ofisi za utawala.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inazo taarifa juu ya matatizo yanayoikabili hospitali hiyo na ndiyo maana imekuwa ikiifanyia hospitali hii ukarabati wa mara kwa mara ili kukidhi mahitaji ya wagonjwa kama ifuatavyo: -

- Mwaka 1966 wodi ya watoto ilijengwa na kufanya hospitali kuongeza wodi na vitanda kufikia 142;

- Mwaka 1988 mfumo wa maji safi na maji taka wa hospitali ulifanyiwa ukarabati kwa msaada wa Serikali ya Ujerumani *(GTZ)* na fedha za Halmashauri;

- Mwaka 1999 hospitali ilipatiwa vifaa vya uchunguzi wa magonjwa, *X-ray* ya kisasa, *ultra sound* na jenereta kubwa ya umeme; na

- Mwaka 2003 Hospitali ya Wilaya ya Korogwe ilikarabatiwa kwa Mfuko wa pamoja wa Afya *(Health Basket Fund)*. Majengo yaliyokarabatiwa ni pamoja na jengo la upasuaji, wodi ya wazazi, wodi ya wanaume, jengo la utawala, jengo la kitengo cha meno na kifua kikuu na mfumo wa maji taka. Jumla ya Sh.29,767,533/= zilitumika katika ukarabati huo.

(c) Mheshimiwa Spika, kutokana na Wilaya ya Korogwe kuingizwa kwenye mpango wa maboresho ya afya tangu mwaka 2003, ukarabati wa ujenzi wa majengo ya hospitali utafanyika mwaka hadi mwaka kwa kutumia Mfuko wa Afya ili iweze kuwahudumia watu wengi zaidi wakiwemo wanaopata ajali. Aidha, watumishi watapatiwa mafunzo na vifaa vya kisasa vitanunuliwa. Kwa mwaka 2004/2005 jumla ya Sh.21,500,000/= zitatolewa na Wizara ya Afya chini ya mpango wa majaribio ya uwiano wa kutibu kifua kikuu na UKIMWI na zitatumika kwa ajili ya ujenzi wa maabara. Kadhalika Wilaya ya Korogwe imeandaa mpango wa afya wa miaka mitatu (2004 - 2006) utakaofadhiliwa na Benki ya Ujerumani *(KfW).* Chini ya mpango huu, *mortuary* ya kisasa itajengwa. Aidha, patakuwepo na ujenzi wa wodi za ziada kwa ajili ya wagonjwa.

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza na napenda nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri yenye matumaini. Nina swali moja tu dogo la nyongeza.

Kwa kuwa hospitali nyingi za Wilaya ikiwemo ya Korogwe zimepatiwa *ultra sound* pamoja na *X-ray,* lakini lipo tatizo sugu la kukosa madaktari, ambao ndiyo wanatakiwa wafanye kazi katika hospitali hizi ikiwemo ya Korogwe. Je, Mheshimiwa Waziri atatuambia nini kuhusiana na suala hili ambalo ndiyo tatizo sugu kwa Hospitali ya Korogwe ambapo madaktari wa upasuaji ni wachache hasa pamoja na wataalam wa mifupa kutokana na ajali ambazo zinajitokeza pale? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nimhakikishie Mheshimiwa Bendera kwamba, si majibu ya matumaini tu, hivi tunavyojibu swali hili tayari Wajerumani wapo Korogwe sasa hivi kwa ajili ya mradi huo. Kwa hiyo, ni kitu cha uhakika kabisa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pili, ni hili la wataalam kwa ajili ya *X-rays.* Tunakubali tatizo lipo na limetokana na nia nzuri kwamba, *X-rays* hizi hasa *ultra sound* zilipoletwa wafadhili walitaka iwepo *special training* kutoka kwa wataalam watakao-*manage* vifaa hivi na ndiyo inavyofanyika hivi sasa. Kwa hiyo, inawezekana baadhi ya

Wilaya zitachelewa kidogo, lakini tunaomba mfanye subira wakati zoezi hilo linakamilishwa.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa karibu kabisa na Hospitali ya Magunga ambayo ilikuwa hasa kwa ajili ya wafanyakazi wa mkonge, kuna Hospitali ya Bumbuli ambayo nayo ilijengwa miaka ya 1920 na ilikuwa inatoa huduma hata kwa wagonjwa wa nchi jirani, lakini sasa hivi uwezo ilionao hautumiki kwa sababu dhehebu linaloangalia hospitali hiyo halina uwezo wa kuweza kupunguza gharama za dawa. Je, Serikali itakubaliana na mimi kwamba, umefika wakati ile sera ya kuwa na *District Designated Hospitals* ina haja ya kuangalia upya ili kuondoa ile *'D'* ya kwanza na kubakiza *'D'* moja iwe *Designated Hospital?* Hii ni kwa maana ya kwamba, Jimbo la Bumbuli siyo Wilaya, lakini lina watu 150,000 kwa hiyo hospitali hiyo ingeweza kupata msaada ikahudumia watu vizuri. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, juzi nilijibu swali moja ambalo nadhani kwa kiasi fulani linaweza kabisa likamsaidia Mheshimiwa Shellukindo. Serikali haikatai hata kidogo kuwa na hospitali ambazo zinapata msaada kutoka Serikali Kuu. Tulichosema tu ni kwamba, ule utaratibu wa maombi ufuatwe ili Wizara ya Afya iweze kubaini mambo yote ya msingi. Kwa hiyo, naomba nikutie moyo, hili jambo liwasilishwe kwenye Wizara ya Afya, walitazame ili tuone tutakavyoweza kusaidiana na wewe.

Na. 52

**Utoaji wa Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)***

**MHE. DR. MILTOM M. MAHANGA** aliuliza: -

Kwa kuwa nchi jirani za Kenya na Uganda zimepunguza kiwango cha kodi ya ongezeko la thamani *(VAT)* kufikia asilimia 16 - 17: -

(a) Je, Serikali haioni kwamba kuendelea kung'ang'ania asilimia 20 ya kodi hiyo ni kuwaongezea mzigo wafanyabiashara na wenye viwanda na kuwaongezea gharama za uzalishaji, ulipaji wa kodi na hivyo haipanui wigo wa kodi ili kupata walipa kodi wengi na kupunguza mapato ya Serikali?

(b) Je, Serikali imeshafanya utafiti wowote kuona kama ikipunguza kiwango cha kodi ya *VAT* kutawezesha kupanua wigo wa kodi na kuondoa ukwepaji wa kodi na hivyo kupata mapato makubwa zaidi kuliko ilivyo sasa?

(c) Je, Serikali haioni kwamba tofauti kati ya viwango vya kodi ya *VAT* kwa nchi za Afrika Mashariki haiwezi kuleta uwiano mzuri wa kibiashara kati ya nchi hizo zenye ushirikiano wa kibiashara?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Milton Makongoro Mahanga, Mbunge wa Ukonga, lenye sehemu (a), (b) na (c), naomba kutoa maelezo yafuatayo: -

(a) Mheshimiwa Spika, kodi ya ongezeko la thamani ni kodi inayolipwa na mlaji anaponunua au kulipia bidhaa au huduma kutoka kwa mfanyabiashara aliyesajiliwa ili kukusanya kodi hii. Kwa hiyo, kodi hii haiathiri faida inayotokana na biashara au mauzo husika.

(b) Mheshimiwa Spika, mzigo halisi wa kodi katika uchumi hupimwa kwa kiwango cha jumla ya kodi inayokusanywa kama sehemu ya Pato la Taifa. Kwa nchi yetu, kiwango hicho ni takriban asilimia 13. Kwa maneno mengine, Watanzania hulipa wastani wa senti 13 kama kodi kwa kila Shilingi moja wanayoipata. Kiwango hiki ni cha chini ikilinganishwa na nchi jirani. Kwa mfano, makusanyo ya kodi nchini Kenya ni zaidi ya asilimia 22 ya Pato la Taifa, wakati Malawi imefikia asilimia 16.

(c) Kodi ya ongezeko la thamani ni kodi yenye wigo mpana na usawa zaidi kwa walipakodi na ina *distortions* kidogo zaidi katika uchumi kuliko kodi nyingine nyingi. Kwa hiyo, wataalam hupendekeza kutumia *VAT* kupanua wigo wa kodi kuliko kutumia aina nyingine za kodi.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa mchango wa *VAT* katika mapato ya Serikali ni mkubwa kuliko kodi nyingine yoyote ile. Kwa mfano, katika mwaka huu wa fedha wa 2003/2004, inatarajiwa kuwa mchango wa kila aina ya kodi utakuwa kama ifuatavyo: *VAT* asilimia 29, kodi ya mapato asilimia 22, ushuru wa forodha asilimia 9, ushuru wa bidhaa asilimia 16, kodi nyinginezo asilimia 14 na mapato yasiyo ya kodi asilimia 10.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Milton Makongoro Mahanga, Mbunge wa Ukonga, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo: -

(a) Kiwango cha asilimia 20 hakiathiri ushindani wa wafanyabiashara wa Tanzania kwa kuwa kodi hiyo hulipwa na walaji. Aidha, kiwango cha jumla ya kodi nchini Tanzania ni kidogo kuliko nchi jirani. Kwa mfano, nchini Kenya na Malawi, kama nilivyoeleza hapo awali.

(b) Mheshimiwa Spika, tafiti zilizofanywa zimeonyesha kwamba, mapato ya Serikali yatapungua kwa Shilingi bilioni 59 iwapo kiwango hicho kitapunguzwa kutoka asilimia 20 hiyo ya sasa hadi asilimia 18.

(c) Mheshimiwa Spika, tofauti katika viwango vya *VAT* haiathiri ushindani wa viwanda vyetu kwa kuwa wazalishaji hurejeshewa *VAT* yote iliyolipwa wanapouza

bidhaa nje ya nchi na kufanya bei za kuuzia nje kutojumuisha kodi. Aidha, bidhaa zote zinazoingizwa kutoka nje hutozwa *VAT* ya asilimia 20 sawa na bidhaa za hapa nchini.

**MHE. DR. MILTON M. MAHANGA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda niulize maswali madogo mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: -

(a) Kwa kuwa katika jibu lake la msingi ameeleza kwamba *VAT* ikipunguzwa kwa asilimia 2 tu kutakuwa na punguzo la Shilingi bilioni 59 na hili limefanyiwa utafiti. Je, anaweza akalipatia Bunge hili au mimi nakala ya utafiti huo ili na sisi wataalam wengine tuuchambue? *(Makofi)*

(b) Kwa kuwa makusanyo ya Pato la Taifa kuwa madogo, asilimia 13 siyo kutokana na *VAT* au kodi zingine, lakini kuna sababu nyingine kama ufanisi katika uendeshaji wa Serikali pamoja na kutotilia umuhimu wa kilimo kama Sekta ya kukuza uchumi. Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kwamba njia ya kuongeza Pato la Taifa siyo kuacha *VAT* kwenye asilimia 20, lakini ni kuangalia Sekta nyingine? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU):** Mheshimiwa Spika, tutampatia Mheshimiwa Dr. Mahanga nakala ya mahesabu yetu ya utafiti jinsi tulivyopata hiyo asilimia 2 kwamba tutapoteza kiasi cha Shilingi milioni 59.

Ninakubaliana naye kwamba, kweli ufanisi katika uendeshaji wa Serikali unaweza ukatupunguzia mapato na ndiyo maana tunapata asilimia 13. Lakini vile vile, nakubaliana naye kwamba, tunaweza kuangalia Sekta nyingine vile vile ili ziweze kutuzidishia mapato yetu ya kodi na hilo siyo kwamba tutalianza, hilo tumelianza toka mwaka 1996, ndiyo maana kila tunapoendelea mbele tunakuwa tunapunguza baadhi ya kodi baada ya kutazama hali yenyewe kama tukipunguza kodi hii na kama tukichukua zaidi upande huu hali yetu ya kifedha na mapato yetu yatakuwaje.

Kwa hiyo, hiyo bado inaendelea na ndiyo maana tunasema kila hali itakapoturuhusu tutakuwa tutaendelea kufanya mambo yakiwa mazuri zaidi na kupanua wigo wa kodi kuwa mkubwa zaidi ili kupata mapato makubwa zaidi.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa hatuna sera ya kumlinda mlaji; na kwa kuwa *VAT* ndiyo ambayo inamwumiza mlaji; na kwa kuwa bado hatujawa na utaratibu mzuri wa ku-*control price* zetu kwa mfano mafuta yanapopanda bei anayeumia ni mlaji:-

(a) Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba kuendelea kuing'ang'ania thamani hii ya asilimia 20 ya *VAT* ni kumwumiza mlaji na hasa tukizingatia kwamba sasa hivi kutokana na ushirikiano baina ya *East African Community* tayari kutakuwa na bidhaa ambazo hazitatozwa ushuru? *(Makofi)*

(b) Haoni kwamba kutegemea tu *VAT* na kumwumiza mlaji si sera nzuri ya kukusanya mapato? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU):** Mheshimiwa Spika, ni kweli hakuna sera ya kumlinda mlaji, lakini Waheshimiwa Wabunge itakumbukwa kwamba, asilimia 20 ya *VAT* imekuja baada ya kuondolewa *sales tax* ni kama imegeuzwa tu. Kwa hiyo, siku zote hii kodi ya mlaji ilikuwepo na kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, tukiiondoa kwa sasa hivi haiwezi kutuletea tija yoyote, itatuletea hasara katika pato letu la nchi.

Tanzania ukilinganisha na nchi zetu za jirani kwa mfano, kuna mambo mengi usichukulie kwamba ni *VAT* tu ambayo ni kodi anayotozwa mwananchi. Kwa mfano, kwenye *corporation tax,* Tanzania tuna viwango vinane wakati Kenya wana viwango 10 na Uganda viwango 11. *Individual taxes,* Tanzania tuna viwango 3, Kenya 4 na Uganda ni 4.

Hivyo hivyo utakuta *tax* zingine mbalimbali. Kwa hiyo, hatuangalii *VAT* peke yake, lazima tuangalie kodi kwa ujumla wake. *(Makofi)*

Na. 53

**Mfumo wa Maji na Mahitaji - Tunduma**

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA** aliuliza: -

Kwa kuwa mtandao wa maji katika Mji wa Tunduma ni mdogo ikilinganishwa na idadi kubwa ya wakazi wake ambao ni zaidi ya mara saba ya wakazi waliokuwepo wakati mfumo huo ulipowekwa na kwa kuwa hapakuwa na michoro sanifu, hivyo baadhi ya nyumba zimejengwa juu ya mabomba: -

(a) Je, Serikali imekusudia kufanya nini katika kurekebisha mfumo huo wa maji ili kukidhi mahitaji ya sasa?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka mashine *(pump)* kubwa za kusukuma maji ya kutosha kutokana na hali halisi ya mji ilivyo sasa?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mbunge wa Mbozi Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, mfumo wa maji uliopo Tunduma ni mdogo na ulisanifiwa mwaka 1957. Kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2002, Mji wa Tunduma una wakazi wapatao 32,000 ikiwa ni karibu mara saba ya watu waliokuwepo wakati wa usanifu wa huduma ya maji kwa

mji huo. Ongezeko la wakazi limesababisha matandao uliopo kukidhi asilimia 25 tu ya mahitaji yote ya maji.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweza kuboresha huduma ya maji katika Mji wa Tunduma ili kupunguza adha hiyo kama ifuatavyo: -

(i) Kati ya mwaka 1999 na 2003 Serikali iligharamia uchimbaji wa visima virefu viwili. Kisima kilichochimbwa mwaka 1999 kina uwezo wa kuzalisha meta za ujazo 16 kwa saa na kisima cha pili ambacho uchimbaji wake ulikamilika tarehe 13 Juni, 2003 kina uwezo wa kuzalisha meta za ujazo nane kwa saa. Visima hivyo viwili vina uwezo wa kutoa meta za ujazo 432 kwa siku. Aidha, Serikali ilinunua pampu mbili za kusukuma maji katika mwaka wa fedha wa 2003/2004. Serikali ilitenga Shilingi 5.5 milioni kwa ajili ya kununua pampu nyingine. Pampu hiyo inatarajiwa kufungwa Septemba, 2004 na upatikanaji wa maji unatarajiwa kupanda kutoka asilimia 27 ya sasa hadi asilimia 35 ya mahitaji baada ya pampu hiyo kufungwa;

(ii) Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, imegharamia upimaji na usanifu wa upanuzi wa mtandao wa maji ya usambazaji unaohusisha sehemu kubwa ya Mji wa Tunduma. Serikali imewaagiza wananchi waliojenga nyumba zipatazo 34 juu ya mabomba, kubomoa nyumba hizo, jambo ambalo limeanza kutekelezwa;

(iii) Katika mwaka 2004/2005, Serikali imetenga Shilingi milioni 20 kwa ajili ya kununulia pampu kwa ajili ya kisima cha tatu. Kisima hicho kitaweza kuongeza uzalishaji wa maji hadi kufikia asilimia 43 ya mahitaji;

(iv) Serikali imekamilisha uundaji wa bodi itakayosimamia Mamlaka ya Maji ya Mji mdogo wa Tunduma. Bodi za maji zimepewa madaraka kamili ya kukusanya mapato yatokanayo na mauzo ya maji na kuyatumia mapato hayo kwa kuboresha huduma ya maji; na

(v) Wilaya ya Mbozi ni moja ya Wilaya 38 ambazo zitaanza kutekeleza programu ya usafi wa mazingira vijijini unaofadhiliwa na Benki ya Dunia. Utekelezaji wa programu hiyo utaanza mwaka huu wa fedha. Nawashauri wananchi wa Tunduma kupitia Halmashauri yao ya Mbozi, kuweka kipaumbele cha uimarishaji wa huduma ya maji Mjini Tunduma katika mipango yake mara utekelezaji wa programu hii utakapoanza.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali haina mpango wowote wa kuweka pampu kubwa za kusukuma maji Mjini Tunduma. Pampu zinazofungwa ni zile zinazolingana na maji yaliyopo kwenye visima. Tatizo lililopo ni kukosekana kwa vyanzo vyenye maji ya kutosha kukidhi mahitaji ya maji. Visima vyote vilivyopo vina maji kidogo kutokana na ukanda unaotumiaka hivi sasa kutokuwa na maji mengi.

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri na yenye matumaini. Ninaomba kuuliza maswali yafuatayo:-

(a) Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa tayari kwenda na mimi baada ya Bunge au wakati wowote, ili aweze kuona hali halisi ilivyo kwa sababu maji yenyewe anayosema hayapo na pampu yenyewe ni pampu hewa tu kwa sababu hakuna maji?

(b) Kwa kuwa sisi tunajua vyanzo vya maji vilipo, je, wako tayari kama Serikali, kutokana na jitihada ambazo tunaona Waziri anazifanya, kwenda ku-*survey* maeneo ya Mwaka na Chipaka ambako tunajua kuna maji mengi sana ili tupate vyanzo vizuri na vikubwa vya maji? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, kwanza kwenda Tunduma nina hakika Mheshimiwa Eliachim Simpasa, anakumbuka nilishafika Tunduma nikaona vyanzo vyote vya maji, nikaona ujenzi wa tanki ambalo lilimalizika katika programu ya kwanza. Kwa hiyo, ningemwomba Mheshimiwa Mbunge, avute subira kwa sababu ufungaji wa pampu na ripoti ambayo inatengenezwa na wataalam ya kutafuta chanzo cha pili cha maji itakapokamilika, nina hakika tutashirikiana naye, kuona mambo yote yanakamilika ili kutatua tatizo la maji la Mji Mdogo wa Tunduma.

Kuhusu vyanzo ambavyo amevieleza nina hakika vinawezekana kabisa kuwa vinaeleweka kwa Ofisa wa Maji wa Wilaya. Hivyo Ofisa wa Maji wa Wilaya kwa vile anahusishwa tunapopeleka watendaji wetu kufanya kazi ya uchunguzi, atatupatia taarifa hiyo ili itumike katika programu endelevu ya kutoa maji kwa ajili ya Mji Mdogo wa Tunduma. *(Makofi)*

Na. 54

**Ufugaji Bora wa Kisasa**

**MHE. ERNEST G. MABINA (k.n.y. MHE. JACOB D. SHIBILITI)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imekuwa ikihimiza ufugaji bora na wa kisasa kwa manufaa ya wafugaji na Taifa kwa ujumla:-

(a) Je, ni ng’ombe wangapi huchinjwa katika Jiji la Dar es Salaam na ni Mkoa gani unafuatia kwa wingi wa ng’ombe wanaochinjwa?

(b) Kwa kuwa maziwa ni zao linalotokana na mifugo hususan ng’ombe na vile vile Serikali imekuwa ikisisitiza unywaji wa maziwa, je ni shule ngapi zinanufaika na unywaji maziwa Mkoani Mwanza hasa ikizingatiwa kuwa *Mabuki Farm* imezungukwa na shule?

(c) Je, ni kiasi gani cha ngozi kimeuzwa kwenye soko la nje ya nchi na Taifa limepata shilingi ngapi?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Jacob Dalali Shibiliti, Mbunge wa Misungwi, swali lake lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kiasi cha ng'ombe wanaochinjwa katika Jiji la Dar es Salaam, wanakadiriwa kuwa 250,000 kwa mwaka, yaani wastani wa ng'ombe 685 kwa siku. Hata hivyo, kutokana na kukosekana kwa machinjio ya kisasa, idadi kamili ya ng'ombe wanaochinjwa kwa siku inawezekana ikawa kubwa zaidi. Mkoa unaofuatia Jiji la Dar es Salaam kwa uchinjaji wa ng'ombe ni Mkoa wa Mwanza, ambao unakadiriwa kuchinja ng'ombe 96,360 kwa mwaka ikiwa ni wastani wa ng'ombe 264 kwa siku. Hii inaonyesha kwamba, mkoa unaofuata wa Mwanza, wananchi wanakula nyama nyingi zaidi kuzidi wakazi wa Dar es Salaam

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Serikali imekuwa ikisisitiza na kuhamasisha unywaji wa maziwa yanayozalishwa hapa nchini kupitia wiki ya maziwa na mpango wa kuhamasisha unywaji wa maziwa shuleni. Taarifa tulizonazo zinaonyesha kuwa katika shule zinazozunguka shamba la kuzalisha mitamba la Mabuki, mpango wa kuhamasisha unywaji wa maziwa mashuleni, bado haujaanza kama ilivyo kwenye shule zilizopo Mikoa ya Arusha na Kilimanjaro, ambako wadau wakishirikiana na wazazi na Halmashauri za Wilaya zao, wamekuwa mstari wa mbele katika kuleta mafanikio yaliyopo.

Mheshimiwa Spika, jukumu la kuhamasisha unywaji wa maziwa na lishe bora ni letu sote, hivyo namshauri Mheshimiwa Mbunge, ashirikiane na wazazi na wadau mbalimbali wakiwemo Halmashauri za Wilaya, kuhamasisha unywaji wa maziwa sio katika shule zinazolizunguka Shamba la Mabuki tu, bali katika jimbo lake lote la Misungwi. *(Makofi)*

(c) Mheshimiwa Spika, ngozi ndilo zao kubwa litokanalo na mifugo linalouzwa nje ya nchi na kuipatia Serikali fedha za kigeni. Katika kipindi cha mwaka 2002/2003, jumla ya vipande, 1,300,000 vya ngozi za ng'ombe, vipande 600,000 vya ngozi za mbuzi na vipande 300,000 vya ngozi za kondoo, viliuzwa na kulipatia Taifa jumla ya Sh. 4.6 bilioni.

Mheshimiwa Spika, kiasi hiki cha fedha kimetokana na mauzo ya ngozi ghafi. Serikali ingeweza kujipatia mapato makubwa zaidi kwa kuuza idadi hii ya ngozi kama zingesindikwa. Ni azma ya Serikali kufufua zao na sekta ya ngozi kwa lengo la kuuza ngozi zilizoongezewa thamani ili sekta hii ya ngozi itoe mchango mkubwa zaidi katika kutupatia Pato la Taifa.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja kama ifuatavyo: Kwa kuwa katika jibu lake Mheshimiwa Naibu Waziri, amesema kwamba ngozi ni zao ambalo linategemea kutoa mchango mkubwa katika Pato la Taifa na inaonyesha kwamba viwanda vyote vya ngozi ambavyo viko hapa nchini vimeshabinafsishwa, lakini katika mpango huo unakuta kwamba viwanda vyote havifanyi kazi. Je, Serikali ina mpango gani wa kuvifufua hivyo viwanda tena? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli viwanda vingi vilivyokuwa vya Serikali vilibinafsishwa. Kubinafsishwa kwa viwanda hivyo kulikuja wakati ambapo sera zetu za uuzaji na utayarishaji wa ngozi hazikuwa zinakidhi uzalishaji wa ngozi hapa nchini ili kuleta faida kwa wenye viwanda. Kwa kujua hilo, Wizara yangu ikishirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara, tulianzisha Mfuko Maalum mwaka 2003 wa kuweza kusaidia utayarishaji wa ngozi, ngozi yetu sasa hivi inatayarishwa vibaya sana, inapigwa chapa ovyo, thamani yake ni ndogo na ingekuwa ngozi hiyo ina ubora unaohitajika hata vile vipande ambavyo nimevielezea vingeleta fedha nyingi zaidi licha ya kuwa havikusindikwa.

Kwa hiyo, Serikali inajitahidi na tumeanza kuzungumza na baadhi ya wawekezaji ambao wameanza kuonyesha nia ya kutaka kuvifufua hivyo viwanda. Lakini sera zetu kuhusiana na sekta ndogo ya ngozi haikuwa inakidhi mahitaji hayo ya biashara ya ngozi hapa nchini. *(Makofi)*

Na. 55

**Soko la *AGOA***

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA** aliuliza:-

Kwa kuwa Tanzania ni mwanachama wa biashara katika Soko la *AGOA,* je, ni kwa kiwango gani Watanzania wanafaidika na biashara ya soko hilo?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mbunge wa Mfenesini, kama ifuatavyo:-

Programu ya *African Growth Opportunity Act (AGOA),* ilipitishwa na Serikali ya Marekani na kuanza kutumika tarehe 1 Oktoba, 2000. Lengo la kuu la sheria hii ni kuweka mazingira yatakayoziwezesha nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara, kuuza mazao na bidhaa zao katika Soko la Marekani bila kulipia ushuru na bila viwango *(Duty Free and Quote Free).* Bidhaa zilizoruhusiwa ni pamoja na mazao mbalimbali ya kilimo na maliasilia, ngozi na bidhaa za ngozi, sanaa za mikono na bidhaa za viwanda kama mavazi na nguo.

Tanzania haijafaidika sana na mpango huu wa *AGOA*. Tuliweza kuuza bidhaa za nguo za mavazi kutoka Kiwanda cha *Sun-Flag* cha Arusha zinazokadiriwa kuwa na thamani ya *US$* 900,000 mwaka 2002/2003. Tanzania haijafanikiwa kwa kiwango kikubwa kwa sababu mbalimbali. Kwanza ni kiwango cha chini cha uzalishaji na ubora wa bidhaa kulingana na matakwa ya Soko la Marekani na ushindani uliopo ndani ya soko hilo. Aidha, masharti magumu ya afya *(Sanitary and Physiosanitary - ASP)* kwa mazao

ya kilimo kama matunda, mboga na maua na masharti ya ufungashaji wa bidhaa ni baadhi ya vikwazo vingine.

Pamoja na matatizo niliyoyaeleza, hivi sasa Serikali ina mkakati maalum utakaotuwezesha kufaidika na *AGOA*. Serikali imechukua hatua za makusudi za kuwapatia wawekezaji watakaowekeza wakilenga Soko la Marekani. Wawekezaji waliopatikana hadi sasa ni kutoka Sri-Lanka ambao tayari wameshaanzisha Kiwanda cha Kushona Nguo na tayari wameajiri watu 1,000. Aidha, wameanza kupeleka bidhaa nje zenye thamani ya dola 300,000 za Kimarekani Mei, 2004. Serikali inaendeleza hatua nyingine za kuhamasisha wawekezaji wa namna hii. Kwa mwaka wa fedha wa 2003 ilitenga fedha za dhamana ya mikopo chini ya *Export Credit Guarantee Scheme* na tayari kampuni tano zimejitokeza na karibu wataanzisha viwanda hivyo. Tunazidi kuwahamasisha Watanzania wajitokeze kuanzisha viwanda vya nguo na kutumia fursa hii ya *AGOA* vizuri. Aidha, kupeleka bidhaa mbalimbali katika Soko hili la *AGOA*.

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja kama ifuatavyo: Kwa kuwa bado Watanzania tuna nafasi kubwa ya kushiriki katika soko hili na kwa kuwa hivi sasa bado tuna makampuni ya ndani ambayo yanataka kushiriki katika soko hili. Je, Wizara ya Viwanda na Biashara haioni kwamba wakati umefika, kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais, kuhamasisha makampuni ya ndani badala ya kuhamasisha makampuni ya nje ambayo sasa hivi wao wanakimbia? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kweli Wizara yangu iko tayari kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais na pia Waheshimiwa Wabunge, kuhakikisha tunalitumia hili Soko la *AGOA* vizuri ili kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Spika, kiwanda kimoja cha nguo kwa mfano kinaajiri watu 1,000 mpaka 2,000, viwanda 10 vinaweza vikaajiri watu 20,000. Kwa masikitiko kabisa, naomba kusema kwamba, Serikali imefanya kila inachoweza kuhakikisha kwamba, Watanzania kwanza wanakuwa wa kwanza kujiunga na soko hili. Baada ya kuona ugumu na utata unaovikabili viwanda vilivyopo vya nguo pamoja na Watanzania wengine ambao tunahamasisha tutaona kuna umuhimu wa kuchukua hatua kabisa za haraka kwanza kuleta ule utalaam Watanzania wajue hilo soko likoje ndiyo sababu tukaenda kuchukua watalaam kutoka Sri-Lanka na pili kuwatafutia Watanzania fedha na tunaanzisha mpango wa *Export Credit Garantee Scheme*. Tatu tukaona tuwapatie majengo. Kuna wakati Serikali ilisimamisha uuzaji wa magodauni yote nchi nzima ili anayetaka achukue tuweze kumsaidia pamoja na pesa aanze kiwanda, pamoja na mtaalam, imetangazwa kwenye magazeti imetangazwa kwenye *TV,* lakini Watanzania hamkujitokeza. Sasa nachukua nafasi hii Waheshimiwa Wabunge, nawaomba sana mwaka huu Waziri wa Fedha, ametangaza bado fedha za ku-*guarantee* mikopo zipo. Tunaomba mjitokeze mje tuanzishe viwanda vya nguo kwenye Soko la *AGOA*. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Na. 56

**Mipaka ya Tanzania na Rwanda**

**MHE. BAKARI SHAMIS FAKI** aliuliza:-

Kwa kuwa mpaka wa Tanzania na Rwanda una utata; na kwa kuwa Wanyarwanda hutumia vivuko haramu kuvusha mifugo na kuingiza wahamiaji haramu nchini Tanzania; na kwa kuwa vikosi vya askari wa Rwanda mpakani mwa Tanzania vinaleta hofu kwa watu wetu wanaoishi karibu na hapo:-

(a) Je, Serikali inao mpango gani wa kuondoa utata huo wa mpaka wa Tanzania na Rwanda?

(b) Je, Serikali inaweza kutueleza mikakati yake juu ya kuwaondoa hofu Watanzania wanaoishi mpakani hapo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mbunge wa Ole, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara haina taarifa kwamba kuna utata wa mpaka wa Kimataifa baina ya nchi yetu na Rwanda. Kwa mujibu wa protokali ya mpaka huo, iliyotiwa saini na wawakilishi wa Serikali ya Uingereza na Ubelgiji tarehe 5 Septemba, 1920, Mjini Kigoma, mpaka kati ya Tanzania na Rwanda ni katikati ya mapitio ya Mto Kagera. Huu ni mto mkubwa na hakuna utata wa mtu kuukosea mpaka huo.

(b) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, pamoja na mpaka huo kujulikana vizuri, kuna matukio ya watu kutoka Rwanda kuvuka mpaka na kuiba mifugo na kufanya ujambazi. Kutokana na hali hii, Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, imechukua hatua thabiti za kuongeza ulinzi katika maeneo ya mpaka wetu na Rwanda na pia mpaka wetu na Burundi na *DRC.*

Hatua hizo ni pamoja na Serikali kupeleka Askari Polisi wa ziada katika makambi yote ya wakimbizi, kuimarisha vitendea kazi hasa *radio calls* na magari. Hali kadhalika Vikosi vya Jeshi la Wananchi vimeudhibiti vizuri mpaka huo. Kwa hiyo, napenda kuwahakikishia wananchi wa maeneo hayo kwamba, waendeshe maisha yao bila ya hofu, kwani vyombo vya ulinzi na usalama vipo imara katika maeneo yao na kuhakikisha usalama wao na mali zao. *(Makofi)*

Na. 57

**Watoto Wasio na Makazi**

**MHE. DIANA M. CHILOLO** aliuliza:-

Kwa kuwa idadi ya watoto wasio na makazi inazidi kuongezeka siku hadi siku na wanakuwa na tabia mbaya:-

(a) Je, Serikali ina utaratibu gani juu ya watoto hao ambao tayari wanarandaranda mitaani?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kutolishughulikia tatizo hilo kunachangia kuongeza idadi ya majambazi, vibaka, hasa watakapokuwa wakubwa hivyo ichukue hatua za haraka na za makusudi za kutatua tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali Na. 57 la Mheshimiwa Diana Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwepo kwa tatizo la watoto wanaozagaa mitaani. Serikali inatambua pia kwamba, upo umuhimu mkubwa wa kushughulikia tatizo hili kwa lengo la kuwaepusha watoto hao kujifunza tabia mbaya zinazoweza kuwadhuru wao wenyewe na wananchi wengine.

Mheshimiwa Spika, utaratibu uliopo sasa wa kuwahudumia watoto wa mitaani unaihusisha Serikali kwa upande mmoja na asasi zisizo za Kiserikali kwa upande mwingine. Asasi hizo kwa kushirikiana na Serikali zinafanya kazi zifuatazo pamoja na nyingine: Kuwatambua watoto waliopo mitaani, kutoa ushauri nasaha kwa watoto, kuwapatia matunzo na ulinzi katika vituo wanamotunzwa, kuwaunganisha na wazazi wao pale wanapogundua na kuwapatia elimu.

Serikali kwa upande wake inatekeleza yafuatayo: Kufanya ukaguzi wa vituo vinavyohifadhi watoto hao na kutoa ushauri wa kitaalam wa namna bora ya kuwahudumia watoto hao, utaratibu wa huduma kwa watoto hao, kutoa mafunzo kwa waendeshaji wa vituo vinavyowahifadhi ili wawe na dira sahihi ya utoaji wa huduma hizo kwa watoto.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia uzito wa tatizo hili, Wizara yangu inaandaa mwongozo wa malezi ya watoto wanaozagaa mitaani. Aidha, napenda Bunge lako Tukufu lifahamu kuwa watoto hao hutoka Mawilayani mwetu ambako sisi Waheshimiwa Wabunge, ni wawakilishi wa wazazi wa watoto hawa. Wizara yangu itafarijika endapo Waheshimiwa Wabunge, tutashirikiana na Halmashauri zetu ili kuandaa mazingira rafiki

katika vijiji watokako watoto hawa, ili wasikimbilie mijini. Serikali Kuu peke yake haiwezi kupata ufumbuzi wa tatizo hili bila kushirikisha asasi nyinginezo. *(Makofi)*

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kuuliza maswali kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri, amekiri kwamba watoto hawa wapo na kweli hata Singida Mjini wapo wengi tu. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, amefanya *counselling* kwa watoto wangapi walioko Singida Mjini ili kuweza kuwachukulia hatua wazazi ambao wanakwepa wajibu wao wa kuwalea watoto kwa kujiingiza kwenye ulevi na watoto hao kukosa huduma muhimu hadi kukimbilia Mijini? *(Makofi)*

(b) Kwa kuwa Singida Mjini kuna kituo ambacho kinahudumiwa na *NGO* ya mtu binafsi na Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba wanatoa baadhi katika *NGOs* hizo ambazo hazitoshelezi. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri haioni kwamba kuna haja ya kutoa huduma ya fedha asilimia fulani kwa kila mwaka pamoja na vifaa ili vituo hivyo viweze kupanuliwa na viweze kupata huduma iliyo bora kama watoto wengine wenye wazazi huko majumbani? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kweli wimbi la watoto kukimbilia mjini liko kubwa na Serikali imekuwa ikijitahidi kufanya utafiti mara kwa mara kujua idadi, maeneo wanakotoka kwa wingi na sababu. Tumefanya hivyo mwaka 1989 na kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, tulifanya hivyo mwaka 1997 kushirikiana na *Serve Children* ya Uingereza na kwa hali ilivyo sasa Mkoa wa Dar es Salaam ndiyo unaongoza kwa kuwa na idadi ya watoto wengi wanaofikia 2,443. Tunavyo vituo 45 kwa Dar es Salaam tu vinavyohudumia hawa watoto. Kwa kweli siyo tunasaidia tu kwa maana ya pesa, lakini tunasaidia vile vile kwa maana ya kutoa ushauri kama nilivyozungumza katika jibu la swali la msingi.

Lakini kuhusu hatua inayochukuliwa kwa wazazi wanaotelekeza watoto hawa, sehemu kubwa kwa kweli ni kuwatafuta wazazi hawa na ndiyo maana tunapokuja kuwagundua tunawarejesha wale watoto kwa wazazi wao. Lakini ni vyema sisi kama viongozi, sote tujitahidi kwenda kwenye chanzo cha watoto wa kuzagaa mitaa, wazazi tuwaelimishe kujua kuzaa na kutunza watoto, siyo wanafyatua tu na kuacha mitaani wanazunguka. Ni jambo linaloumiza sana lakini lazima tuliseme, siyo wakati wa kuficha tena sasa kama tunataka kuwapunguza watoto hao kuzagaa mitaani. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, suala la kutunza familia, mimi nafikiri wakati tunaendelea kuongeza ukubwa wetu wa bajeti la msingi hapa ni kurudi kule kule, tuwaambie wazazi wetu wapunguze migogoro ndani ya familia waweze kubeba majukumu yao, kutunza watoto ambao wanawazaa na vile vile tusichoke tuendelee kusema tu, mwisho watasikia tu. *(Makofi)*

Na. 58

**Kituo cha Walemavu - Ngehe**

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA** aliuliza:-

Kwa kuwa Kituo cha Walemavu cha Ngehe kina walemavu na watumishi na kwa kuwa kwa muda mrefu Serikali haijatoa huduma inayotakiwa itolewe kwa walengwa kama ilivyokuwa huko nyuma:-

(a) Je, kwa nini Serikali haikihudumii kituo hicho ipasavyo?

(b) Je, kwa Serikali kuacha kuhudumia kituo hicho, haioni kwamba inasababisha usumbufu mkubwa kwa walengwa?

(c) Je, Serikali ina msimamo gani kwa baadaye juu ya kituo hicho cha walemavu?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali na Mheshimiwa Dr. Thadeus M. Luoga, Mbunge wa Mbinga Magharibi, lenye sehemu (a), (b), (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, makazi ya Ngehe ni miongoni mwa makazi 17 yanayoendeshwa na Serikali kwa ajili ya kutoa matunzo kwa watu wenye ulemavu na wasiojiweza. Makazi haya yalijengwa kabla ya uhuru kwa ajili ya kuwatunza watu walioathirika na ukoma. Makazi karibu yote yanaathiriwa na uchakavu wa majengo, vitanda na magodoro. Jitihada za Wizara za kukarabati majengo na vifaa na kutoa huduma timilifu zinakwama kutokana na ufinyu wa Bajeti ya Serikali.

Wizara yangu inafanya kila jitihada kuhakikisha kwamba, wakazi wa Ngehe, wanapatiwa huduma za msingi kama chakula na malazi, kwa kuzingatia Bajeti ya kila mwaka kama inavyoidhinishwa na Bunge lako.

Mheshimiwa Spika, ninazo taarifa juu ya hali isiyoridhisha ya huduma katika makazi ya Ngehe, ikiwa ni pamoja na kubomoka kwa majengo na ukosefu wa vifaa, nyenzo na mahitaji ya wahudumiwa. Kutokana na hali hiyo, Wizara imemwagiza Kamishna wa Ustawi wa Jamii kwenda Ngehe kufanya tathmini na pia kufanya majadiliano na Mkurugenzi wa Halmashauri husika ili kuona namna gani tutashirikiana kuhudumia wananchi hawa.

Mheshimiwa Spika, ni imani yangu kwamba, Mheshimiwa Mbunge, atashirikiana na Wizara yangu hasa katika kuishauri Halmashauri iweze kutoa mchango wake wa huduma kwa wananchi walio ndani ya mipaka yake.

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali moja kama ifuatavyo: Baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningeomba kufahamu kuwa kamishna amepewa muda gani kwenda kutathimini hali ya kituo hiki cha Ngehe na baada ya tathmini Serikali Kuu ama Wizara itasaidiana na Halmashauri yetu ya Mbinga kusaidia hiki kituo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, tumemwagiza Kamishna aende Mbinga kwenye Kituo cha Ngeye mara baada ya Bajeti yetu kusomwa na akishamaliza kukagua pale atashauriana na Mkurugenzi kama nilivyoeleza katika jibu la swali la msingi ili tuone hatua za haraka za kuweza kusaidia hali ya Kituo kile kabla ya hatua za kawaida kuendelea.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha, tunaendelea na matangazo. Kuna vikao viwili vimepangwa kwa siku ya leo vya Kamati. Moja ni Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Eliachim Simpasa, anaomba Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane saa tano asubuhi hii Chumba Na. 133 ghorofa ya kwanza. Kamati ya pili, ni Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Athumani Janguo, anawaomba Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane Ukumbi Na. 227 ghorofa ya pili mara baada ya kipindi cha Maswali.

Mwisho wa matangazo ya vikao. Lakini mjadala wa Bajeti na Hali ya Uchumi unaendelea. Wasemaji wa leo wameshawekwa kwenye ubao wa matangazo. Wa nne wa kwanza watakuwa Mheshimiwa Dr. William Shija, Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo, Mheshimiwa Aggrey Mwanri na Mheshimiwa Philip Magani. Tunaendelea na *Order Paper,* Katibu.

## HOJA ZA SERIKALI

### Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2003, Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2004/2005 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2004/2005

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Namwita Mheshimiwa Dr. William Shija afungue dimba.

**MHE. DR. WILLIAM F. SHIJA:** Mheshimiwa Spika, napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi asubuhi hii ili niweze kutoa mchango wangu kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Sengerema na kwa niaba yangu mimi mwenyewe kwenye hoja ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji na hoja ya Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda niungane na wenzangu kumpa pole Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na dada yake Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kumpoteza baba yao mpenzi. Tunawaombea huruma ya Mwenyezi Mungu na marehemu ampumzishe mahali pema Peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, napenda vile vile niwape pole sana wenzetu waliopatwa na matatizo mbalimbali hapa katikati, ya ajali, kushambuliwa na majambazi kama Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Ndugu yetu Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere na vile vile ajali aliyopata ndugu yetu Mheshimiwa Estherina Kilasi, ambaye tunashukuru kwamba ameungana nasi.

Mheshimiwa Spika, napenda vilevile niseme mapema kwamba, moja ya kazi kubwa ya Mheshimiwa Mbunge ni kufikiria na kupitisha Bajeti ya Serikali na kazi hii ndiyo tunaifanya wiki hii na kwa maana hiyo napenda niseme mapema kwamba, ninaunga mkono hoja zote mbili. Kwa sababu Serikali lazima tuiwezeshe kufanya kazi zake ambapo ndiyo inawajibika Kikatiba kwa wananchi na sisi sote.

Mheshimiwa Spika, pili, napenda niulize maswali kwanza kabla sijaingia kwenye maeneo ya maoni ninayofikiri mimi. Nayo ni kwamba, kwa nini wastaafu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki bado wanalalamika? Narudia kwa nini wastaafu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki bado wanalalamika kiasi kwamba wanaliaibisha Taifa letu na Serikali yetu kwamba sisi tulifanya vitu tofauti na wenzetu wa Uganda na Kenya, kwa nini malalamiko bado yapo na sasa hivi ni malalamiko makali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda niulize kwa nini waliostaafishwa wa *Tanzania Elimu Supplies* bado wanalalamika kiasi hicho? Kwa nini kama wenzetu walitufanyia kazi *Tanzania Elimu Supplies* tumewatelekeza na wamefikia kulalamika kiasi hicho? Kuna nini ambacho hatuwezi kufanya kama Serikali, kama Tanzania, kama Taifa, ili wenzetu wa *Tanzania Elimu Supplies* tuwapatie haki yao ili waweze kukaa na familia zao, waweze kuelimisha watoto wao, kuna nini ambacho hatujafanya?

Mheshimiwa Spika, napenda niulize kuna nini Shirika la Reli Tanzania? Kuna kitu lazima Shirika la Reli Tanzania kinapangwa vibaya au kinatekelezwa vibaya, ambacho hatukifahamu hapa Bungeni? Ningependa niseme kwamba, Shirika la Reli linatuogopesha, baada ya ajali mbaya kutokea hapa Dodoma na baada ya kuanza kutokea migomo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, migomo hii inatutisha kwa sababu si kwamba inaathiri maisha ya watu ya kila siku tu katika usafiri wao, lakini vile vile yanaathiri uchumi. Reli yetu ya Kati kwa mfano, tokea Dar es Salaam, Tabora mpaka Mwanza na Kigoma ni reli ambayo ni muhimu na lazima tuhakikishe kwamba, hakuna dosari ambazo zinaendelea kutokea kwa sababu athari zake kiuchumi na kijamii ni kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, hayo yalikuwa maswali sasa napenda niingie sehemu ya tatu ya mchango wangu. Nayo ni kwamba, tumeulizwa hapa na Mheshimiwa Waziri kwamba, je, mngetusaidiaje katika kutazama namna ya kupanga katika Taifa letu? Sasa ni kweli Tanzania kama nchi zingine za Afrika na dunia inayoendelea, zina matatizo sana ya namna ya kupanga mipango yake. Matatizo yanatokea kwa sababu tunapanga mipango lakini vile vile tunategemea sana kusaidiwa na watu wa nje katika kutekeleza mipango yetu. Kwa hiyo, inafikia mahali lazima tupewe masharti.

Mheshimiwa Spika, ningefurahi kama Serikali ingekuwa inasema wazi wazi kwamba, katika kitu fulani tumepewa masharti na *IMF* na *World Bank,* lazima tutekeleze. Hapa ndiyo mahali pa kusemea ili nchi ikipata nafasi ya kufahamu mahali gani kweli lazima tumefungwa na lazima tufuate jambo fulani. Kuficha hakutusaidii kwa sababu tunajua tunatumia asilimia arobaini ya fedha za wenzetu na lazima kuna masharti mahali, kama ambavyo tuliwahi kupewa masharti ya kuhakikisha kwamba, *TIPPER* inasimama, lakini leo kwa matatizo ya mafuta tunaona sasa umuhimu wa kuwepo *TIPPER.*

Mheshimiwa Spika, ili tuweze kusaidiana katika mipango yetu daima lazima tukumbuke kwamba mahitaji ya binadamu yanafahamika vizuri na tukiyatumia mahitaji hayo ya msingi yatatusaidia sana katika kupanga mipango yetu na hatimaye kuwashawishi wale ambao tunasaidiana nao katika kukubaliana na mipango hiyo. Mahitaji haya ni chakula na maji. Binadamu yeyote yule, awe amesoma, hakusoma, mzima wa viungo na mlemavu, lazima anahitaji chakula na maji, mavazi, malazi na makazi, elimu, haki ya raia. Hayo ndiyo maeneo matano ambayo mimi nimeyabaini na kila tunapopanga kwa mwaka ni vyema tukazingatia ni namna gani tunakidhi maeneo haya.

Unapozungumzia kilimo, unazungumzia chakula na maji. Lazima binadamu ayapate. Sasa tumeandika Dira ya Taifa. Tumeandika Ilani ya Uchaguzi kwenye Chama chetu cha Mapinduzi, tunaifahamu. Tumeandika programu ya kupunguza umaskini na tunasaidiwa na wafadhili mbalimbali katika kutekeleza maeneo hayo. Suala ambalo mimi nauliza ni kwamba, je, dira hii sasa Watanzania tunaifahamu vizuri kwa pamoja?

Mheshimiwa Spika, dira hii ya maendeleo ya mwaka 2025 tuko pamoja katika kuifuatilia? Kwa sababu huko nyuma Watanzania tulipata fursa ya kuambiwa mipango ya Azimio la Arusha na tukaelezana wote karibu tukafahamu na kila mmoja wetu alikuwa anajitahidi kufuata ni nini kinazungumzwa kwenye Azimio la Arusha. Sasa leo tuna dira na katika dira hii kuna mambo mengi, unaweza kuwa unachagua mwaka hadi mwaka ni nini utekeleze kutokana na dira. Lakini tumefanya njia gani za mawasiliano ili Watanzania walio vijijini, walio mijini na sisi ambao tunawawakilisha, tunakuwa pamoja katika kuielewa dira hii.

Mheshimiwa Spika, mimi nina mashaka. Kwa sababu dira hii hata hapa Bungeni tulifanya Semina ya siku mbili, tatu, nne na kuendelea. Bahati nzuri tunajua kusoma na kufuatilia maandishi vizuri. Lakini bado hatujashonana vizuri Watanzania katika kutengeneza dira yetu mpya ifanye kazi. Hilo mimi natoa changamoto na changamoto hii inahitaji mawasiliano ya kina, ya Kitaifa ili tuweze kutekeleza masuala mbalimbali kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, vilevile nasema katika suala la kupunguza umaskini bado tuna changamoto ya kuelewana kwamba hasa unatakiwa ushambulie maeneo gani. Mara nyingi kunakuja na maandishi. Juzi hapa Waheshimiwa Wabunge, tulipata nafasi ya kuhudhuria semina ya namna ya kupunguza umaskini na umaskini unaonekana kweli kweli vijijini na mijini. Leo hii kuna malalamiko ya wazi wazi kwamba, pamoja na

kusemwa kwamba uchumi unaimarika lakini hali ya vijijini ni mbaya kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tutajivuniaje hali hii kama hali inakuwa duni kama ambavyo inaonekana vijijini? Mimi nasema kwamba katika maeneo haya lazima tuelewane na unakuta tunaandika maandishi kwa Kiingereza, ma-*book* makubwa makubwa ambayo huwezi ukayatumia katika kuwasiliana na ndugu zako wengine vijijini mkaelewana mnazungumza nini juu ya umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lazima maeneo haya tuendelee kuyaangalia upya, tushauriane vizuri, twende pamoja. Sasa katika eneo la kipaumbele mimi nasema kitu cha kwanza ambacho ningesema ni maji. Kama tungekubaliana kushambulia eneo la maji, maji yataleta chakula, maji yataleta afya bora, maji yataleta karibu kila kitu. Ni uhai huo huo wa maji kwa binadamu, pamoja na maji tunajua elimu yetu lazima tuendelee nayo. Mtu anayepata maji na elimu utakuta maeneo mengine haya ya afya na kilimo yanaingia vizuri kwa sababu mtu anakuwa na uwezo wa kujikomboa kwa sababu anapata maji kwa ajili ya mifugo yake, anapata maji kwa ajili ya yeye mwenyewe, anapata maji kwa ajili ya mimea. Tukubaliane Watanzania tufungue njia ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa elimu najua tunakubaliana, lakini katika elimu mimi napenda niseme kwamba, hebu tuchambue upya hali ya elimu yetu. Katika hali ya utandawazi hatuwezi kuendelea kubishana kwamba, je, kitumike Kiingereza au kitumike Kiswahili na tunaendelea mwaka hadi mwaka. Sasa kama ni Kiingereza kinatumika mpaka kwenye kompyuta tukifundishe vizuri kwa programu maalum, kwa *reform* nzima ya elimu na tuulizane Kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja yangu ni kwamba, tuulizane Kitaifa ni namna gani elimu yetu sasa tuipange upya, kuliko kusema kwamba, tunajenga madarasa na sasa tunaendelea na tunasaidiwa na hela za *HIPC* na kadhalika. Haitoshi katika eneo la elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi inatakiwa tutazame ni namna gani utaimarisha ufundi ili unapotengeneza mfumo wa maji, unapotengeneza mifumo ya mawasiliano unakuwa unaweza kuitengeneza au kuikarabati. Maana udhaifu wetu mkubwa upo katika eneo hilo. Hali kadhalika sasa utakuja katika eneo la tatu mawasiliano, barabara na vyombo vyake.

Nilipopendekeza mwaka 1989 kwamba, tuwe na simu za mkononi, kuna watu Watanzania fulani walinibishia, mwezi Februari kuna *article* ilitoka kwenye *Sunday News*. Nikapendekeza Tanzania ianze kutumia simu za mkononi, baadhi ya Watanzania wakanibishia. Lakini leo nafarijika kuona kwamba, simu za mkononi zimeenea mpaka vijijini Sengerema huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa mawasiliano hayo yanatusaidia kupunguza safari zisizo za lazima, kuwa na uhakika wa mawasiliano na vile vile katika kuzalisha vitu mbalimbali. Sasa barabara zetu zinakwenda vizuri. Lakini tungetazama maeneo haya na

mawasiliano ya kawaida, kwa Kiingereza wanaita *soft communications,* tukaziimarisha hizi zikaweza kupunguza matumizi katika maeneo kadhaa.

Mheshimiwa Spika, la nne ni nishati, kwa sababu muda ulioupanga na tukakubaliana ni mdogo. Hebu nielekee kumalizia mchango wangu katika eneo la fedha na uzalishaji. Mimi naomba tukubaliane kwamba, wawekezaji wa uhakika wako hapa hapa Tanzania, wapo hapa hapa Bungeni. Tuelezane ukweli tu, kama alivyojibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara sasa hivi amejibu vizuri sana, kwanza kama kuna taarifa kwamba kuna fedha ambazo Wabunge na Wataalam mbalimbali kwa taaluma zao wanafahamu, wanaweza kuzitumia ili kuzidisha uzalishaji wa nchi, basi tuambizane tuzitumie. Lengo letu ni kujikomboa hapa.

Lakini kwa sababu tunasita katika kupeana taarifa hizi, nimalizie kwa kusema kwamba, Viongozi wa Afrika hatuwatendei haki waliotuamini. Tukubaliane kabisa kwamba, tunahitaji kubadilika ili tusiwapuuze wanaotuamini. Bunge lako Tukufu lianze sasa kupokea taarifa za utekelezaji wa Serikali katika kila Mkutano wa Bunge ili tuambizane kwa uwazi na ukweli. *(Makofi)*

Tujue fedha zimetumiwa namna gani kila robo ya mwaka au tunapokutana ili tuweze kushauri na kusahihisha ipasavyo. Nasema hivyo kwa sababu kuna mashinikizo ya ukoloni mamboleo yanakuja Tanzania, *conditionalities,* masharti fanyeni hivi, fungeni hili, mfungue lile kabla hata hatujaelewana vitu unakuta tumebadilisha na hatimaye unakuta hatuna mpango wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, viongozi wa Afrika tunaisaliti Afrika sisi wenyewe na tunawasaliti wananchi wanaotuamini, tunaharibu mali, tunajipendelea, tunakuwa wanafiki, tunajenga majumba na kununua magari ya anasa bila utaratibu wa kujua kwamba kwa nini tutumie fedha namna hiyo, wakati wananchi hawana maji vijijini. Zitazamwe takwimu za Afrika utaona viongozi tumefuja mali na tumewasaliti wananchi wanaotuchagua. Tazama Afrika yote hii, mimi nisingependa Tanzania tuwe mmoja wa nchi za Kiafrika ambazo zinasaliti wananchi wake na kuwaacha hoi miaka hadi miaka. Tutazame upya mipango yetu na namna tunavyoitekeleza ili wananchi wetu wawe na matumaini ya kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga hoja mkono. *(Makofi)*

**MHE. DR. AARON D. CHIDUO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie katika kujadili hoja za Mawaziri wawili, Waziri wa Fedha na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsihaji. Kwanza kabisa, naunga mkono hoja zote mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza kwa hotuba zao ambazo zinaleta matumaini. Jumamosi na Jumapili iliyopita baada ya hotuba nilikwenda Jimboni kwangu, kupata mawazo ya wananchi wanazionaje hotuba hizi na hasa wanaionaje Bajeti ya mwaka huu. Wananchi wametoa pongezi na wamefurahia bajeti hii na wastaafu waliokuwa wakinikera, wale ambao walipewa pensheni za mkupuo, wameishiwa, hali zao ziko hoi,

wamefurahia sana kuona kwamba, neema inakuja na wangependa sana ama utaratibu huo ungeanza Julai, mwanzoni mwa mwaka wa fedha lakini kungoja mpaka Januari, kama ikiwezekana basi angalau hata miezi ipunguzwe ya kuanza kutoa neema hiyo.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea mbele, naomba niungane na wenzangu kuwapa pole Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kifo cha baba yao mpendwa. Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amin.*

MheshimiwaSpika, nichukue nafasi hii vilevile kumpongeza Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kukinyakua tena kiti chake cha Bariadi Mashariki na kukiangusha Kigogo cha *UDP*. Tunamkaribisha sana na ameona aje huku kwa *back-banchers* kwa hiyo tunamkaribisha. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kufurahia uzuri wa bajeti na mipango pake yake haitoshi, ni muhimu zaidi kuwepo na utekelezaji makini na usimamizi imara na ufuatiliaji wa utekelezaji wakati wote ili tuweze kupata mafanikio. Bahati mbaya katika nchi yetu maneno yetu hayalingani na vitendo vyetu. Tumefanya kauli za kubabaisha kuwa utamaduni wetu. *(Makofi)*

Tumeelezwa katika bajeti kwamba imeandaliwa kwa msingi wa utelelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2000, Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2005 na mkakati wa kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, ukweli wa mambo ni kwamba, huko Vijijini kwenye Vijiji, kwenye Kata na hata Wilaya na Mijini, wananchi wa kawaida hawana uelewa wowote juu ya Dira ya Maendeleo na Mkakati wa Kupunguza Umaskini. Kwa hiyo, kuna haja ya kufanya juhudi za ziada kuhamasisha wananchi wakati wote waelewe vizuri zaidi Sera na mikakati ya kuondoa umaskini na Dira ya maendeleo ya Taifa ili washiriki kwa ukamilifu katika programu mbalimbali za kupambana na umaskini. Katika hili, Waheshimiwa Wabunge tuna jukumu maalum la kushirikiana na watumishi wa Serikali kwenye maeneo yetu. Tushirikiane, tusaidiane, tuwashirikishe wananchi kwa ukamilifu, kwa kufanya hivyo tunaweza kusukuma maendeleo kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya kupewa kipaumbele yameainishwa vizuri katika Mkakati wa Kupunguza Umaskini, kama kuna marekebisho yoyote juhudi zielekezwe zaidi kwenye yale maeneo ya uzalishaji mali, kilimo, mifugo, uvuvi, viwanda, utalii na vile vile yale maeneo yenye kuwawezesha wananchi waweze kuwa wazalishaji wazuri. Wananchi wengi vijijini wanashughulika na kilimo. Lakini wananchi hawa wanahitaji kuelimishwa waelewe juu ya kilimo cha kisasa, kilimo bora, wapate ujuzi, wapate zana na wapate pembejeo kwa wakati wake ili wabadilishe kilimo chao na la msingi kabisa lazima hatua za makusudi zichukuliwe tuondokane na jembe la mkono.

Mheshimiwa Spika, haya yamekuwa yakisemwa miaka nenda, miaka rudi, lakini bado tupo pale pale. Kwa hiyo, juhudi za makusudi zielekezwe katika kuwabadili wakulima hawa na njia mojawapo ya kuwabadili wakulima hawa vile vile ni kuweka uzito mkubwa kwenye elimu kwa ngazi zote. Lazima tuwe na Taifa lililoelimika na watu

wanaotaka kujiendeleza kwa elimu wakati wote, bila ya kufanya hivyo hatuwezi kujitoa katika dimbwi la umaskini.

Mheshimiwa Spika, tuige mifano ya wale walioweza kujikomboa katika kilimo duni kwa mfano India kwa njia ya *The Green Revolution.* India pamoja na idadi kubwa ya wananchi, zaidi ya watu bilioni wameweza kujitosheleza kwa chakula cha nafaka. Sisi kila baada ya miaka michache ni njaa. Kuomba chakula ni aibu. Kama ninavyosema, yanayotakiwa kuyafanya tunayajua, hatuyafanyi. Kilimo cha umwagiliaji maji mashamba ndicho kitakachotutoa katika aibu hii ya kuomba omba chakula. Lakini hebu tutazame hali ilivyo, kilimo cha umwagiliaji mashamba kinatekelezwa kwa asilimia 0.68 tu ya hekta ambazo zinafaa kwa kilimo cha umwagiliaji hapa nchini. Hivi sasa kilimo cha umwagiliaji kinaendelezwa katika hekta laki mbili na laki nane tisini na tano tu kati ya hekta milioni ishirini na tisa ambazo zinafaa kwa kilimo cha umwagiliaji maji. Ni aibu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, lazima fedha zitengwe zaidi kwenye kilimo cha umwagiliaji maji mashamba. Kwa mfano, hela zilizotengwa mwaka huu ni shilingi bilioni 4 lakini hapo hapo utaona kwamba, kuna shilingi bilioni 11 zilizotengwa kwa maendeleo ya mazao. Hizi naziuliza ni kwa kazi gani ikiwa kazi ya kuendeleza mazao inafanywa na wakulima wenyewe?

Haiwezekani sehemu ya kiasi hicho cha shilingi bilioni 11 ikachukuliwa ikapelekwa kwenye kilimo cha umwagiliaji maji mashambani? Hayo ni mawazo yangu na pendekezo.

Mheshimiwa Spika, viwanda vya kusindika mazao, ukitazama fedha inayotengwa kwa ajili ya viwanda ni ndogo. Tunasema viwanda ni sekta kiongozi lakini kiasi cha fedha kinachotengwa kwenye viwanda hakilingani na fedha zinazostali kwenda kwenye sekta kiongozi.

Mheshimiwa Spika, biashara ya nje, bado tunahangaika, tunatafuta fedha za kigeni, lakini njia mojawapo ni kuongeza uzalishaji vile vile kusukuma upelekaji bidhaa zetu nje ya nchi. Hapa tumeambiwa hatujatumia kwa ukamilifu fursa za *AGOA, EBA.* Hatujajiingiza vya kutosha katika kupeleka bidhaa zetu kwenye nchi za *SADC* na tusipoangalia katika Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki tutaachwa nyuma katika kufuatilia masoko yaliyoko Afrika Mashariki.

Kwa hiyo, chombo cha kusimamia na kusukuma upelekeaji bidhaa nje ya nchi, yaani Halmashauri ya Biashara ya Nje, kinastahili kuwezeshwa kifedha ili kiweze kufanya kazi yake kwa ukamilifu. Ukiona fedha zinazotengwa kwenye bajeti kwa ajili ya kusaidia vyombo kama hivi utashangaa kusema kweli mwaka huu Halmashauri hiyo haikupewa fedha zozote imepewa *zero.* Sasa tutasukuma vipi mauzo nje ya nchi na kupata fedha za kigeni?

Mheshimiwa Spika, hayo niliyoyataja ni maeneo ambayo yanastahili kupewa kipaumbele. Twende kwenye maeneo ya kutuongezea uzalishaji na hasa tuelekeze nguvu

zetu vijijini. Hali ya maisha vijijini, hali ya uchumi vijijini ni tofauti kabisa ukilinganisha na hali tuliyonayo mijini na ndio sababu vijana wetu wengi wanakimbilia mijini wakidhani huko hali ni afadhali lakini ukweli wenyewe wanapata tabu wanapokuwa mijini. Wakati mwingine hata msamaha huu wa ada za leseni waliopewa hawa *Marching Guys* yaani Machinga isije ikawa ni kivutio cha vijana wetu wengi kutoka vijijini kwenda mjini. Kwa hiyo, tubadili hali ya maendeleo vijijini. Mkakati wa maendeleo vijijini ndio unastahili kuwekewa uzito unaostahili, tubadili hali yetu vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, namwomba Mwenyezi Mungu, amsaidie Rais wetu Benjamin William Mkapa, aendelee kupata nafuu, apone na arudi kuliendeleza Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, kwa kuwa mengi yameshasemwa na wenzangu, naunga mkono hoja zote mbili. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kutoa mchango wa wananchi wa Jimbo langu la Siha katika Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu, naomba nichukue nafasi hii kwanza, kutoa pole sana kwa rafiki yangu, kila wakati nam-*refer* kama rafiki yangu, sitanii, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, nampa pole sana. Nilijua kwamba amefiwa na baba yake mzazi hapa hapa Bungeni, sikufahamu kabla walau ningempelekea kadi. Kwa niaba ya wananchi wote, napenda kuchukua nafasi hii kuwapa pole sana yeye na dada yake kwa kuondokewa na baba yao mpenzi.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Siha, pia napenda nichukue nafasi hii, kumpongeza sana ndugu yangu, Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kazi nzuri. Kila siku nilikuwa namwambia kwamba, Chama hiki ni Chama cha Wakulima na Wafanyakazi na kazi yake ni kutetea wakulima na wafanyakazi, njoo huku kama ni purukushani tufanye humu humu ndani ya CCM. Sasa naona amezingatia mawaidha yangu, amekuja, tuendelee kufanya kazi ya kuwapigania wananchi wetu wote. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninatambua kwamba, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, yuko nje na anaendelea kutibiwa. Wananchi wa Jimbo la Siha, wanapenda kuchukua nafasi hii kumtakia kila la kheri na fanaka, apone mapema ili aweze kurudi nchini tuendelee na shughuli zetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa ninaomba nijielekeze katika bajeti na kwa vile ninatambua kwamba baadaye nitakwenda *speed* kidogo, nianze kabisa kuomba msamaha, sauti ikiwa kubwa ujue tu kwamba ni msisitizo, mkiona maneno yamekuwa mengi sana, makali sana, mniwie radhi, nia na shabaha ni kuijenga nchi yetu. Yale ambayo nafikiri yamenifurahisha na yamewafurahisha wananchi wa Jimbo langu la Siha nianze kuyasema mapema. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mimi kwangu nasema, *it is my judgment* kama Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Siha kwamba, bajeti hii ni nzuri kwa sababu inawaangalia wakulima na wafanyakazi wa nchi hii, mapungufu yake nitaeleza mbele ya safari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, iko *notion* kwamba, unajua bajeti hii imetengenezwa kwa sababu mwaka 2005 unakuja, dunia nzima ndivyo wanavyofanya na si kweli kwamba imefanyika hivyo kwa sababu hiyo. Mimi toka nimeingia Bungeni mwaka 2000, sikumbuki bajeti ambayo ililetwa hapa ambayo ilikuwa si nzuri, bajeti zote zilikuwa ni nzuri, sikumbuki bajeti hata moja ambayo ilikuwa mbaya. Inaweza kuwa na matatizo katika *implementation* lakini toka Mheshimiwa Basil Mramba amekuwa Waziri wa Fedha, bajeti zote zilizopita hapa tuliziunga mkono tulisema ni nzuri na zimekwenda vizuri. Kusema kwamba, bajeti ya mwaka huu inaonekana nzuri kwa sababu tunasogea kule mbele, sio kweli ni kwamba, Chama cha Mapinduzi kupitia Serikali yake, kinafanya kazi ya kuwafanya wananchi wafurahi. Kazi ya Serikali yoyote inayoongozwa na matakwa ya wananchi ni ku-*impress,* unafanya vitu vinaudhi wananchi inakuwaje sasa? Hilo, moja nilitaka niliweke vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kule kwangu unasema kuanzia sasa wafanyabiashara hawatahitaji kuwa na leseni labda awe anapata mapato ya shilingi milioni 40. Haraka haraka niseme kwamba, hakuna kitu hapo wakati najua pale kwenye Mji wa Sanya Juu tatizo lililokuwepo pale la vijana wangu kushindwa kuanzisha biashara limekwisha, Ngarenairobi hawana matatizo, Lawate hawana matatizo, Madukani hawana matatizo, Karansi hawana matatizo wanaanzisha biashara, haiwezekani. Hili mimi sihitaji kwenda Chuo Kikuu kujua ni akili ya kawaida tu kwa sababu zamani ilivyokuwa na *mark* nilikuwa Mkuu wa Wilaya, ilikuwa kupata leseni kwanza upate *Clearance* ya *Income Tax Department* waseme huyu jamaa hana chochote anachodaiwa kwa hiyo mpe leseni, ilikuwa ni *contradiction.* Mtu alikuwa hajafanya biashara yoyote, hajafanya kitu chochote, unamtaka aonyeshe mapato, sasa tumefika mahali tukasema kuanzia sasa hata hao wa shilingi milioni 40 akishalipa mara moja tu basi, halipi tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nasimama vipi hapa niseme hakuna kitu wakati nina jeshi nyuma yangu kutoka Siha linasema wewe ndio utakayesema kwa niaba yetu wote halafu *records* ziseme hakuna kitu hapa, hapana iko kitu, mimi ninakiona. Kazi yangu ni kwenda kukaa na wananchi wangu wa Jimbo la Siha na kuwaonyesha, hiyo moja. Najua hatua ya pili inayofuata ni kuwa-*empower* wananchi wetu kwa kuwasaidia wapate mikopo nafuu waweze kuendesha biashara, waweze na wao kuingia katika hali hii ya ushindani na kuweza kuendesha biashara, nilitaka niliseme hilo. Ninayo mengine mengi lakini hayo machache ni sehemu ya mambo ambayo yamenifurahisha.

Mheshimiwa Spika, twende mbele, tunazungumza habari ya mpango, mpango ni *component* ya kijamaa sio ya kibepari, ushirika ni ya kibepari na kijamaa, ushirika uko kote kuwili. Katika uchumi wa kibepari hakuna mipango, unaendeshwa na sheria ya utashi na urari, sheria ya mashindano na sheria ya thamani *(The Law of Value, the Law of Competition and the Law of Demand and Supply),* ndizo zinafanya kazi. Huendi tu hivi ukapanga, kupanga katika mazingira ya kibepari wanapanga katika *level* ya *enterprise,*

kiwanda kimoja kimoja, Jimbo moja moja na ndio maana wanapata mgogoro wakati mwingine wanafika mahali unawaona wanazalisha kuliko walivyotegemea, inawaletea matatizo kwenye sheria hiyo hiyo ya utashi na urari *(The Law of Demand and Supply)* ni kwa sababu California huku wamezalisha, Manitoba wamezalisha, sasa hawana kitu kinachowaunganisha matokeo yake inabidi vingine umwage Baharini ili ku-*stabilize economy* ili mambo yaende vizuri. Huku kwetu tunayosema nchi ya kijamaa tunasimamia, tunahakikisha kwamba shughuli zote zinaendeshwa kwa kutumia chombo ambacho kinatuongoza. Hutegemei kwamba utaambiwa hivi unajua bwana kuna na *market failure* na vitu vingine.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, ametuambia uchumi ume-*drop* kidogo na tumemwuliza kwa nini ume-*drop*? Anasema kilimo chetu kimepata matatizo kidogo lakini *overall* anasema kwamba uchumi umepanda. Mimi nimezungumza habari hii, nikienda katika Jimbo langu la Siha, nilishasema na narudia tena, nikisema uchumi umekua, uko juu kwa hiyo tumefanya vizuri. Wataniambia hivi, wewe huu ndio mwisho wako wa kuwa Mbunge, wewe unatuambia nini? Sisi hali yetu hapa ni ngumu, wale Wachaga, Mheshimiwa Mramba anawafahamu, kama hawana hela mfukoni ukiwaambia kitu, hawaelewi. Wanakuambia unazungumza maneno gani hapa, unatuambia uchumi umekua hapa, uchumi umekua halafu sisi hatuna kitu mfukoni, maneno gani unatuambia?

Sasa hivi sio Wachaga tu na Wapare wale watani zetu nao wamekuwa hivyo hivyo akina Mheshimiwa Jumanne Maghembe, wote wale wamefika mahali ukiwaambia uchumi umekua anataka kuona kitu kinachoitwa *a one to one function* kati ya kukua kwa uchumi na maisha yake ya kila siku. Kuna kitu kinachoitwa *economic growth* na *economic development,* hivi vitu viwili ni tofauti. Uking'ang'ania kwamba uchumi umekua *and therefore automatically* una-*assume* kwamba, maendeleo yanakuja, *it is wrong.* Ni lazima kuwepo na kitu kinachoitwa *trickling down policies* zinazoagiza kutoka kwenye uchumi mpana unashuka nao kuja nao hapa chini, nikisema hivyo sina maana kwamba haijafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo la elimu, ndio kazi nzuri imefanyika. Ukimwambia mtu uchumi umekua na kuna maendeleo ya kiuchumi ni kweli utaona watoto walikuwa wanakwenda 200 sasa 500. Kwa hiyo, hapa naona *economic development,* naona uchumi umekua katika maana kwamba watoto wanakwenda darasani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo tumefanya vizuri ni barabara. Juzi tumekwenda kutembelea Daraja la Mkapa limefunguliwa. Hivi tunavyozungumza, Wasukuma wanajua kabisa barabara zinakwenda kwao. Mimi kule kwangu katika Jimbo la Siha nimepiga kelele nitakuja kueleza hapa nimeziona barabara zinatengenezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumefanya vizuri kwenye eneo la maji la Mheshimiwa Edward Lowassa, unaona kabisa watu wanashughulika. Katika nchi hizi za kibepari walifanya nini? Ni kweli kabisa huwezi kuchukua hela mkononi unawaambia haya

Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Spika, chukua hizi weka mfukoni wana-*create* kitu kinachoitwa *welfare states* kwa maana kwamba, hakikisha kwamba, unaimarisha huduma zetu, hakikisha kwamba watu wanapata maji safi na salama, hakikisha kwamba watu wetu wanapata umeme, hakikisha kwamba watoto wanakwenda shule, ukishafanya hivyo ndio unaondokana na umaskini, ndio uchumi unaonekana unakua na unaonekana una maana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine na hapa *I want to be critical*, ni eneo la kilimo. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Siha nataka niseme hili bado lina matatizo. Mimi nilisimama hapa mkasema mnachukua Mikoa minne mtawapelekea *subsidy*. Nimeuliza swali hapa na nangoja majibu yake je, ni kwa kiasi gani mpango huo umemsaidia mkulima? Mbolea ilipotoka pale bandarini ilipokwenda Mbozi, Rukwa, ilipofika kule bei yake ilikuwa shilingi ngapi? Je, mwananchi wa kawaida ameweza kumudu hizo bei?

Mheshimiwa Waziri wa Fedha, tulisema hapa hii habari ya kuanza kwanza na Mikoa minne, mitano, anza na Mikoa yote ya Tanzania kwa sababu nchi hii ni nchi ya kilimo. *Development* ninayoiona humu wanasema tutaangalia ile Mikoa ambayo ina mvua nyingi tutawasaidia kidogo na nini. Hivi ni Mkoa upi na Wilaya ipi na Kata ipi katika nchi hii ambayo haitegemei kilimo? *(Makofi)*

*It is my judgment and my sincere opinion Mr. Speaker Sir* kwamba, ni lazima Serikali ifike mahali wala isipate kigugumizi, suala la kutoa *subsidy* kwa ajili ya mbolea, *whether you like it or not,* kuleta *revolution* ya kilimo ni lazima utoe *subsidy*. Sasa hili Serikali inajua *position* yake, nchi kubwa kama vile Marekani, Norway, Sweden, *South Africa,* wanatoa *subsidy* kwa ajili ya wakulima wao, sisi tunasema tuwaambie wasitoe *subsidy* ili tulingane, hii hadithi hii hakuna mtu anayesikiliza hapa duniani. Wewe ukishindwa na watu wako hapo na Chama chako cha Mapinduzi usipotoa *subsidy* kwa ajili ya wakulima wako, *it is up to you,* lakini unaitoaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wewe unaruhusu mfumo hii mbolea inayotoka Dar es Salaam ikiwa inapita Chalinze utajuaje kwamba hii ni ile ya *subsidy* inaelekea Mbozi na hii inayokwenda Kilimanjaro hawapo kwenye *subsidy?* Ukisharuhusu mifumo miwili mfumo mmoja uta-*undermine* mfumo mwingine *especially* unapokuwa umetamka kwamba, nchi hii sasa inaingia katika *the law of competition, the law of demand and supply and the law of value* kwa sababu kitakacho-*determine* bei ya mbolea itakapofika Kagera ni kuadimika au kutoadimika kwa mbolea. Ikifika pale ikakuta hakuna mbolea bei inakwenda Sh.25,000, Sh.26,000, hakuna cha kwamba wewe ulipata *subsidy* ya Serikali pale, kitakacho-*determine* pale ni kwamba, hakuna mbolea kwa hiyo unatakiwa utoe ile mbolea kwa bei yoyote ile. Serikali ituambie hivi unafanyaje? Maoni yangu peleka mbolea mpaka Kilimanjaro halafu kutoka pale anza ku-*determine* hiyo bei unayotaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halafu watu wengine wanatuambia hivi unajua tuko kwenye Soko Huria, kwa hiyo, tusiingilie kati, kwa vipi? Serikali inaweka *subsidy* kwenye mbolea halafu kule mbele usimwambie *DAS, RAS,* Mkuu wa Mkoa na Mkuu Wilaya,

wasimamie kuona kwamba bei hizi zinakwenda? Msome David Ricardo, Adam Smith, Lord Canes, wote wanakuambia mahali popote ambapo kuna matatizo kama haya Serikali itaingilia kati. Hapa sisi tunasema ooh unajua lazima nguvu za soko zifanye kazi, zimeshindwa. Anataja David Ricardo na Adam Smith mahali popote ambapo pana *market failure,* Serikali itaingilia kati, mahali popote ambapo panahitaji mtaji mkubwa Serikali itaingilia kati. Nimeacha kina Lenin na Marx kwa sababu naona hatuelewani humu, nawataja basi na hao wakibepari sasa ili tuelewane. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, hao wa kibepari ndio Mheshimiwa Lowassa wanaokuambia hivi mahali ambapo ni *sensitive* kwa *economy* ya nchi, Serikali itaingilia kati. Ninyi mnaona inatokea tatizo pale mtu tumeshampa *subsidy* mbolea bei ni ile ile halafu unasema ni sawa. Tunampa *subsidy* hapa tunamwambia hutalipa ushuru chakula kinakwenda mpaka kule, bei ni ile ile, Serikali ni lazima iingalie kati wanasema kina David Ricardo, Adam Smith wala sio akina Marx acha kina Marx sasa maana yake wanaleta shida, hao hao mnaosema hao. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mwisho ni kuhusu barabara. Mheshimiwa Mramba, barabara itakwenda mpaka pale Tarekea, mpaka pale Kamwanga. Nimekwenda Kenya nimeona wanavyofanya Mlima ule wa Kenya tu wamewapeleka barabara zote pale, wamezirundika pale sisi hapa bajeti yetu 45% inategemea watu kutoka nje. Tunasema hivi barabara ile ambayo Serikali imepanga kujenga na hii najua namsemea Mheshimiwa Edward Lowassa, Mheshimiwa Lekule Laizer na wananchi wote wa Jimbo la Siha, barabara ile izunguke moja kwa moja badala ya kufika mahali inafanana na ndizi au mbalamwezi inapotokea asubuhi, izunguke mlima mzima barabara itoke kutoka pale Kamwanga - Ngarenairobi - Sanya Juu - Boma Ng'ombe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. PHILIP A. MAGANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hizi mbili ya Waziri wa Fedha na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza, napenda kuchukua fursa hii kuungana na Wabunge wenzangu waliotangulia, kuwapa pole Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kupotelewa na baba yao mpendwa, Mzee Omar Kigoda. Tunaomba Mwenyezi Mungu, aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amin.*

Vile vile napenda kuchukua nafasi hii kama walivyofanya Wabunge waliotangulia, kumpongeza Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kuchaguliwa tena kuwa Mbunge safari hii kupitia tiketi ya CCM. Hii inaonyesha imani ambayo wananchi walikuwa nayo kwake yeye kama Mbunge kwa wananchi wa Bariadi Mashariki. Pia napenda kuwapongeza Wabunge wote ambao kwa kupitia tiketi ya Bunge hili, wamepata fursa mbalimbali katika mashirika mbalimbali duniani akiwemo jirani yangu Mheshimiwa Balozi Getride Mongella, ambaye amechaguliwa kuwa Rais wa Bunge la Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nielekeze pongezi tena kwa Mawaziri hawa wawili pamoja na wasaidizi wao. Kwa kweli kama walivyosema waliotangulia, wametuletea bajeti na mipango ya maendeleo ambayo kama ikitekelezwa inaleta matumaini.

Mheshimiwa Spika, nitajikita zaidi katika sekta ya kilimo, sekta ambayo waliotangulia wameizungumzia sana nami nichangie kidogo sio kwamba nina jipya, isipokuwa naendeleza kilio ambacho kimesemwa na waliotangulia kwamba, jinsi gani sekta hii imelala na inatakiwa iamshwe ili isaidie maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa kilimo umekubalika na umesemwa na Mawaziri wote wawili, Waziri wa Fedha amezungumzia na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji amezungumzia. Aidha, juzi siku ya Jumamosi katika uzinduzi wa Ripoti ya Pili ya Hali ya Umaskini iliongelewa kwa undani sana jinsi gani sekta ya kilimo ingeweza kusaidia katika kuondoa umaskini uliokithiri hususan vijijini. Kwa mfano, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsiahaji, katika *paragraph* ya 37 ya hotuba yake amesema, naomba kunukuu: "Kukua kwa Pato la Taifa kunategemea kwa kiasi kikubwa akuaji wa sekta ya kilimo." Waziri mwenyewe anakubali. Kwa hiyo, kama juhudi hazifanywi katika kuendeleza sekta ya kilimo, maana yake ukuaji wa Pato la Taifa kwa asilimia tulizoweka hapa hatutafikia kwa vile tumesahau au kudharau sekta ambayo ingetoa mchango mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, malalamiko ambayo yametolewa hapa na waliotangulia juu ya sekta ya kilimo yanaonyesha wazi kabisa msingi wake mkubwa ninavyotafsiri mimi ni ukosefu wa mipango ya maendeleo ya sekta ya kilimo. Kama kungelikuwa na mipango ya maendeleo ya sekta ya kilimo iliyowazi kabisa ukizingatia ardhi, mabonde, maji na mifugo tuliyonayo, nadhani malalamiko ya Wabunge yangepungua sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huko nyuma kulikuwa na malalamiko juu ya kuzorota kwa sekta ya elimu hususan Elimu ya Msingi. Kwa bahati nzuri tumempata Waziri mwanamapinduzi ambaye baada ya kusikia kilio hiki cha wananchi alikaa na wataalam wake na wakabuni Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi. Mpango huu ulizamia kwa undani kabisa kubaini matatizo ya Elimu ya Msingi na nini tufanye ili kuibua matatizo hayo. Wakaanzisha Mradi wa MMEM, ambapo kwa kweli ni mradi ambao umekubalika na mafanikio yake yanaonekana wazi. Kila unapokwenda, kila Wilaya, kila Kata, wanaufahamu mpango wa MMEM kwa sababu maandalizi yalikuwa mazuri na wahusika wote walishirikishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani sio vibaya kwa wahusika wa sekta ya kilimo na hapa nikisema kilimo namaanisha kilimo cha mazao ya mashambani, mifugo pamoja na samaki kwa upande mwingine. Kama wahusika wa sekta ya kilimo wakikaa chini na wataalam wao na kuangalia kwa undani matatizo yaliyozungumzwa na Waheshimiwa Wabunge hapa wakishirikiana na wananchi wao, wangeweza kubuni mradi wa maendeleo ya kilimo hapa nchini. Sio vibaya kuiga kwa wenzako ambao wamefaulu. Kwa maana hiyo ningetoa ushauri kwamba, Wizara ya Kilimo sio vibayakuiga mfano uliooneshwa na Mheshimiwa Joseph Mungai katika kuibua matatizo yaliyokuwepo

katika Elimu ya Msingi hapa nchini. Wataalam wapo, wala hatuhitaji wataalam kutoka nje, hapa hapa ndani tunao wataalam ambao wanaweza kutayarisha mradi wa maendeleo ya kilimo kwa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kubuni mpango kama huo kwanza tujue tuna kitu gani, kwa maana ya *resources,* tunayo ardhi nzuri sana, mabonde kama nilivyosema, maji na watu ambapo asilimia 85 ya wananchi wa Tanzania wanaishi vijijini na wanategemea kilimo. Tukiweza kubuni mradi wa maendeleo ulio wazi na ambao unabaini nafasi ya kila mtu na kila eneo toka Taifa, Mkoani, Wilayani, Kata mpaka Kijijini, kulingana na hali ya hewa ya sehemu husika, ukasema kwamba katika eneo hili ni mazao gani mtazalisha na nini mnasaidiwa na wataalam wakawekwa pale wa kuwasaidia wananchi hao katika kutekeleza miradi yao, naamini kabisa tukifanya hivyo tutafanikiwa. Ni lazima tujiwekee malengo. Kilimo ni sekta ambayo haiwezi kuendelea bila kuweka malengo.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, tukitaka kuongeza zao la korosho tunakaa chini na kuchagua maeneo gani tutakwenda kupanua mashamba ya mikorosho na kwa kiasi gani. Kwa hiyo, unagawa kila Kata na kila Wilaya, mwaka huu mtapanda mikorosho eka *so much,* mwaka unaofuata eka *so much* na hivi hivi kwa kila zao ili tuweze kuongeza uzalishaji wa mazao hayo kwa malengo tuliyojiwekea. Kwa mfano, chukua mpunga, mwaka huu unazalisha mathalan tani laki moja, tunataka katika kipindi kinachokuja, miaka mitatu au minne inayokuja, tuwe tumefikia tani mia tatu elfu, inawezekana kwa sababu mpunga ni zao la mwaka. Ukitoa malengo yaliyo sahihi, ukatoa na *inputs* pamoja na utaalam, utaweza kufikia malengo hayo. Maeneo ya kulima mazao haya yapo.

Mheshimiwa Spika, labda niachie hapo katika suala hilo la kilimo, lakini niende moja kwa moja kwenye suala ambalo linahusika na kilimo ambapo napenda kuongelea suala la utoaji wa mikopo kwa wakulima. Nimefurahi sana kusoma katika Hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji kwamba, Serikali imekubali kimsingi uanzishwaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo. Suala hili la chombo cha kuwahudumia wakulima kwa upande wa mikopo limezungumzwa tangu mimi naingia Bungeni lakini mpaka leo sijaona kitu gani kimefanyika. Kwa upande wa Serikali inatakiwa kuhakikisha kwamba tunapata taasisi hiyo itakayoweza kuwahudumia wakulima. Lakini sasa tunaambiwa tu Serikali imekubali kimsingi. Sasa sijui hatua gani zinachukuliwa, naona wanashauriana na Baraza la Tanzania la Biashara, sijui kama hawa ndiyo wataalam wa masuala ya mikopo ya kilimo. Mimi nilidhani wao ni wataalam wa biashara siyo masuala ya mikopo ya kilimo.

Ili uwe na chombo cha kukopesha wakulima unahitaji wataalam, mipango ya kilimo iliyo wazi, unahitaji kubaini kila mkulima anahitaji vitu gani na katika yale anayohitaji ni yapi ambayo yanaweza kupatikana kwa mikopo. Vile vile kwa upande wa walengwa lazima uwe na taasisi ambazo zinaweza kushirikiana na Benki hiyo utakayoiunda katika utoaji wa mikopo kwa mkulima mmoja mmoja kwa sababu benki haitaweza kutoa mikopo moja kwa moja kwa mkulima mmoja mmoja. Kufanya hivyo, itakuwa ni gharama kubwa sana na hivyo kufanya *interest* itakuwa ya juu sana. Sasa kupunguza makali hayo lazima tutumie utaratibu wa taasisi za wakulima wenyewe kama

*SACCOS*, Vyama vya Wakulima kama *TFA* ili viwe *intermediaries* katika utoaji wa mikopo kwa wakulima hawa.

Mheshimiwa Spika, tusipofanya hivyo tutarudi kule kule tulikotoka, tutaanzisha benki ya kilimo halafu itakufa kama ilivyokufa *Land Bank,* kama ilivyotaka kufa *CRDB,* kama tusingechukua hatua za haraka haraka za kuiunda upya. Katika kufanya hivyo, tuwahusishe wakulima kupitia Vyama vyao vya Ushirika. Nataka kusema nini? Nataka kusema kwamba, ukitaka kuwa na benki ambayo inawahudumia wakulima wa Tanzania, wakulima mmoja mmoja, wakulima wadogo ambao wanahitaji pembejeo kidogo kidogo hapa na pale, ni lazima utumie taasisi zao hizi ili uweze kufikisha huduma hiyo kwa wakulima hao. Kwa hiyo basi, naiomba Serikali iweke mkazo mkubwa sana katika kutayarisha Vyama vya Ushirika kwa ushirikiano wa wananchi wenyewe, Vyama vya Ushirika na *SACCOS* ili benki hii itakapoundwa, tayari ikute mtandao wa Vyama hivyo na utoaji wa mikopo kwa wakulima urahisishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa kusema mikopo peke yake siyo mwarobaini, kuna mambo mengine mengi ambayo nimeyataja yanahitajika ili kumfanya mkulima huyu aweze kuongeza mchango wake katika kuinua uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, narudia tena kuunga mkono hoja zilizo mbele yetu na naunga mkono mia kwa mia na nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hizi. *(Makofi)*

**MHE. SHAMSA S. MWANGUNGA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kutoa shukrani zangu kwako kwa kuweza kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo napenda kuanza kwa kutoa pole kwa ndugu zetu, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kufiwa na baba yao mpendwa.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote na Waheshimiwa Mawaziri wote, ambao wamebahatika wameteuliwa katika nyadhifa mbalimbali za Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pongezi zangu za mwisho napenda kumpongeza Mheshimiwa Danhi Makanga, ambaye kwa sasa hivi ni jirani yangu, yuko huku *back-bencher,* kwa kuweza kunyakua tena Jimbo la Bariadi Mashariki lakini safari hii kwa tiketi maarufu na maalum ya Chama imara na madhubuti cha CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wawili, Mheshimiwa Basil Mramba pamoja na Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, kwa kazi kubwa waliyoifanya ya maandalizi mazuri na makini ya Bajeti na Mwelekeo mzima wa Dira ya Maendeleo ya kutufikisha pale ambapo Ilani yetu ya Chama Tawala ilipolenga tufike ifikapo mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuongea, napenda niunge mkono hoja hizi mbili, yaani ya Bajeti na ya Dira ya Mwelekeo wa Maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo naomba nichangie kama ifuatavyo: Napenda kuipongeza Serikali kwa mchango wake mkubwa katika shughuli mbalimbali mojawapo ikiwepo vita dhidi ya UKIMWI ambayo sasa hivi ni mwiba wa Taifa letu. Makongamano mengi, semina nyingi na mafundisho mengi, yametolewa kuhusu vita dhidi ya UKIMWI na imefikia hatua sasa na ni imani yangu kwamba, wananchi wengi wameelewa nini maana ya UKIMWI na UKIMWI unaambukizwa vipi. Sasa basi makongamano na hizo elimu zimefikia kikomo chake tuingie hatua ya pili. Hatua ya pili, ni kuwanusuru wale walioathirika kwa kuweza kupatiwa tiba na pia kuweza kuwapa lishe ya kuweza kurefusha maisha yao.

Mheshimiwa Spika, naomba kazi hii Serikali isiziachie asasi zisizo rasmi ambazo ni *NGOs* na vikundi mbalimbali ambavyo ndivyo vinavyohangaika na kujaribu kutoa tiba na lishe kwa waathirika. Lakini mimi nionavyo ni kwamba, hii ni kazi ya Serikali waingie hatua hiyo kwani tukiendelea hivyo siku hadi siku nguvu kazi yetu inapungua. Kuwa mwathirika siyo kufa, mwathirika anaweza akaendelea kuishi hata zaidi ya miaka kumi na saba na akachangia mchango mzuri tu kwenye Taifa letu ikiwa tu atawezeshwa kurefushiwa maisha yake. Hii imeonyesha wazi hata nchi mbalimbali kama Marekani, tuna kumbukumbu kwamba, kuna baadhi ya watu mashuhuri Marekani ambao imefikia sasa karibu miaka kumi na tano tangu wajitangaze wana Virusi vya UKIMWI lakini bado wanaishi vizuri, wanaendelea vizuri kwa sababu ya dawa na lishe. Kwa hiyo na sisi Serikali yetu ijaribu kufikiria kitu hicho ili tuweze kusaidia nguvu kazi yetu, wale ambao bado wanajiweza waweze kutusaidia katika kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hilo, ningependa pia niongelee kuhusu matangazo ya mambo ya UKIMWI. Kuna matangazo mengi yanayotolewa kuhusu vita dhidi ya UKIMWI, ambayo sasa hivi yapo kwenye *TVs*. Ni mazuri kwa sababu yanatusaidia kuona kivitendo kwamba UKIMWI ukoje, lakini pia mimi naangalia kwa msimamo mwingine je, maadili yetu yakoje kwani baadhi ya haya matangazo ingawa yanavunja ukimya lakini yamepita mipaka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano wa tangazo moja ambalo mpaka mimi linanitia aibu. Linaonekana watu wamekaa, chini kwa chini unaona wanakunana miguu baada ya muda wananyanyuka na *condom* imeonyeshwa. Je, tangazo kama hilo linatufundisha nini na kwa watoto wetu wanaelewa nini? Naomba Serikali pia itupie macho matangazo ya namna hiyo, kwa sababu badala ya kuondoa UKIMWI yanashawishi ngono zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo pia ningependa kuchangia kuhusu biashara ndogondogo. Naipongeza Serikali mia kwa mia kwa hatua waliyochukua kwa kuweza kuwasaidia wale wafanyabiashara wadogo wadogo ambao wanaishia kiwango cha milioni ishirini kwa mwaka. Kwa kweli wamefanya kitu kizuri sana kwa kuwafutia ushuru wa stempu, kwa kuondoa *VAT* chini ya viwango vya mpaka shilingi milioni ishirini na pia kutoa ada za leseni. Kwa kweli hiyo imeleta unafuu mkubwa, mzigo

umepungua na isitoshe ile purukushani ambayo tulikuwa tunaishuhudia kila mara kati ya Maafisa Biashara na Maafisa wa *TRA* wakikimbizana na hawa wafanyabiashara wadogo wadogo, wafanyabiashara wadogo wadogo kufunga maduka yao kwa ajili ya kuogopa kodi, yataisha. Pia nina uhakika kwamba, ukusanyaji wa kodi utaongezeka na kuwa madhubuti.

Mheshimiwa Spika, lakini basi baada ya hayo bado wafanyabiashara wadogo wadogo wana mambo mengine mengi ambayo bado yanahitaji msaada. Ningependa hapa kuongolea mawili tu. La kwanza, hawa wafanyabiashara wadogo wadogo bado hawana uhakika wa kukopeshwa mtaji wa kufanyia biashara. Serikali imeonyesha katika hotuba ya safari hii kwamba, kuna hii *Credit Guarantee Scheme* ambayo wameahidi kwamba, matayarisho yapo katika hatua za mwisho. Lakini bado mimi nina wasiwasi, huyu mfanyabiashara mdogo mdogo hakuna mahali ambapo anakubalika ili aweze kukopa, anazungushwa kila mahali. Atakwenda kwenye vyombo vya mabenki hali itakuwa vile vile na nina uhakika hii *Credit Guarantee Scheme* isipoandaliwa vema tutakuta kwamba, wafanyabiashara wa kati ndiyo watanufaika na hiyo na wale wadogo bado watabakia pale pale. Itakuwa vigumu kumkwamua huyu mfanyabiashara mdogo kiuchumi hata kama tumemtolea hizo kodi lakini hana mtaji atafanya nini, bado atakuwa pale pale.

Kwa hiyo, napenda kutoa tu pendekezo kwa Serikali kwamba, hii *Credit Guarantee Scheme* aliyoianzisha kwa kweli imlenge huyu mfanyabiashara mdogo, imwekee masharti madogo ili aweze kukopa, awe anaingia mlango mmoja anakopa na mwingine anatoka. La sivyo, bado watanufaika wengine, huyu atabakia pale pale, tutakuwa tunachekelea vile vile na kuahidiwa wamepewa huku hawajapewa chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili katika kero ndogo ndogo za wafanyabiashara kuna hili la gharama za umeme ambazo sasa hivi zimeongezeka mara mbili au tatu zaidi. Tuna wafanyabiashara wadogo wadogo ambao tunawaita wana viwanda vidogo vidogo ambao wanaangaliwa chini ya *SIDO* na pia wengine wanajiangalia wenyewe. Hivi viwanda vidogo vidogo vinatustiri sana na kama baadhi ya Mijini hawastiriki lakini kwenye Vijiji bidhaa nyingi wanazotumia, vitu vingi wanavyotumia vinatoka kwenye hivi viwanda vidogo vidogo. Hii gharama ya umeme kiasi ilipoongozeka mimi nina wasiwasi mkubwa sana kwamba, viwanda vingi vidogo vitafungwa kwa sababu hawataweza kulipia umeme. *(Makofi)*

Kwa hali hiyo basi mimi naisihi Serikali iliangalie upya hili suala la kupanda umeme. Hata kama kigezo ni kizuri kwamba kwa nini wanapandisha umeme lakini bado kuna sehemu kubwa ya watu watashindwa kulipia katika kuzalisha vizuri. Pia hizi gharama zimepanda na sasa tunataka watu wote waingie kwenye teknolojia, watu waishi vizuri. Je, mwananchi wa Kijijini kwa gharama hizi mpya ataweza kuingiza umeme nyumbani kwake. Kwa hiyo, wananchi wa Vijijini bado watarudi kwenye koroboi kama zamani, tutabaki wa Mjini ndiyo tunanufaika na huo umeme wetu na hawa tunawadanganya kwani hawataweza kuwa na umeme. Jambo hilo pia naomba Serikali iliangalie upya hata kama kuna sababu yoyote lakini bado tumfikirie mwananchi wa kawaida, mwananchi mlipa kodi na mwananchi mpiga kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la tatu ambalo ningependa kuchangia ni katika sekta ya madini. Katika sekta ya madini kuna hawa wachimbaji wadogo wadogo. Wachimbaji madini wadogo wadogo sasa hivi wanawake wamejitokeza kwa nguvu sana. Wanawake hawa napenda kuwaita ni majasiri na mashujaa. Kazi hii siyo kazi nyepesi wamejiingiza kwenye kazi ngumu, kazi ya kupambana, kazi ya kudhulumiwa na kama wasiposaidiwa hii nguvu kubwa ya wanawake ambao wamejiingiza katika fani ngumu itakwisha.

Mheshimiwa Spika, kina mama katika kujikwamua na kuhangaika ili na wenyewe watambulike wameanzisha Chama chao kinaitwa *Tanzania Women Miners Association (TAWOMA).* Chama hiki kina mtandao mzuri, wapo karibu kila sehemu ambapo madini yanapatikana. Wamejitahidi wamepata na wenyewe vitalu vya kuchimba madini lakini hawana vifaa vya aina yoyote, wanachimba kwa majembe na kwamba wanafanya kazi nzuri kwa sababu pia wachimbaji wao wakubwa ni vijana, wanapata ajira. Lakini sasa kama hawa wasipowezeshwa katika vifaa, wasipopewa mitaji, watakata tamaa, vitalu vile vitaharibika kwa sababu vitalu ni mali yao, mali hii itaendelea kukaa chini. Kwa hiyo, kwa upande huo naomba pia Serikali iangalie hao wachimbaji madini wadogo wadogo hususan wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huko katika kuchimba madini wanawake wapo wa aina mbili, wapo hawa wachimbaji madini na pia kuna akinamama lishe ambao sasa hivi wametapakaa katika kila sehemu ya migodi ya madini. Hawa akinamama pia wanaishi katika hali ngumu kwa sababu hali za kule machimboni pa kulala kwenyewe ni hivyo hivyo bora kunakucha, kazi wanayofanya kule ni nzuri wanahudumia watu wetu, wanahudumia wachimba madini ambao wanaleta uchumi katika nchi yetu. Lakini hawa akinamama zaidi ya kwamba mitaji yao ni midogo kuna tatizo lingine kubwa ambapo mimi nimekwenda kuwatembelea, hili tatizo nimeona ni hatari, tatizo hili ni la UKIMWI. *(Makofi)*

Tusipoangalia kwenye migodi yetu itakuwa ndiyo zalio kubwa la UKIMWI, vijana wetu wengi watapotea huko, hata akinamama waliokwenda kujitolea kazi kule nao pia watakuwa hatarini kwa sababu ya UKIMWI, ingawa elimu inakwenda lakini bado hali ipo pale pale. Mimi mwenyewe nimeshuhudia nikiongea na akinamama kwenye hii migodi, wanaongelea kwamba, kule mtu anapewa masharti anaambiwa kwamba ukitaka kutumia *condom* nitakupa Sh. 2,000/=, usipotumia *condom* utachukua Sh. 15,000/=. Sasa mama kwa kuwa anahitaji mtaji ili aweze kujiendeleza pale aweze ku-*survive* basi atakubali hela nyingi. Kwa hiyo, kwa hali kama hizi mimi naomba Serikali iweze kuangalia haya mambo kwani yanatisha na ni mambo ambayo kama tunacheka kweli tutakuja kuadhirika siku moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo napenda tena kuunga mkono hojahii na naipongeza Serikali na nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. *(Makofi)*

**MHE. SALOME J. MBATIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja zilizo mezani, hoja ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji na hoja ya Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Spika, nami niungane na wenzangu kuwapa pole Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda na Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, kwa kuondokewa na mpenzi baba yao. Pia niwape pole Wabunge ambao wamepata majanga mbalimbali siku za karibuni.

Mheshimiwa Spika, naomba niruhusu pia nimpongeze Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kurudi nyumbani. Alipotea njia lakini akajua kwamba sasa anapaswa kurudi nyumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia uniruhusu niwapongeze Watanzania wote, hasa wanawake na hususan wanawake wa Kilimanjaro, kwa kufanya kazi kwa bidii sana katika kipindi kilichopita cha mwaka mmoja. Pia niwapongeze Watanzania na niwape pole Watanzania wale walio katika Mikoa ambayo ilipatwa na ukame na hivyo kugubikwa na baa la njaa.

Mheshimiwa Spika, sasa niwapongeze Mawaziri wawili, Mheshimiwa Basil Mramba na Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, kwa namna ambavyo kwa kweli wamefanya kazi kubwa ya kutuletea mpango mzuri na bajeti nzuri kwa kuangalia kazi ambayo imefanywa katika kipindi kilichopita na kupanga mipango ya kipindi kijacho. Tusingeweza kutarajia bajeti nzuri au mipango mizuri zaidi ya hii iliyoletwa. Sote tunajua katika kipindi kilichopita tulikuwa na ukame, bei ya mafuta imepanda pia *TANESCO* wamepandisha gharama zao. Kwa kweli katika nchi ambayo ni maskini kama ya kwetu, tusingetarajia bajeti nzuri zaidi ya hii iliyoletwa. Kwa hiyo, mimi moja kwa moja nawapongeza na ninaziunga mkono mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, sisi ni mafundi sana wa kutunga sera kwa ujumla. *We are very good in formulating macro-economic policies* lakini tukiingia katika jinsi ya kushusha sera hizo kwa wananchi si mafundi sana. Ni kweli *performance indicators* zote kwa ujumla wake zimeonyesha hali ya kukua na kwa kweli zimeonyesha kwamba tupo katika mwelekeo mzuri wa kurekebisha hali ya uchumi. Kwa mfano, Pato la Taifa limeongezeka mwaka hadi mwaka kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita ingawa katika mwaka huu tumeambiwa kwamba, limepungua kwa sababu ya matatizo yaliyokuwepo ya ukame na kadhalika. Ni kweli tumeweza kutawala mfumuko wa bei tukabaki katika *single digit* kwa kiasi cha miaka mitano iliyopita na ni kweli tuna akiba ya fedha za kigeni ambazo zinaweza kuagiza mali na tumetoka kwenye uwezo wa kuagiza mali kwa kipindi cha mwezi mmoja na nusu na sasa tupo katika miezi nane. Pia riba ya mikopo imeendelea kushuka kutoka asilimia 28 mwaka 1995 na sasa ni asilimia 13.8.

Lakini hapo hapo tunaambiwa kwamba, tumeshindwa katika mambo ya *balance of payment.* Tumeshindwa kupeleka nje bidhaa ambazo zinapaswa kukidhi *imports* zetu ambazo tunaingiza. Kwa namna hiyo kwa kweli tuna *trade deficit* na ni kwamba, tumeshindwa kabisa kupeleka bidhaa nje tuweze kupata *foreign exchange* ya kuweza kufanya shughuli zetu za ndani. Kwa kweli *deficit* hiyo imeongezeka mwaka 2002 kutoka dola 608.7 na imefikia dola 806 sasa hivi. Kwa hiyo, tunazidi kupata *deficit* kubwa kadri tunavyoendelea. Sasa dawa ya hii ni nini?

Mheshimiwa Spika, dawa ya hii mimi ninavyoona ni *combination* ya njia mbalimbali. Kama ingekuwa ni suala la afya basi tungepaswa kunywa dawa za aina nyingi, *chloroquine,* tungefunga vidonda, tungetoa minyoo, tungekula *panadol* na kadhalika. Sasa hii *vicious circle*, ni lazima tuweze kujua ni namna gani tuivunje. Mimi nafikiri njia mojawapo ni kuongeza *export.*

Tulipitisha Sheria ya *EPZ* miaka mitatu iliyopita hapa hapa Bungeni lakini ni kiasi gani tumeweza kuchochea sera hii iweze kutuletea mafanikio ya *Export.* Ni namna gani tumechukua fursa za *AGOA* na nyingine ambazo zimejitokeza. Ni kweli tuna viwanda sasa vya *NIDA* na *Starapparel* kama alivyotuambia Mheshimiwa Waziri asubuhi, lakini kwa kweli tunapaswa kuongeza bidii katika eneo hili. *NDC* ndiyo waliokabidhiwa jukumu la kuratibu na kuandaa miundombinu ya *EPZ*. Nasikitika kusema kwamba, *NDC* wamekuwa wakipewa shilingi milioni 50 tu kwa kazi hii. Katika mpango wa Mheshimiwa Waziri tumeambiwa tayari wamesha-*identify* Mikoa kama mitano ya kuweza kuendeleza biashara ya *export* na maeneo ya *EPZ* lakini shilingi milioni 50 hizi zitatosha kwa *NDC* kufanya kazi hii? *I think we are not serious. NDC* waliokabidhiwa jukumu hili ni vizuri wakapewa fedha za kutosha za kuanzisha miundombinu katika maeneo haya ya *EPZ* ili waweze kuvutia wawekezaji wa kuweza kuyakodisha maeneo hayo ili nao wazalishe ili kuongeza *export* na hivyo kuchangia Pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, viwanda vinavyochangia *export* kwa njia ya *EPZ* vinatengeneza zaidi nguo, nyuzi, mashuka, *T-Shirts* na vitu vingine, lakini mimi nafikiri kama nchi nyingine zilizoendelea zilivyofanya, nafikiri si vibaya vile vile kuingia katika utengenezaji wa *spare-parts* ambazo tunaweza kutengeneza hapa kwetu tukazipeleka katika nchi za wenzetu wakaweza kuziuza katika mashine mbalimbali ziwe za *computer*, ziwe *duplicating machines* au vitu kama hivyo. Ni lazima tuwe watundu katika eneo hili ili tuweze kuongeza *export.*

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mipango ukurasa namba kumi na nne kuhusu *AGOA* na *EBA,* amezungumza kama ifuatavyo na naomba kunukuu: “Hata hivyo, bado hatujaweza kutumia fursa hizi kwa ufanisi kama wenzetu katika nchi jirani wanavyofanya. Tatizo linalotukwamisha ni pamoja na kutokuwa na uzalishaji wa bidhaa nyingi na bora, miundombinu hafifu na ujuzi mdogo wa masoko na ujasiriamali.”

Mheshimiwa Spika, ninakubaliana sana na Mheshimiwa Waziri lakini ni lazima tukubali vile vile hapa katikati Watanzania tulikuwa hatujaweza kuwa *developed, mind set* zetu zilikuwa ni kama vile tulikuwa tumelala. Naomba nitumie mfano wa kuku wa kizungu. Kuku wa kizungu huwa anaweza kutamba sana kwenye banda lakini ukimtoa nje anabaki pale pale hawezi kusogea. Hapa katikati hatukuzoezwa sisi kufikiria kibiashara, hatukuwa na ujasiriamali, hatukuwa na *entrepreneurial approach* ya vitu, hatukuwa na *business acumen*. Katika eneo hili ni lazima Serikali iweke nguvu zaidi hasa ya kutoa elimu ya ujasiriamali, ni namna gani tunaweza kupata bidhaa bora, ni masoko gani tupeleke bidhaa hizo, pembejeo ni namna gani na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, pia nigusie wafanyabiashara wadogo wadogo. Ninafikiri pamoja na juhudi zinazofanyika Dar es Salaam lakini nafikiri *we are yet to organize* na ku-*coordinate them* katika *groups* na *groups* hizi ziwe ni biashara ambazo zinafanana ili Serikali iweze kuwahudumia vizuri katika masuala hayo yote ya elimu katika kuwaelimisha kuhusu masoko na kadhalika. Ninaamini kabisa wafanyabiashara wadogo wadogo wakiweza kuwa *grouped* na kuwa *organized* katika vikundi mbalimbali si kwamba watapata manufaa wao tu na kupata ujuzi na kupanua upeo wao wa biashara lakini Serikali nayo itapata kodi kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Waswahili wanasema kwamba: "Maji ukishayavulia nguo lazima uyaoge." Sisi tumeuvulia nguo utandawazi hatuna namna ya kufanya ni lazima tuoge maji ya utandawazi na katika hili mimi nafikiri sasa *is high time* Serikali iangalie uwezekano wa kuanzisha *internet services centres* katika Miji na siyo mikubwa tu hata midogo. Kwa nini nasema hivyo, tunaongelea juu ya *groups*, ushirika na kadhalika na hapa naomba nimpongeze sana *The First Lady,* kwa sababu katika kipindi cha miaka kumi mfululizo, amekuwa akileta vikundi mbalimbali vya akinamama kutoka katika Mikoa yote katika Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (Saba Saba). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maonyesho haya siyo tu yamewapa upeo lakini yamewapa utundu yameingiza *entrepreneurial spirit* kwa wanawake hawa. Sasa wakirudi huko kwao katika masuala ya upangaji bei, masuala ya masoko, masuala ya kujua bidhaa zao zinatakiwa wapi, ni lazima waingie katika masuala ya *internet.* Kwa hiyo, nafikiri si vibaya katika kila Mkoa au katika Miji Midogo, Serikali kufanya mpango wa kuwa na hizi *centers* kuwa na *agent* mmoja na kum-*train properly,* huyu ndiye ambaye ataweza ku-*service* vikundi hivyo.

Mheshimiwa Spika, bidhaa zetu haziuziki kutokana na gharama kubwa na hapa naomba nigusie suala la umeme ambalo wenzangu wamegusia sana. Tupende tusipende suala hili lazima tuliangalie. Wamekuja *Net Group Solution* lakini sidhani kama wameleta *solution* yoyote ya umeme, lililotokea ni kuongeza ruzuku kuwa *subsidized,* lakini sidhani hata siku moja wamekalishwa watu hao wakaambiwa twambieni tangu mmekuja mmefanya nini na mmepata matatizo gani? Sisi hatujasikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumezungumza kuhusu suala la mboga mboga na matunda na kuhusu suala la *value addition.* Ni kweli tumehamasishwa kwamba ni lazima tuongeze *value* ya mazao yetu tunayolima na kadhalika. Lakini ni kiasi gani tumewafuata watu hawa katika maeneo yao ya kazi kuangalia kwamba sera zetu zimeshuka hadi huko chini. Ni namna gani kwa mfano, wazalishaji wa Lushoto wa mboga mboga na matunda wanafanya usindikaji huo na wanaongeza value. Tunachosikia tu ni vyombo mbalimbali kuita watu hawa mijini na kuwafanyia semina, kuwaonyesha namna ya kutengeneza jams, *juices* na kadhalika. Kwa nini wasiwafuate hawa watu huko walioko ili waweze kujua matatizo yao na ili waweze kusimamia usindikaji huo na kujua mahitaji yao ya masuala haya ya *juices, pineapple* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, suala la madini sasa hata sisi tunaanza kupata wasiwasi, hata sisi ambao tulikuwa hatuamini yanayozungumzwa kwamba huenda tunaibiwa lakini sisi wengine tumeishaanza kuamini kwamba yapo maneno katika nyanja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtu hawezi kuamini kirahisi akiambiwa kwamba sekta hii hadi sasa ni mwaka kama wa tano hivi tangu wameanza kuchimba madini kwa kiasi kikubwa kwamba hadi sasa sekta hii inachangia asilimia 3 tu katika Pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mpango na nafikiri ni hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha amesema kwamba imeundwa *Commission* ya kufuatilia jambo hili. Ninaomba hilo lifanyike mapema kwa sababu kuna leo na kesho. Nchi hii mimi nafikiri inawajibika kwa wananchi wake milioni takriban 34 hivi, wawajibikaji watakuwa siyo sisi tu tuliokuwa katika Wizara leo, lakini vilevile wale walioanzisha Mikataba hii. Ni vizuri sana Tume hiyo iliyoundwa ifanye kazi yake kwa haraka kwa kweli itupatie majibu na kama ni kusahihisha tusione aibu kujisahihisha. Mimi nafikiri gharama ya kusahihisha au kurekebisha mikataba ni ndogo zaidi ya hasara ya nchi inayopata na aibu ya kuambiwa kwamba tunaibiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia jedwali namba 3 ukurasa wa 62 kuhusu thamani ya bidhaa za asili na zisizo za asali zinazouzwa nje ya nchi kwa kipindi cha miaka mitano hivi iliyopita unaona kwamba bidhaa ambazo siyo za asili ni nyingi zaidi ya bidhaa za asili.

Mheshimiwa Spika, hii ashirio lake ni nini? Mimi nafikiri hii inaashiria sasa *is higher time* tume-*concentrate* vilevile si katika mazao ya asili tu lakini tuchanganye na mazao mengine. Ni lazima tuweke mkazo katika mazao ambayo siyo ya asili kwa mfano, mazao ya misitu, asali, samaki mboga mboga, matunda na mazao mengine hata pilipili, maparachichi, nyanya mwitu na kadhalika na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, hata humu ndani ya nchi ni lazima tuweze kuchanganya mazao haya. Nikitoa mfano wa Kilimanjaro bei ya kahawa imeshuka.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga hoja mkono. *(Makofi)*

**MHE. BERNADINE R. NDABOINE:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii nami kuwapa salaam za rambirambi Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda kwa kuondolewa na mpenzi baba yao, naomba Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nichukue fursa hii kuwapa pole wale wote waliokumbwa na mikasa wakati huu. Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, kwa ajali ya gari, Mheshimiwa Estherina Kilasi kwa ajali ya gari pia na Mheshimiwa Anne Malecela kwa kukumbwa na tatizo la majambazi.

Mheshimiwa Spika, naomba nami nimpongeza Mheshimiwa Danhi Makanga kwa ushindi alioupata wa Jimbo la Bariadi na kurudi tena Bungeni kwa tiketi ya CCM. Karibu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nichukue fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote wawili, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji pamoja na watendaji wao kwa kutayarisha Bajeti hii na mwisho kuiwasilisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii ni Bajeti ambayo ina mwelekeo wa maendeleo. Bajeti hii ina mwelekeo wa maendeleo kwa sababu imegusia kilimo ambacho ndiyo uti wa mgongo wa nchi yetu. Itakumbukwa kwamba mimi katika kuchangia kwangu mara ya kwanza humu Bungeni nilichangia juu ya kilimo. Niliishauri Serikali kwamba nchi yetu isingekuwa na umaskini kama tungewekeza katika kilimo. Nilisema kwamba ikiwa vijana wetu wangepelekwa mashambani wakapewa mahitaji yote wanayoyahitaji, kwa mfano, mahema, wakaweza kulimiwa kwa matrekta, wakapewa pembejeo, wakapewa mbolea hayo yote kama mikopo na baada ya kulimiwa wakatafutiwa masoko ya mazao yao na gharama zote zikakatwa kwenye mapato yao ya kilimo, nadhani nchi yetu ingekuwa imepiga hatua mbele na tusingekuwa na shida ya njaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo Mkoa wa Kigoma kama nilivyowahi kusema una ardhi nzuri safi ambayo inafaa kilimo, lakini ni Mkoa ambao umesahaulika sana. Mkoa wa Kigoma hauna njia za mawasiliano, reli ambayo ndiyo tegemeo pekee kwa Mkoa Kigoma ina matatizo, mabehewa yameisha muda wake, injini zimeisha muda wake, lakini vilevile reli yenyewe ni ya mwaka 1905, ajali za mara kwa mara, na kutokana na hiyo kunakuwa na migomo ya wafanyakazi na hii yote ni kwa sababu reli haitoshelezi tena matakwa ya Watanzania kwa sababu haina uwezo.

Mheshimiwa Spika, nashangaa sana kwa nini Serikali isiisaidie *TRC,* mbona kuna fedha za barabara, Mheshimiwa John Magufuli amejitahidi sana ametengeneza barabara katika nchi nzima lakini hakuna fedha za kuweza kuinusuru *TRC.* Naiomba Serikali ijitahidi angalau katika kipindi hiki ambapo *TRC* haijabinafsishwa ijaribu kuisaidia *TRC* iweze kuwasaidia wananchi hasa wale ambao hatuna barabara, wananchi wa Kigoma ambao njia yao pekee ya kuwafikia ni reli, kwa sababu barabara ni mbovu, tunayo barabara moja tu ya kutoka Mkoa wa Kigoma ambayo ni ile inayounganishwa na Kagera. Lakini na vilevile na hiyo barabara kwa sasa imeanza kuharibika. Tunategemea mpaka watakapoitengeneza kwa kiwango cha lami na muda wa kuitengeneza kwa kiwango cha lami haujulikani wanasema mpaka mwaka 2007, je, wakati huu tutafanya nini?

Mheshimiwa Spika, tunaomba barabara ya Tabora hadi Kigoma ipitike, nilishawahi kusema kwamba barabara hii haina daraja, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi alisema kwamba liko daraja, lakini daraja hili lililopo naweza nikasema kwamba lime *hang hang* tu halipitiki, lipo daraja lakini hakuna barabara. Wananchi wa Kigoma ambao tunategemea kwamba wanaweza wakalisha nchi nzima kwa chakula watapitisha wapi hiki chakula ikiwa reli ni mbovu na barabara haipitiki. Wananchi wa Kigoma

ambao wanalima sana wako upande wa Kusini, wanapaswa wavuke mto Malangarasi, huu mto Malangarasi unahitaji kivuko cha uhakika au unahitaji daraja, lakini mpaka sasa katika Bajeti hii hakuna fedha zilizotengwa kutengeneza daraja hili au kutuwekea kivuko chenye uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa ana-*wind up* atueleza ni kwa nini wananchi wa Kigoma wanasahaulika kwa kiasi hicho, kiasi cha kwamba wanatengwa kabisa katika nchi yao. Licha ya kutengwa kwa mawasiliano na Mikoa mingine ya Tanzania vilevile tumetengwa na nchi jirani. Tuna tatizo la wakimbizi, wakimbizi ambao tumewahifadhi sisi wenyewe wanatufanya tuwe wakimbizi katika nchi yetu. Wananchi wanashindwa kulima na wakilima mazao yao yanaibiwa yakiwa mashambani na hao hao wakimbizi. Tumeshuhudia mara nyingi mihogo inachimbwa, tumeshuhudia mara nyingi kwamba watu wanaporwa mali zao, wanauawa Ziwani, wanauawa porini na ulinzi wa uhakika hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti hii sikuona mahali popote ambapo fedha zimetengwa kwa ajili ya ulinzi ikiwa ni pamoja na watu wa Kigoma. Tumesema mara nyingi na nakumbuka Mheshimiwa Rais wa nchi alisema kwamba wakimbizi sasa ndiyo mwisho warudishwe makwao. Hatua ya kuanza kuwarudisha imeishaanza lakini nasikitika kuona kwa nini hizi hatua zinakwenda pole pole mno. Burundi sasa hivi ni shwari sioni kwa nini wasirudi makwao au wakawahifadhi makwao. Kwa sababu tunapata matatizo na madhara mengi zaidi kutokana na ujio wa wakimbizi kuliko tunavyofaidika. Kwa nini hawahimizwi hao ambao wanawahifadhi wakimbizi wasitutengenezee barabara na kwa nini wasitusaidie katika ulinzi. Inasikitisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niongelee upande wa Afya, wananchi walio wengi wana matatizo ya kiafya, lakini wanawake na watoto ndiyo waathirika zaidi. Katika bajeti hii nimejaribu kuangalia fedha zilizotengewa kwa uhai wa mama na mtoto. Aidha hakuna katika Mkoa fulani au zilizotengewa ni kidogo mno. Tunapokuwa vijijini tunashuhudia mara nyingi akinamama wanajifungulia chini hakuna vitanda vya kujifungulia.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kigoma umekuwa wa kwanza kwa ongezeko la watu la 4.8 ni watoto wengi wanaozaliwa, sasa tuwaue hao watoto kwa kutowapa huduma siyo kosa lao. Tunaomba fedha zitengwe kwa ajili ya huduma ya mama na mtoto kwa Mkoa wa Kigoma hakuna fedha hata kidogo ambazo zimetengwa katika kasma hii. Kwa sababu tunazaa sana, tunaomba wanawake na watoto katika Mkoa wa Kigoma wapewa kipaumbele kwa upande wa afya.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nichangie kuhusu wastaafu. Nilitumwa mara nyingi kuwatetea hawa wastaafu na ninaomba waliopo katika Mkoa wa Kigoma akina Mzee Chubwa wanisaidie kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kuwarudisha katika *Pay Roll*. Ninachoomba zaidi ni kwamba wako wastaafu wengine ambao wameishapoteza kumbukumbu zao, kwa hiyo naomba wasaidiwe hata kwa kuonyesha

cheti cha kuonyesha kwamba bado wangali hai kiwe ni uthibitisho wao ili waweze kurudishwa katika Pay roll. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Fedha kwa kuweka mikopo ya masharti nafuu kwa wafanyabiashara wadogo wadogo pamoja na wenye viwanda vidogo vidogo. Lakini naomba pia katika hili hayo masharti nafuu yawafikie hao hao walengwa wayafahamu na kwa hiyo wanahitaji mafunzo. Kuna vijana wengi ambao wana ujuzi. Nikitoa mfano wa kijana mmoja ambaye yeye ana uwezo wa kutengeneza *test tubes,* nchi nzima sasa hivi tunaagiza *test tube* kutoka nje. Huyu kijana amekwama kwa kuzunguka katika sehemu nyingi ameenda *SIDO* wakasema hawana msaada huo, kwenye benki hawezi kukopeshwa kwa sababu hana dhamana. Naomba kwa msaada wa Mheshimiwa Waziri basi huyu kijana aweze kusaidiwa ili aweze kutengeneza vyombo vya maabara ambavyo vinahitajika katika shule zetu kusudi na wanafunzi wetu waweze kuwa mstari wa mbele katika karne hii ya Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Naungana na wenzangu kwanza kabisa kuwapa pole wale wote waliopata matatizo tangu kipindi cha Bunge lililopita na hasa Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Dr. Aisha Kigoda nawapa pole kwa msiba wa baba yao.

Pili, naomba niwapongeze wale wote waliopata nyadhifa mbalimbali na hasa kaka yangu Mheshimiwa Danhi Makanga kwa kupata Ubunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, naomba na mimi nichangie. Nawaomba ndugu zangu Waheshimiwa Mawaziri wawili, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Basil Mramba msikatae tamaa kwa virungu tunavyowapa. Hii ni kwa sababu tunawasukuma ili tuendelee. Maendeleo hayana mwisho, ukiwa unakwenda kwa miguu, ukipata baiskeli utataka gari, ukipata gari utataka treni, ukipata treni utataka ndege, kwa hiyo haya yote ni kuwasukuma nyie muweze kuweka mipango vizuri kwa hiyo msikate tamaa.

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa naomba tu hili nitakalolitamka nieleweke vizuri na ninaomba Waandishi wa Habari wanielewe vizuri. Tukitaka tuondoe umaskini lakini tuelewe kuwa utajiri ni utukufu, umaskini ni udhaifu, kwa hiyo kila tunapozidi kuendelea kuwa maskini maana yake mipango yetu ni dhaifu. Kwa hiyo mimi naomba na wananchi wote kwamba tuukubali utajiri ni utukufu, watu watakubaliana na mimi kwamba kuna msemo unaosema: "Pesa ni sabuni ya roho, inaweza ikatoa hata nyoka pangoni." Kwa hiyo tukikubaliana na hilo tukubaliane utajiri ni utukufu na sisi tuhangaike kuupiga vita umaskini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, naomba kabisa nisimame hapa kutoa shukrani zangu kwa Serikali na hasa TAMISEMI na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Mwaka jana nilikaa hapa ninyi wote Waheshimiwa Wabunge wenzangu

mliniona nikizungumzia standi ya Maili Moja, nilikaribia kulia, nilipoambiwa kwamba ninachozungumza si kweli. Lakini naomba nitoe taarifa kwa niaba ya wananchi wa Kibaha na hasa wa standi na kwa niaba yangu TAMISEMI imejitahidi na imeondoa kero ya wananchi kabisa, naomba niishukuru Wizara ya TAMISEMI. Wale Maaskari waliokuwa wanazurura ovyo kumlinda Saru ili wapate hela hawapo sasa, ukiwaona wamekuja kwenye basi au ni matrafiki. Kwa hiyo mimi naomba kabisa kwa dhati kuishukuru Serikali kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia naomba niishukuru bado Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi hasa *RPC* wa Mkoa wa Dodoma sasa hivi ujambazi umepungua. Kwa kweli ninaomba Mikoa mingine iige Mkoa wa Dodoma. Ilikuwa hapa watu wanauawa ovyo na wanapigwa ovyo, lakini sasa kazi anayoifanya *RPC* wa Dodoma naomba tumpongeze. Naomba na mimi nitoe wito kwa *RPC* wangu aige Mkoa wa Dodoma. Ikitokea mtu anakwenda kuripoti tukio la wizi inachukua wiki nzima au mwezi mmoja ndiyo Askari anakwenda kwenye tukio. Kwa hiyo, naomba na mimi *RPC* wangu wa Mkoa wa Pwani aige Mkoa wa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, mimi nilikuwa nataka Wizara ya Ujenzi bahati mbaya siwaoni, lakini Serikali ipo wanielimishe tulikubaliana hapa kwamba nyumba za Serikali zitanunuliwa kwa wale wanaoishi katika nyumba hizo wafanyakazi, tulipiga piga makelele lakini mwisho tulikubaliana. Lakini kuna kitu kingine kinatokea na kinanishangaza. Ujenzi ilipewa maeneo mbalimbali ya kujenga nyumba, lakini kuna maeneo ambapo hawakuweza kujenga nyumba yakabaki viwanja. Mfano, Kibaha eneo ambalo linakaribia Mwanarugari walijenga nyumba na kweli watu mbalimbali walipewa kwa utaratibu mzuri tu.

Mheshimiwa Spika, lakini kinachonishangaza kitengo cha ujenzi sasa hivi kimechukua maeneo yale ambayo hawakujengwa yamekaa kama viwanja au mapori wameanza kuyapima na kugawia watu bila ya kushauri wa Halmashauri au Mji wa Kibaha na wanawauzia wengine mpaka kwa shilingi laki tano. Je, Wizara ya Ujenzi tulikubaliana hivyo? Nimemuuliza *DED* wa Mji akasema hajui, wakasema wanaopima ni Halmashauri, nikwenda kwenye Halmashauri wakasema hivi, aah sisi kitengo cha Ujenzi ndiyo kimetupa fursa hiyo tuwapimie, nikawauliza kwa nini waje kwenu Halmashauri wasiende katika Mji mdogo. Sasa mimi naomba nifafanuliwe hapa kusiwe na ujambazi na fedha zile zinakwenda wapi na zinafanya nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningeomba Serikali niwaombe sana wananchi wetu hali zao ni duni wanapochangia miradi basi tuhakikishe miradi ile inakuwa endelevu au miradi ile isihujumiwe. Nitatoa mfano wa shule iliyoko Mbwewe, shule ile ilijengwa kwanza kwa nguvu za wananchi lakini baadaye ikaingia kwenye huu mradi wa MMEM, cha kusikitisha ile shule imeishawekwa alama ya X inavunjwa iko barabarani wakati ikijengwa Maafisa Ujenzi wa Wilaya waliokuweko hawakusema kama iko katika maeneo ya barabarani, je, hakuna *coordination* kati ya Idara zetu za Ujenzi za Wilaya? Je, baada ya kuvunjiwa Serikali itagharamia tena kujenga pale maana wananchi wetu hawana fedha kule. Mimi nilikuwa naomba hili nifafanuliwe hii shule ya Mbwewe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu chakula cha njaa. Naomba basi tukikubaliana kuna njaa na tukaweka muda wa kugawa chakula iwe kwa muda unaotakiwa. Inasikitisha chakula kinachelewa watu wanaanza angalau kudokoa dokoa mahindi ndiyo chakula cha njaa kinaletwa. Kwa mfano Jimbo la Chalinze. Kwa hiyo, mimi hilo nilitaka nilizungumze.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine nilikuwa naomba niulize kuna milioni 61 *arrears* za walimu katika Wilaya ya Bagamoyo zilitumiwa vibaya, walimu hawajapewa *arrears* zao katika Wilaya ya Bagamoyo milioni 61. *DED* na Kamati yake ya fedha na Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha walizi-*mis allocate* au *misuse.* Je, walimu hao hizi fedha watapewa na fedha hizi zilitolewa Hazina? Je, *DED* na wale Madiwani waliokaa wakazihujumu hizo fedha wamechukuliwa hatua gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, labda ninaloomba lingine nisaidiwe mradi wa maji, nashukuru sana katika Jimbo la Bagamoyo na katika Jimbo la Chalinze tumepata maji wananchi walikuwa wanapata shida hasa pale Chalinze nafikiri mlikuwa mnawaona naishukuru sana Serikali. Lakini wananchi wanauliza huu mradi wa maji ni lini utapelekwa Kwangwandu, Kwaruhodo, Kibindu, Kwamduma, Kiwangwa, Pogwe, Ubena na vijiji vyake na Tarawada. Kwa hiyo mimi nataka msaada. Lingine nasema kuna tatizo sasa hivi katika barabara hii ya Mtwara hadi Dar es Salaam tusipoangalia itaharibika kabla haijamalizika kutengenezwa. Sasa ukitazama magari yanayobeba magogo na wanafanya ujanja wakifika karibu na Mkuranga wanayateremsha kwa sababu kuna *weighing bridge* kama wanakwenda Dar es Salaam, lakini huku nyuma magari hayo yanapita yakiwa mazito mazito. Kwa hiyo, mimi naomba hili litazamwe vizuri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *TASAF.* Mradi wa *TASAF* ni mzuri sana kabisa lakini ninaomba tuwe tunauchunguza hasa watendaji wetu wanauhujumu. Utakuta wanaambiwa kujenga hospitali au kujenga shule analeta *document* anasema nimenunua mabati ya *gauge 28,* lakini ukitazama mabati yale ni *reject. Reject* kabisa na katika Wilaya ya Kibaha tumethibitisha hiyo. Sasa mimi naomba Serikali itazame huu mradi ama siyo unahujumiwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu dampo la Tabata ingekuwa nchi za wenzetu wengine Serikali ingeshitakiwa. Wananchi walikwenda pale walijenga kwa utaratibu uliokubaliwa, lakini baadaye Serikali ikaenda ikapeleka dampo, nenda katazame watu wa maeneo yale wanaathirika kiafya, wanajikuta moshi unawaathiri wakati wote, moto unalipuka muda wote na harufu inatishiamaisha na nyumba nyingine zinaporomoka. Sehemu nyingine ya uchafu unaingia ndani ya maji unakwenda baharini. Nafikiri ingekuwa katika nchi zingine Serikali ingeshtakiwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *PCB* mimi naomba niipongeze *PCB* kwa uhakika kabisa hasa baada ya kufika *PCB* sasa iko Wilayani. Ninachoomba tuanze sasa mikakati ya kuelimisha wananchi kuhusu suala la rushwa, na mimi kwenye hili naomba nizungumzie, imeandikwa ndani ya gazeti watu wakanipigia simu sana Dr. ninaomba niirudie hapa. Linasema hivi: "Kiongozi akiingia madarakani kwa njia ya rushwa na

hasa sisi Waheshimiwa Wabunge na hasa hasa ukipata Uwaziri huwezi kusimamia rushwa, *grant corruption* itazidi na ikizidi *petty corruption* itazidi." Ninasema tunalazimika sisi viongozi tuhakikishe rushwa haipo hasa sisi tunaoingia Bungeni. Lakini nilisema mwakani ni mwaka wa uchaguzi. Uchaguzi wa Rais sasa hivi Rais wetu aliyetusaidia kwa kufanya kazi nzuri ya kupambana na rushwa anaondoka. Sasa tuwaangalie hao wanaotaka Urais wasiwe wala rushwa na tuwaangalie kuanzia sasa mpaka hapo watakapojaza fomu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme, tunazungumzia suala lazima la umeme na mafuta kupanda bei na tunalipongeza na tunalizungumza. Lakini wamepandisha umeme na mafuta, wenye magari wanapandisha nauli mnalalamika na mnawalazimisha, na mnasema hamsimamii bei, lakini umeme sawa, mafuta sawa, watu wa magari wakipandisha nauli tatizo tutawadhibiti, mnawanyanyasa. *(Makofi)*

Mwisho, Mheshimiwa Spika, ni kwamba waliokwenda nchini Canada wamekuta kuna nafasi tumepewa sisi Watanzania za masomo, nafasi sita (6) kila mwaka sasa hivi hazitumiwi na Tanzania kwa nini, tunaomba tupewe jibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu *East African Legislative Assembly (EALA)* imekaa kama haina mzazi ni watoto yatima. Tunawachukua Mawaziri wa nchi za nje ndiyo wanaosimamia kule, lakini inasikitisha hawana muda hao Mawaziri, naomba tuwawekee Mawaziri wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri wa Kilimo aliahidi kutupa mashine za kubangua korosho 140, wananchi wa Mkoa wa Pwani wanasubiri mashine zile amewadanganya. Alikuja akatuonyesha hapa mifano ya mashine ya kutoa unga wa mhogo ziko wapi, watu wanazitaka mpaka Mtwara, hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, daraja la Mkapa linahujumiwa ndugu zangu tuhangaike. Waziri wa Mambo ya Ndani naomba ifanyiwe kazi wanaondoa nati zile. Inatuuma sisi wengine ambao kweli ni watu wa Mkoa wa Pwani. Naomba tulifanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo nasema kaka zangu wawili wote naipongeza Bajeti na naiunga mkono ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru na mimi kunipatia nafasi niweze kuchangia hoja hii ya Bajeti.

Kwanza nitoe pole kwa Mheshimiwa Abdallah Kigoda na familia yake kwa msiba walioupata.

Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri Serikali haiko *serious* kwenye mambo ya kilimo, kuna mchezo! Kama tunataka nchi yetu iendelee wote kwa pamoja tunasema ni lazima tunyanyue kilimo. Kilimo kimepewa majina mengi ni uti wa mgongo, ni sekta Kiongozi. Sasa kilimo hicho ukiangalia Bajeti ya mwaka jana, *Development Budget* ilikuwa shilingi bilioni 31. Bajeti yake ya mwaka huu ni shilingi bilioni 29. *Are we*

*real serious?* Tunasema tunanyanyua kilimo. Mauzo ya nje yanazidi kupungua. Rais ametuambia hapa. Tumeshindwa kushindana kwa sababu hatuuzi. Fedha zetu zinapungua thamani kila siku kwa sababu hatuuzi, lazima tuelewe hilo kuwa watuwetu ni wachumi wanaelewa hilo. Hatuuzi, hatuna cha kuuza zaidi ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, leo hii tunapunguza Bajeti kutoka bilioni 31 hadi 29. Kwa kweli ningeiomba Serikali iwe *serious* kwenye kilimo. Serikali yetu ya Tanzania ielewe kabisa kwamba nchi yetu tumekalia utajiri na hakuna utajiri tulioukalia zaidi ya kilimo. Tuna mito mingi nchi hii zaidi ya mito 200 na yote ina maji inapeleka baharini. Hatujachukua *seriousness* ya kuchukua yale maji tuweze kunyweshea mashamba yetu Fedha tunazo ndiyo hizo tunazogawagawa. Tunasamehe malipo kwenye leseni, tunasema watu waliokuwa *turn over* yao haifiki milioni 20 hawatakata leseni. Sasa mimi naiona hii Bajeti ni Bajeti ya uchaguzi. Na sio Bajeti hasa ya kuongeza uchumi wa nchi hii. Ni Bajeti kwa ajili ya uchaguzi wa mwaka kesho. Kwa sababu huwezi kusema kwamba unasamehe watu wadogo kulipa leseni huyo mtu mdogo unapomsamehe kulipa leseni *identity* yake itakuwa nini. Kila mmoja atatoka jambazi atasema mimi nafanya biashara ndogo ndogo na sina leseni hii ni vurugu.

Mheshimiwa Spika, nafuu mngesema kwamba leseni ziwepo lakini badala ya kukata leseni kwa Sh. 20,000 unampa kwa Sh. 2,000 ndiyo *identity* afanye biashara huyo labda tungewaelewa. Lakini unasema wawepo tu hata wazururaji watasema mimi nafanya biashara utafanyaje, utamwita mzururaji na wakati atakuambia biashara yangu ni ndogo nafanya hii hapa. Sasa hayo mambo kama hayo tunakojielekeza je tunyanyua uchumi. Mimi sioni kama tunanyanyua uchumi tunajipendekeza tu. Tujipendekeze kwenye kilimo. Tunajaribu kusema hayo.

Mheshimiwa Spika, mwaka juzi katika Bunge la Bajeti nilisema hapa na mimi naomba Mawaziri wachukue ushauri wetu. Nilisema hapa kwamba wanafunzi wanaotoka mashuleni wakopeshwe mashamba hasa wale waliopitia kilimo na wakopeshwe mashamba wapewe mashamba eka tano tano nilisema hapa. Lakini nimekwenda Cairo nimekuta hiyo system inafanya kazi. Kule Cairo *system* hiyo inafanya kazi. Wanafunzi wanakopeshwa eka mbili mbili kwa kule Misri.

Lakini huku nili-*suggest* eka tano tano wakopeshwe halafu wanalipwa mshahara mpaka wanapoanza kuvuna mwaka wa pili ndio wasimamishwe kulipwa mishahara kwani watakula kile walichokuwa wanalima pale hao. Wataleta faida kwa ajira na wataongeza vile vile kipato cha Taifa kwa sababu tutauza yale mazao ambayo watakuwa wamelima pale. Taifa litakuwa limepata yeye mwenyewe atakuwa pia amepata ajira. Sasa haya mawazo wenzetu wa Tanzania kwa nini hawataki kuyachukua. Wakubwa zetu Mawaziri kwa nini hamtaki mawazo hayo. Hayo ndiyo mawazo ya kuchukua ili hizo fedha zifanye kazi tuzalishe, tuuze ili fedha yetu iwe na thamani.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi shilingi moja ya Kenya unatoa shilingi 14 mpaka 15 kupata shilingi ya Kenya. Ni jirani yetu hapa. Dola moja sasa hivi ni shilingi 1,125 mpaka mwisho wa mwaka huu itakuwa shilingi 2,000, kwa dola moja. EE!! Ndiyo haijawahi kushuka. Kila siku inapaa. Lakini sio kwamba hawajui sababu yake ni

kwamba hatuuzi, tuuze nini. Dhahabu zile kule asilimia 3 zote tumekwishawapa wazaungu tunauza nini? Kama hatuwezi kulima tumekubaliana tunajenga barabara ya Rombo ili tupeleke mahindi Kenya. Sasa hayo mahindi umetupa mbolea Mheshimiwa Waziri. Tupeleke mahindi walau tuuze huko tuweze kupata fedha za kigeni . Sasa umetupa mbolea. Hatujapata mbolea. Tunasema tunakuza kilimo, tunakuza uchumi hatuwezi kwenda kw namna hii.

Mheshimiwa Spika, ningeomba tuangalie sana ukurasa wa 38 wa kitabu hiki unazungumzia mipango ya kuendeleza kilimo. Inasema kifungu cha 5 hapa: “Mipango ya kuendeleza kilimo katika ngazi ya Wilaya kwa utaratibu angalau zao moja la chakula na zao moja la biashara utaendelezwa”. Nataka sasa kabla ya kuendelezwa Wizara inieleze. Mwaka jana mgao huo uligawaje na matunda yake ni nini? Nataka nipate taarifa ili niweze kujua tunaendeleza kuanzia wapi. Tujue hilo.

Mheshimiwa Spika, tunaona kabisa fedha inashuka thamani, petroli inapanda, umeme unapanda, tunasema tunamsaidia huyu mtu wa chini. Huyo wa chini anasaidiwaje kwani hatumii umeme? Huyo wa chini anasaidiwaje hapandi Mabasi ya kwenda kazini? Huyo wa chini anasaidiwaje hakodi chumba wakati anatoka kazini kwake? Sasa kama vitu vyote hivyo vikubwa kama umeme umepanda bei nauli za Mabasi zimepanda bei, petroli imepanda bei tunawasaidiaje hawa. Tunasema tunawasaidia je mmewaongezea mshahara?

**MBUNGE FULANI:** Hapana !!!!

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Tunamsaidiaje huyu mtu wa chini. Tunasema hii bajeti ni ya watu wa chini. Nawashangaa watu wa magazeti wanaandika eti hii Bajeti inamsaidia mtu wa chini. Watueleze hili. Mheshimiwa Spika, nakulenga wewe. Atueleze ni namna gani inamsaidia huyu mtu wa chini wakati bei ya petroli bado haijapungua, hakuna *subside* hakuna mshahara uliongezeka, hakuna mkulima aliyepewa mbolea. Hakuna suala la irrigation lililotajwa. Huyo mtu unamsaidiaje, huyo mzururaji tuliyesema azurure na biashara bila leseni ndiyo kweli tunamsaidia mtu wa chini. Naomba tuwe *serious* tuangalie hayo mambo ya kilimo na mimi nitafurahi kweli kweli kama tutafanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, yule mkulima pale Moshi wanalima Kahawa wameniambia nije hapa nimwulize Mheshimiwa Waziri. Dawa ya Kahawa aina ya sumu ya kuua wadudu ni shilingi 9,000 kwa lita moja. Wakati kilo mojaya Kahawa ni shilingi 500/= sasa vinaoana vipi na Serikali inaangalie. Inasema tunamsaidia mtu wa chini. Shilingi 9,000 dawa ya kuua wadudu inaitwa sumu kwa lita moja. Sasa tunamsaidiaje tuna *STABEX* huko hata tupeleke madawa basi wasaidiwe angalau hicho kidogo wanachokipata angalau tununue hizo dawa tuwapelekee. Kwa hiyo, dawa hakuna bado wanaambiwa tunamsaidia mtu wa chini, huyo mtu wa chini anakaa wapi? Wakati analima eka moja tu ya kahawa pale Moshi. Je ni chini ya hapo ya yule anayelima Kahawa au chini zaidi Mimi sijui chini wapi? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naamini wa mwisho ni yule anayelima eka moja tu ya Kahawa hapa nyumbani na yeye hasaidiwi. Sasa ningeomba niweze kusaidiwa kujibu hayo na mimi bahati nzuri huwa naongea na kushauri. Bado nasema Wizara zinazohusika ziangalie mambo ya dhahabu, mambo ya *TANZANITE,* mambo ya madini tunayovuna huku nchini. Tuyaelekeze 50% ziende kwenye kilimo na asilimia zingine ziende kufanya hizo kazi zingine ili tuweze kuzalisha na baadaye tunavuna zaidi.

Mheshimiwa Spika, hivi muda unakimbia kweli. Sawa *anyway!!.* Mimi nazungumzia nina *highlight* sana kwenye mambo ya *COMESA.* Tumejiondoa kwenye *COMESA* tumejidanganya. *COMESA* sasa hivi wenzetu wametushauri kwamba tumeondoka kwenye *COMESA* tumekosea. *COMESA* ina nchi 21 ambazo ni *Member States* ambako tumezungukwa na Congo, Uganda, Kenya na Kaskazini yote ya Afrika. Sisi tunalia na Kusini tu. Leo hii tumeungana kwa Bandari. Hizi bandari tunasafirisha mazao ya *COMESA.* Tunasafirisha mazao ya *Congo,* bidhaa za Uganda, tunatumia Bandari hizi tunasema zimeungana.

Lakini sisi wenyewe tumejitoa kwenye *COMESA. Those people are enjoying our facilities* wakati sisi hatumo kwenye hilo kapu. Mimi nataka nipate maelezo kwa upana sana maana nilikuwa naangalia nisije nikasahau hilo. Nipate maelezo kwa kina ni hasara ngapi tungepata tena kwa hesabu ni hasara ngapi tungepata kama tungeendelea na *COMESA* na vile vile ni faida ngapi tungepata kama tukirudi kwenye *COMESA.* Biashara zitapanuka na tutaweza kuendelea na wenzetu na tukajilinganisha. Sasa hivi nchi yetu ni maskini. Ukiangalia kwenye orodha ni maskini sana duniani. Mheshimiwa Spika, naomba unilinde tena uniongezee dakika naingiliwa na Wabunge wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi namalizia kwa kusema kwamba kwa sababu *customs* zetu ni moja. Naamini kwamba *COMESA* inaweza ikatusaidia tukijiunga na naamini kwamba tutaweza kukuza ushirikiano huu ambao tunao sasa hivi wa Afrika ya Mashariki. Basi hakuna sababu ya kusita ningeomba wakubwa wakae mko hapa hapa muangalie namna ya kurudi kwenye *COMESA* hatutapata hasara. Tutafaidika kwa kurudi kwenye *COMESA* badala ya kupata hasara na tutaweza kusaidiana mambo mengi kibiashara na masoko .

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hatuko kwenye soko hilo tuna vitu vingi tunakosa. Ni katika hao hao majirani zetu ambao tuliwatembelea walitushauri vizuri. Nilikuwa na Waziri wa Kilimo kule Misri amenishauri sana kwamba ninaporudi Tanzania niwaambie wenzetu kwamba wasiwe nje na *COMESA.* Vile vile tuwe na masoko yetuwenyewe kwa kuwa sasa hivi soko la dunia linatuchezea katika bidhaa katika bei za vitu.

Kwa hiyo, tuwe na ushirikiano wa Afrika nzima tusijitoe *SADC* wala *COMESA.* Tuangalie tuwe nao tutajua faida tutapata namna gani au ni lazima tutapata faida tena sio hasara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi napendekeza vile vile kwamba basi wakulima wadogo wadogo wapatiwe mikopo ya kununulia hizo pembejeo na wapate msaada wa mbolea ili wapate kipato na kuongeza pato la Taifa. Hilo ni pendekezo.

Vile vile hao watu wa leseni msiseme wasilipe leseni, walipe leseni lakini muwape mikopo ya unafuu yaani asilimia ziteremke. Nchi zingine wanasema Benki ya Wakulima wanatoza asilimia 7 tu hapa hatuna cha mkulima, hatuna anayenunua Basi wala mwenye biashara kubwa, wote wanakopa kwenye Benki moja. Nashukuru mmesema mna mpango wa kuweka Benki ya Wakulima ningeomba hili likamilike haraka sana.

Kwa kweli ningesema kwamba hiyo Benki basi ianzishwe na hizo fedha za dhahabu, *TANZANITE* zijazwe humo ndani ili wakulima waweze kupata asilimia ndogo ya fidia na kwamba iwe ni Benki ya Kimaskini. Mngerudisha ile *NMB* basi ikawa ndiyo hiyo. Si majumba yako kila mahali, majengo hayo ya Mabenki yako kila mahaliyatumike hayo .

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. FRANK G. MAGHOBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia kidogo hoja hizi mbili zilizo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, lakini kabla sijachangia ningeomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kigamboni kuwapa pole Mheshimiwa Abdallah Kigoda na dada yake Mheshimiwa Aisha Kigoda, kwa msiba uliowapata.

Pia niwape pole Wabunge ambao walipata matatizo wakiwa safarini kuja Dodoma. Mheshimiwa Makongoro, Mheshimiwa Kilasi kwa kupata ajali na pia nimpe pole Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, kwa kuvamiwa na majambazi. Naomba Mungu aongeze nguvu ili wapone haraka waweze kusaidia kuchangia kwenye Bajeti hizi mbili.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji kwa kuandaa Bajeti yao vizuri yenye mwelekeo wa uchumi ambao tunadhani sasa hivi tunakwenda mbele. *(Makofi)*

Pia nachukua nafasi hii kuwapongeza Maafisa na Makatibu Wakuu wa Wizara hizo mbili kwa maandalizi hayo na kuwawezesha Mawaziri wawili kuwasilisha Bajeti yao vizuri mbele yetu hapa.

Mheshimiwa Spika, kazi ya kuandaa Bajeti ni kazi kubwa sio kazi ya mchezo na ni kazi inaelekea kuwa na mtazamo mpana. Tukizingatia kwamba nchi yetu ni kubwa na huko nyuma tulikokuwa tuko katika kipindi cha Ujamaa na Kujitegemea. Toka kipindi hicho kimepita kumekuwa na mabadiliko angalau kidogo ya mwelekeo wa uchumi wetu.

Kwa hiyo, tunaposema au kuchangia katika hoja hizi tuangalie na hayo badala ya kuangalia upande mmoja.

Mheshimiwa Spika, mimi nitachangia kidogo sana katika hoja hizo mbili hasa maeneo machache machache. Nakumbuka mwaka jana Waziri wa Fedha Mheshimiwa Basil Mramba, alitamka kwamba Serikali imeondoa kero zote zilizokuwa zinawakera wananchi wetu zile ndogo ndogo hasa kwenye upande wa majengo. Lakini sasa sijajua vizuri au labda nilielewa vibaya kule kwangu kumekuwa na tatizo kidogo. Suala la kodi ya majengo *(Property Tax).* Nakumbuka mwaka jana Waziri alisema kwamba ataondoa *Property Tax,* kwa majengo ambayo hayajapimwa na kwamba hawatabughudhiwa wale watu kwa sababu ni watu ambao walikuwa wanafanyiwa maandalizi kwa ajili ya kupimiwa maeneo yao.

Lakini mpaka sasa hivi ninavyozungumza kuna wananchi wangu wengi katika eneo langu wamepewa notisi ya kupelekwa Mahakamani kwa ajili ya kutokulipa *Propety Tax* katika maeneo yao. Sasa nilikuwa naomba Serikali itoe ufafanuzi ni kero zipi zilizotolewa katika hiyo. Ni watu gani watatakiwa kulipa na watu gani ambao hawatakiwi kulipa hizo *Property Tax.* Kwa sababu sasa imekuwa ni usumbufu naulizwa maswali mengi ambayo nashindwa kuyajibu. Nimeona niseme hivi kwa sababu Waziri huyo aliyetamka kipindi kile labda nimwulize kipindi hiki aseme na afafanue ni watu gani kama nilivyosema walipe na watu gani ambao hawatakiwi kulipa kodi hiyo ili kuondokana na usumbufu huo.

Nachukua nafasi hii pia kuipongeza Serikali kwa kufanya mipango thabiti kabisa ya kuhakikisha kwamba daraja la Kigamboni linajengwa mwaka huu, kuanzia mwezi Septemba, 2004. Mipango hiyo nimeiona nilikuwa naifuatilia kwa karibu sana nahakikisha kabisa kwamba kuanzia mwezi Septemba, 2004 daraja la Kigamboni linajengwa. Ndiyo maana wananchi wengi wa Mkoa wa Dar es Salaam wameweza kununua viwanja vingi katika mpango wa viwanja 20,000 vya mpango wa Serikali. Kwa sababu wanajua wazi kwamba daraja hilo linajengwa hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, naamini kabisa kuwa daraja la Kigamboni likijengwa kutakuwa na uchumi wa hali ya juu sana kuzingatia na maeneo kwamba ni maeneo karibu na bahari na ambayo sasa hivi watu wengi, haata watalii wanakimbilia Kigamboni kufanya mapumziko yao katika siku za *week-end.* Kwa hiyo, naamini daraja likijengwa litapunguza matatizo mengi na wananchi wengi watavutiwa na eneo hayo. Naamini pia Serikali itasimamia vizuri katika ujenzi wa nyumba na nyumba hizo hazitajengwa za kienyeji kwa sababu tunaamini kwamba lile jimbo la Kigamboni litakuwa ni jiji jipya katika Mkoa wa Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye sekta ya madini. Wenzangu wamezungumza kwa kirefu lakini nasema ni vizuri sekta ya madini iangaliwe upya, mipango yake na mikataba yake waiangalie. Kwa sababu naamini kwamba madini ni kitu muhimu katika uchumi wa nchi yetu. Tukiyachezea kwa kipindi hiki ambacho tumeyaona madini yapo mwishoni madini yatakwisha hayatakuwa tena madini sasa sijui tutakwenda wapi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ningeshauri kwamba kipindi hiki ambacho kuna madini yanagundulika katika kila pembe ya Tanzania, wajaribu kuangalia mikataba yetu ili Tanzania kama nchi ifaidike na madini hayo badala ya kuwatajirisha watu wengine. Ni jambo la msingi na jambo la muhimu kwa sababu uchumi wetu lazima utegemee madini kwa sababu Mungu ametujalia kupata raslimali hiyo. Kwa hiyo, tunaiomba mikataba ambayo inaingizwa au inasainiwa kwa ajili ya kuwapa watu kuchimba madini waangalie upya mikataba hiyo kama inatusaidia au haitusaidii.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali iangalie wale ambao wanakaa maeneo ya madini wanafaidika na madini hayo ambayo yanachimbwa maeneo yao. Kwa hiyo, Serikali iangalie hilo ili wananchi wao wafaidike aidha kwa kujengewa shule au kujengewa barabara na mahospitali kuliko kuachwa katika hali hiyo mbaya kuachwa mahame ya mashimo makubwa makubwa ambayo yamechimbwa madini mbalimbali.

Hivi karibuni nimesoma gazeti kwamba Kigoma kuna madini yamegundulika ni madini ambayo ni muhimu sana katika uchumi wetu hasa kwa kutengenezea simu za mikononi na mambo kadhaa. Sasa kama kweli Mungu ametujalia kiasi hicho ni nini kinatushinda kuinua uchumi wetu kwenda kwenye asilimia 8 tuliyoikusudia. Barabara ya Kigoma itengenezwe haraka sana ili wananchi wafaidike na kutunza madini hayo kwa muda wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikiingia kwenye suala la elimu. Nampongeza Waziri wa Elimu na Utamaduni, kwamba kwa kweli kipindi cha Bajeti ya mwaka jana amejitahidi kuhakikisha kwamba shule zinajengwa. Nampongeza sana kwa sababu amesimamia vizuri mradi huo wa MMEM na maeneo mengine kwamba shule zinajengwa ili watoto wetu ambao walikuwa wanapata taabu ya kwenda shule sasa hakuna msongamano katika mashule. Hususan katika jimbo langu shule nyingi zimejengwa mpya na zile mbovu zimekarabatiwa upya kwa kushirikiana na mradi wa *TASAF.*

Mimi naamini kwamba kwa hali hiyo kama tukienda vizuri tutafikia sehemu kwamba shule zitakuwa zinatosheleza na watoto wetu watakuwa hawapati taabu tena ya kuingia darasa la kwanza mpaka Sekondari. Namwomba tu Mheshimiwa Waziri wa Elimu aongeze bidii ili hata Shule za Sekondari zipate nafasi za kujengwa ili watoto wanapotoka darasa la saba wapate nafasi ya kuingia Sekondari. Kwa sababu kujenga tu Shule za Msingi haitoshi ni lazima pia tuweke na Shule za Sekondari ili watoto wakitoka hapo waingie Sekondari.

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye mradi wa viwanja 20,000. Nampongeza Waziri wa Ardhi na Makazi kwa juhudi kubwa anayofanya na jinsi ambavyo amesimamia mradi huo ambao kwa kiasi kikubwa hakuna malalamiko kama pale awali. Mradi huo umekuwa mzuri na sasa wananchi wanaufurahia. Kwa sababu sasa hivi wanapata hati zao kwa muda mfupi mno. Nampongeza sana kwa sababu hiyo ilikuwa ni kero kubwa kwa wananchi. Lakini sasa hivi ukipata kiwanja chako baada ya wiki mbili au tatu unapata hati yako ambayo haina matatizo. Tofauti na siku za nyuma ambazo watu walikuwa wanasota mpaka miaka mitatu au sita hawajapata Hati. Leo hii lazima tuwe

wazi kwamba baadhi ya Mawaziri wanafanya kazi yao vizuri na lazima tuwapongeze hadharani sio huko uchochoroni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye upande wa Wizara ya Ujenzi nawashukuru. Nampongeza sana Waziri Magufuli kwa juhudi anazoziendeleza na kusimamia vizuri miradi ya kusimamia barabara ambazo tunaamini kwamba barabara ni kiungo muhimu katika uchumi wa nchi yetu. Ni sawa sawa na mishipa ya binadamu mwilini. Kwa sababu damu kama haitakuwa na mishipa ya kupeleka sehemu nyingine basi maeneo mengine yatakuwa mawasiliano hakuna la kufanya ile mishipa au damu ipite sehemu nyingine.

Kwa hiyo, tunaamini barabara zikitengenezwa kama Mheshimiwa Magufuli akisimamia vizuri tunaamini kabisa kwamba nchi yetu itaboreka kwa uchumi na uchumi wetu utapanda kwa haraka sana kwa sababu wakulima na wananchi mbalimbali wanaweza kutembeleana kwa uharaka zaidi kuliko ambavyo ilivyokuwa siku za nyuma.

Mheshimiwa Spika, namsisitizia tu Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi kwamba akumbuke barabara ya kutoka Uhasibu kwenda Kongowe ambayo inapita katika jimbo langu kwenda Mbagala. Barabara hiyo wananchi wanaisubiri kwa hamu kubwa sana kwa sababu waliahidi kwamba kuanzia mwezi Julai barabara hii ingeanza kujengwa. Sasa sina uhakika sana lakini naamini kwamba nitapata majibu hapa katika kipindi hiki cha Bunge la Bajeti.

Hiyo barabara ni kiungo muhimu kwa sababu barabara hiyo inaunganisha na barabara ambayo inakwenda kwenye daraja la Mheshimiwa Mkapa ambayo inaunganisha mpaka Kusini. Kwa hiyo, naamini kwamba barabara ikitengenezwa kwa upana wa barabara mbili kwenda na kurudi itapunguza msongamano mkubwa ambao sasa wananchi wa Kigamboni wamekuwa wengi maeneo yale na wamehamia hivi karibuni kwa sababu Serikali ina mpango wa kutengeneza barabara na hatimaye wananchi watajenga nyumba zao kutokana na mradi wa viwanja 20,000 ambavyo viko kwenye mradi wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunisikiliza naunga mkono Bajeti. *(Makofi)*

**MHE. YETE S. MWALYEGO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kunipa nafasi ili niweze kujadili Bajeti ya mwaka huu.

Kwanza kabisa natoa pole kwa Mheshimiwa Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Aisha Kigoda, kwa kupotelewa na baba yao mzazi. Vile vile natoa pole kwa Mheshimiwa Kilasi, Mheshimiwa Makongoro na Mheshimiwa Anne Killango Malecela, kwa kupata ajali za magari na vile vile kuporwa na majambazi.

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Danhi Beatus Makanga kwa kurudi Bungeni, tena kwa kishindo baada ya kufanya vitu vyake kule Bariadi. Kwanza alimwangusha Mwenyekiti wa *UDP,* Bwana Mapesa, John M. Cheyo. Pili,

kumwangusha mgombea Urais wa mwaka 1995 na 2000 kupitia Chama cha *UDP.* Tuna imani kwamba hatagombea tena Urais ila Udiwani. Tatu, kurudi Bungeni kwa tiketi ya Chama Tawala - CCM Daima. *(Makofi)*

Pia tunatoa pongezi kwa Bajeti nzuri ambayo Waheshimiwa Mawaziri, Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mramba na Dr. Abdallah Kigoda kwa kuiwakilisha hapa kwetu. Hii Bajeti nzuri. Kuna wengine wanasema eti ni Bajeti ya uchaguzi kwani kuna ubaya gani ikiwa ya uchaguzi. Hata wewe ungefanya hivyo. Kitu kingine napongeza kwa wastaafu wale waliolipwa kwa mkupuo kurudishwa tena kwa kulipwa na Serikali. Pia ningependa kutoa hoja kwamba Wizara hii iangalie upya muda wa wastaafu hao kulipwa badala ya miezi sita angalau kuwe miezi mitatu. Wanalalamika sana kwamba muda ni mrefu mno wanakopa sana na mwisho wanaishia kulipa madeni. Kwa hiyo labda wangepunguziwa muda wangeweza kujikimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kidogo kuhusu ubinafsishaji wa Mashirika nyeti ya *TRC, THA* na *TANESCO.* Sidhani kama wakati huu ni muafaka, Serikali iangalie upya suala hili na kusubiri kwa sababu tumeona mifano mingi. Bush na Blair wamezidisha utekelezaji wa *foreign policy* kiasi kwamba sasa imekuwa ni matatizo kisiasa na sisi tumeishabinafsisha Mashirika mengi, haya tuyasubiri yasije yakatuletea matatizo kisiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Madini inalalamikiwa sana na labda kwa sababu ni mwanzo tungoje hayo marekebisho. Lakini nadhani ni vizuri tukajua kwamba madini ni mali ya Tanzania. Kwa hiyo, unaposema unayo dhahabu Bulyanhulu sema kwamba: "Kila asilimia 25 utakayozalisha ni ya kwangu na wewe asilimia 75 itumike kufidia gharama zako, baada ya hapo basi tutagawana nusu kwa nusu ukimaliza kuondoa gharama zako." *Otherwise,* Serikali inaingia hasara kubwa sana na ina maana hatupati faida yoyote afadhali ingebaki pale pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *VAT* ya asilimia 20 ni kubwa mno. Mara ya mwisho niliomba mfanye mchanganuo ili kuangalia uwezekano wa kuipunguza. Hapa mmesema kwamba mkishusha kwa asilimia 2 Serikali itapoteza bilioni 59. Binafsi sidhani kama hizi ni kupoteza, ina maana hizi fedha zinabaki kwa mlaji, ina maana hizi fedha ana-*reinvest* yule mlaji, ina maana hizi fedha kunapatikana ajira zaidi, ina maana hizi fedha unalipa kodi nyingine zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba tena kwamba waachiwe walaji hizi bilioni 59 na *VAT* iwe asilimia 18 na utakuta kwamba tutapata fedha nyingi zaidi kwa sababu ya *multiplier effect.* Hivyo, tutasaidia kuondoa umaskini. Vile vile, hii *VAT* ikiwa chini inaleta *compliance,* watu watalipa zaidi na kuongeza mitaji yao. Kwa hiyo, naomba sana Serikali ikubali kushusha *VAT* kuwa asilimia 18. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu mapato ya kodi ya mafuta, ninawapongeza *TRA* kwamba wameongeza kukusanya mapato haya na wameongeza kwa asilimia 25 na tunadhani tukiwa na *flow meters* asilimia 25 nyingine ambazo zimebaki zitaongezwa.

Serikali wawe waangalifu kwa utumiaji huu wa mita kwamba wawajulishe makampuni waongee nao na kuwaeleza kama wana maoni yoyote watoe, lakini wasishtukizwe ikaonekana ni kitu kipya.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la hili la hii *Central Tender Board* na *Procurement Act* ya 2002 inayotumika sasa. Nadhani ni vizuri tukawa na *Tender Regulatory Board* badala na kuwa na *Central Tender Board* na hizi tenda zishughulikiwe kwenye Wizara na ku-*award* kwenye Wizara. Hii *Central Tender Board* iwe ndiyo *Tender Regulatory Board,* kama kuna malalamishi basi waende *Tender Regulatory Board* au chombo kingine chochote kile *(Regulatory Authority)* ambayo haipo, ndiyo ishughulikie malalamisho yoyote yale.

Lakini sasa hivi kwamba kila kitu kiende *Central Tender Board,* inapoteza muda mwingi sana na watu wanalalamika kwamba kuna upendeleo na vile vile kuna hujuma, kuna rushwa na kadhalika. Sasa ni vizuri Wizara ikaliangalia upya hili na kupendekeza kitu kizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, *Procurement Act* imelalamikiwa sana na ni vizuri Wizara ikarekebisha na hasa kutoa upendeleo wa wazi kabisa kwa wazalendo kwa sababu tenda nyingi wanapewa watu wa nje. *Procurement Act* haisemi umpe nani, kwa hiyo watu wanatumia hiyo *loophole* kwamba wanatoa tenda za *consultancy, tenda* za *construction* na kadhalika kwa watu wa nje. Fedha nyingi zinatoka kwenda nje ya nchi. Kwa hiyo, kuondoa umaskini hapa nchini itakuwa vigumu sana kwa sababu tenda mnawapa watu wa nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wale watu wa nje hizo fedha wanakwenda kujisaidia huko kwao, lakini tungewapa *contractors* wa hapa na *consultants* wa hapa kama anajenga, kama anafanya nini ni hapa Tanzania, lakini siyo wale watu wa nje fedha zote wanatoa. Kwa mfano, *contractors* wa nje ni asilimia 3 tu, lakini wanachukua zaidi ya asilimia 90 ya *value* ya fedha za hapa. Sasa sijui kama tunaweza kuondoa umaskini kwa Bajeti hii kama haturekebishi hii sheria ya *Procurement Act.* Afrika Kusini wanaita *empowerment* na iko wazi kwenye *Procurement Act* yao. Botswana wanaita *Citizen Contractor* au *Citizen Consultant* kwamba kuwe na upendeleo maalum wa kumpa Mtanzania kazi hizi, *otherwise* kwa kweli tunapoteza muda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Kilimo kwa upande wa ile Mikoa minne ya Nyanda za Juu Kusini tunashukuru tulipata mbolea ya ruzuku, lakini ilichelewa kufika. Vile vile, mpango mzima ulikuwa haueleweki kwa sababu kulikuwa na mbolea ya ruzuku na mbolea isiyo ya ruzuku. Sasa huwezi kujua mbolea ya ruzuku ni ipi na isiyokuwa ya ruzuku ni ipi. Kwa hiyo, kulitokea mwanya kwamba iliuzwa kwa muda mfupi tu halafu ikapanda bei tena kuwa mbaya zaidi. Hatujui kwa mwaka huu, kwa sababu ule ulikuwa ni mwaka wa mwanzo. Mwaka huu mpango uwe mzuri zaidi, mbolea iende mapema zaidi na ni vizuri ukawa ni mfumo mmoja tu, siyo hii kwamba mimi ni ya kwangu siyo ya ruzuku. Kwa hiyo, inakuwa siyo rahisi kudhibiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mbeya masuala ya elimu, masuala ya afya, masuala ya kilimo, masuala ya barabara yamefanikiwa vizuri sana, lakini masuala ya maji kwa kweli hii miradi kwa upande wa Mbeya haijafanikiwa. Ninapendekeza kwamba tuwe na Mfuko wa Maji kama tulivyo na Mfuko wa Barabara na kama tulivyo na Mfuko wa Elimu, ili kusaidia hii miradi ya maji. Bila hivyo kwa kweli unapopeleka milioni 12 Idara ya Maji kwa mwezi, hizo ni *imprests* tu zitakwisha, haziwezi kusaidia maji. Nadhani tukiwa na Mfuko wa Maji, vile vile miradi ile mikubwa ya maji ijaribu kusaidiwa.

Mheshimiwa Spika, la mwisho na la muhimu zaidi ni ujenzi wa uwanja wa ndege Songwe. Tunaishukuru sana Serikali kwa kutenga fedha za kutosha. Mwaka huu tumetenga fedha Shilingi bilioni 1, lakini tumesaini mikataba ya ujenzi wa kiwanja hicho Shilingi bilioni 7 na zaidi. Kuna mapungufu makubwa sana, tunaomba Waziri wa Fedha atusaidie kutafuta fedha hizo ambazo tusipokuwa nazo ni kwamba tutashtakiwa kama Serikali na vile vile tukishtakiwa tutalipa fedha nyingi zaidi Serikali hiyo hiyo tena. Kwa hiyo, ni vizuri ukatafuta chanzo kingine cha fedha na kufanya *Supplementary Budget* ili tuweze kupata hizo fedha. Tunaomba sana Waziri aweze kutusaidia hilo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja zote mbili kwa asilimia mia moja. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. HASSY H. B. KITINE:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika hoja hizi mbili za Waheshimiwa Mawaziri wa Fedha na Mipango. Lakini kabla sijaanza kuchangia ningependa kukumbusha tu kidogo kwamba wakati wa Bajeti ya mwaka juzi, siyo ya mwaka jana, mwaka jana sikuwepo.

Mheshimiwa Spika, unafahamu sana sikuwepo wakati wa Bajeti ya mwaka jana, 2003. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, wakati wa Bajeti ya mwaka juzi 2002 nilitoa mchango wangu hapa halafu ukaniandikia ki-*note* kidogo inawezekana umesahau, ukaniambia: “Waheshimiwa Wabunge wamesikia semina uliyotoa na sasa wanataka ile *allowance* ya bahasha ambazo huwa wanapata mara kwa mara.” *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naomba nikuthibitishie kwamba mchango wangu wa leo hauwezi kuwa wa kiuchumi kwa kiasi hicho kwa sababu kwanza sina hela, maana unaweza kunikumbusha tena. Halafu pili, pengine wenzangu wamekwishatoa mawazo mengi sana juu ya shughuli za uchumi yanayotokana na Bajeti yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwanza kwa niaba ya Wananchi wa Makete, ninaomba nikushukuru sana na niishukuru Serikali na kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote wawili kwa kutoa bajeti safi na mipango safi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niseme moja kwa moja kwa sababu huwa ninakuwa na matatizo. Ualimu una matatizo yake, ninaweza nikasahau kuunga mkono huko mbele

ya safari halafu nikaonekana kama mpinzani mpinzani hivi kidogo. Kwa hiyo, nataka kusema kwamba ninaunga mkono hoja hotuba zote mbili za Waheshimiwa Mawaziri. *(Makofi)*

Pili, naomba niungane na wenzangu kutoa pole kwa Waheshimiwa Dr. Kigoda na Dr. Kigoda mdogo kwa kufiwa na mzee wetu, mzee Omary Kigoda. Bahati nzuri mimi nilimfahamu sana kwa sababu niliwahi kufanya kazi Mkoa wa Tanga kwa muda wa miaka miwili. Ni mzee wangu mimi kama alivyokuwa kwa akina Dr. Kigoda wawili. Inaonyesha mzee alivyofanya kazi, kaacha madaktari wawili katika familia na wengine nadhani wanaelekea kwenye udaktari. Kwa hiyo, naomba kutoa pole sana kwa Waheshimiwa hawa wawili. *(Makofi)*

Vile vile, naomba nitoe pole kwa Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, Mheshimiwa Kilasi na Mheshimiwa Hoogan Singh kwa kufiwa na binti yake. Naomba nitoe pole za dhati. Kwa hao Waheshimiwa wengine naomba nitoe pole kwa kupata ajali kama walivyopata.

Mheshimiwa Spika, tatu, naomba nitoe pongezi, kama nilivyosema kwa Mawaziri wote wawili kwa hotuba zao nzuri na vile vile nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Getrude Mongella, Mheshimiwa Ntagazwa na Mheshimiwa Danhi Makanga. Wote *respectively* wa kwanza kwa kuwa Rais wa Bunge la Afrika. Wa pili, kwa kuwa Rais wa *Council* ya Mawaziri wa Mazingira Duniani na tatu kwa Mheshimiwa Makanga kuwa Mbunge kwa kupitia Chama sahihi na chenye uwezo wa kuongoza nchi. Ninampongeza sana Mheshimiwa Makanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nne, ninaomba tena kwa niaba ya Wananchi wa Makete na kwa kweli kwa niaba ya nchi. Pengine kama ninaweza kuwa ninakosea *protocol* sijui, ninaomba Mwenyezi Mungu amsaidie na kumjaalia Mheshimiwa Rais apate matibabu, aweze kupata nafuu na arudi kuja kufanya kazi ya kuongoza harakati za nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu ni mfupi kama nilivyosema. Kwanza, kuna matatizo ambayo yamezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi. Kama tunafuatilia, baadhi yetu tunafuatilia mambo karibu karibu kwamba, mambo yanayozungumzwa na Waheshimiwa Wabunge kwa kweli ni *reflection* ya matatizo au kero ambazo Wananchi wanazipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kero zenyewe wenzangu wamezisema, narudia tu, lakini si vibaya kuweka *emphasis.* Kwanza ni kilimo. Kuhusu kilimo kweli kumetokea mazungumzo. Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia na hii mimi ninajua ni msaada mkubwa kwa Mheshimiwa Keenja kwamba anakoendelea huko mbele ya safari yeye atakuwa siyo askari wa mwavuli tu, bali atakuwa vile vile askari wa matenki na mabuldoza katika kujaribu kusukuma kilimo cha nchi hii kwa sababu kumetokea *concern* kubwa sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge wameongea, inaongelewa vile vile kwenye mihadhara mbalimbali na hiki ni kitu ambacho pengine Serikali ingejaribu kutafuta *specific strategies* za kuweza kuhakikisha kilimo cha nchi yetu kinakwenda vizuri.

Kuna maandishi mengi sana juu ya kilimo na kama vile ilivyo juu ya *sectors* nyingine, lakini *action* kweli haziko kama vile yanavyokuwa maandishi. Kwa hiyo, naomba kwa niaba ya Wananchi wa Makete na kwa kweli kwa nchi nzima kwa sababu kilimo kimelalamikiwa na Waheshimiwa wengi na nchi kwa jumla.

Mheshimiwa Spika, kero ya pili na ambalo ni tatizo linazungumziwa na Wananchi pamoja na Wabunge wameongea ni madini. Habari ya madini ni lazima tu-*revise.* Ni lazima tu-*revise* sera na utaratibu mzima ambao tumeingia kama nchi ambayo imeanza kuchimba madini. Ndani ya miaka mitano inaelekea mapatano na mikataba tuliyofanya kama nchi na haya makampuni kwa kweli siyo mizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu mimi nilikuwa *Local Director* wa makampuni ya *Anglo Gold.* Nilikuwa *Local Director* wa hii *Geita Gold,* sasa wamenihamisha wamenipeleka kwenye *exploration* na kwa sababu ya kuchangia changia tu, hamna lolote. Wanafikiri kama naweza kuchangia changia, nina uwezo wa kuwachangia na kuwaeleza. Nawaambia: *"Fine, if you can do it."*

Lakini nawaambia kwamba: "Hii mikataba ninyi mmetulalia sana." Wengine wanacheka, wengine wanasema hivi. *But in fact this is a fact and you have to do something about it. Its seriously the Government must do something about this. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *there is no way* kama kero inazungumzwa, inazungumzwa, inazungumwa, halafu *no action is taken. At least* kuwe na *symbolism of action on the part of the Government.* Nadhani hiyo ni kero ya pili ambayo Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kero ya tatu ambayo pengine *somehow* ninakuwa *scared* kuizungumza na mnajua ni ipi hiyo ni *gap* na hii imetokana na hali ya siasa yetu. *Political direction* ya nchi yetu imekuwa *such that visibly* kwa sababu ya siasa yenyewe kwa kuwa sasa hivi tunafuata siasa ya kibepari. *Really attributes* za uongozi wa uchumi wa kibepari ndizo zinazofuatwa.

Kwa hiyo, matokeo yake kuna nafasi kubwa sana hapa wenyewe wanaita *gap.* Kuna *gap* kubwa sana la *the so called high income or middle income* na Wananchi wa kawaida ambao tunawaongoza. *There is a serious gap between us* na wale wananchi wa kawaida. *Fine,* akina Mengi wanaweza kuwa na hela nyingi, akina nani na wengine wengi, *those are in business,* kazi yao ni ku-*make money*. Lakini kama mimi Kitine ninakuwa na mamilioni ya dola, *I have to explain* na siwezi kueleza *in fact.* Siwezi kueleza *if I have a couple of million dollars.* Siwezi kueleza! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hii kitu kuna wengine wamesema hapa, pengine siyo rahisi kuanza kutaja majina, *it's not my job; my job is* kuwa Mbunge wa Makete kwa sasa

hivi. Kwa hiyo, hiyo ni kero nyingine kubwa. *Of course* hii ya *gap* ndiyo inaungana na hiyo ya rushwa ambayo sina haja ya kuisema zaidi kwa sababu *I could have burn my fingers again. (Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninajua inawezekana ninawa-*disturb* baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, lakini hii ndiyo hali yenyewe ya mambo yalivyo. *Actually* nasema pengine inawezekana mimi siyo mwanasiasa kwa sababu ninaona ninapata matatizo. Ukitaka kusema ukweli kama unavyoona unapata matatizo makubwa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kero ya nne ni uwezeshaji wa Wananchi ili waweze kushiriki kikamilifu katika uchumi wa nchi yao. Kero ya tano naona niiache. Hizo kero nne zinatosha. *(Kicheko)*

Sisemi Serikali hai-*address* hizi kero, ina-*address.* Lakini *efforts* ambazo zinatumika pengine hazi-*match* na *intensity* na uzito wa matatizo yenyewe. Kwa sababu kama Serikali ina-*address problems,* za wananchi, wananchi wanajua na viongozi wanaona.

Kwa mfano, tatizo la elimu Serikali inali-*address squarely* na kila mtu anasema humu ndani kwamba *the Government is doing the best* kuhakikisha inapanua elimu. Pia barabara, *everybody talks about it.* Kwa hiyo, kama Serikali inaamua na uwezo Serikali ndiyo inao, kama Serikali inaamua kutatua matatizo haya yatatatulika yote *including* la rushwa, yatatatulika *seriously* kabisa kabisa.

Mheshimiwa Spika, watu wanaita *strong political will and therefore to take strategies necessary to solve the problems and implement those strategies* ili kusudi matatizo haya yatatulike, hatuwezi kuendelea kulalamika. Tunalalamika, tunalalamika, tunalalamika! Najua hata Waheshimiwa Mawaziri wanalalamika kwamba kwa kweli inawezekana kweli kuna rushwa, lakini sasa hali yenyewe ni ngumu kidogo kuweza kuitatua. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, inawezekana nika-*save some minutes.* Ninaomba kuishukuru sana Serikali kwa Bajeti nzuri na mipango mizuri *specifically* uondoaji wa ununuzi wa *license* kwa wafanyabiashara wadogo wadogo na hii *in effect* ni kujaribu kutekeleza tatizo moja la kupunguza *gap* ya sisi na Wananchi. *Actually* sisi wote *if I may say* hatuishi maisha ya kitanzania, tunaishi maisha ya Ulaya huko.

Mheshimiwa Spika, mimi nilivyovaa hivi unafikiri kule Makete vijijini nani anaweza kuvaa namna hii? Ingawa wapo, lakini ni wachache sana.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaah!

**MHE. DR. HASSY H. B. KITINE:** Eeeh, hawavai. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba nirudie kuipongeza Serikali kwa *aspect* hii na hasa hususan kwa Wananchi wa Makete kwa sababu wao *they are scattered all over the country.*

Moja ya tatizo la *incidences* kule za UKIMWI ni tatizo kwamba hawa watu wako kila mahali. Utawakula Mtukula, utawakuta kwenye mpaka wa Rwanda na hadi mpaka wa Burundi. Mheshimiwa Waziri wa Fedha anawafahamu sana hawa watu kwa sababu ya *background* ya shughuli zake alizofanya akiwa Mkoa wa Mbeya, wapo kila mahali.

Pia, wapo kwenye mpaka wa Tanga. Mimi niliishi Tanga kwa muda wa mwaka mmoja na nusu, miwili hivi, wako kule mpakani Lungalunga na kila mahali. Sasa hawa wanafanya biashara. Ni nafuu kubwa sana na hii inaweza kunisaidia sana kama Halmashauri Kuu itarudisha jina langu kugombea tena. Itanisaidia sana mimi kupata kura huko mbele ya safari. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, ninaomba niishukuru tena Serikali na kwa bahati nzuri Mheshimiwa Waziri Mkuu aliongeza hapo katika kujibu maswali ya Serikali na leo nimeongea naye pale nje kuishukuru Serikali kwa kazi iliyofanya *specifically* ya kutusaidia wakulima wa pareto wameweza kupata pesa ambazo wametutuliza *politically* na kwa hiyo nadhani Chama chetu kitachukua pamoja na kura za Mheshimiwa Rais atakayekuwa anagombea, atapata kura nyingi Makete, naweza kuthibitisha hilo.

Mheshimiwa Spika, hata kama mimi nitakuwa sipo, lakini yeye tutahakikisha anapata hizo kura nyingi kwa sababu Serikali imefanya kazi kubwa sana juu ya pareto na kwa bahati nzuri hata utawala na uongozi wa shughuli hiyo na kiwanda uko chini ya watu wenye uwezo mkubwa sana wa kuweza kudhibiti. Ni wenye *interest* na ni viongozi katika nchi ambao wanakuwa na *interest* ya Watanzania kwanza. *Again* hii ni uwezeshaji.

Kwa hiyo, uwezeshaji wa watu wa chini na inaonyesha kwamba inajaribu kutekelezwa. *(Makofi)*

*(Hapa Kengele ya Kwanza ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kumalizika)*

**WABUNGE FULANI:** Unga mkono hoja.

**MBUNGE FULANI:** Bado dakika tano.

**MHE. DR. HASSY H. B. KITINE:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja zote mbili. Ahsante sana, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, msemaji wa kwanza kipindi cha mchana atakuwa Mheshimiwa Ibrahim Marwa.

Baada ya kufikia hapo, sasa nasitisha Shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 06.54 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti*

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kuweza kufungua hili pazia jioni ya leo ili na mimi niweze kujiunga na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuchangia hotuba mbili zilizoko mbele yetu, Hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji na Hotuba ya Waziri ya Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba kwa niaba ya wapiga kura wangu wa Jimbo la Musoma Mjini na mimi niungane na Wabunge, wenzangu kumpa pole Mheshimiwa Waziri Dr. Abdallah Kigoda, pamoja na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa msiba mkubwa uliowakuta wa kumpoteza baba yao. Naomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi. Amen.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kwa haraka kabisa nimpongeze sana Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mbunge wa Bariadi kupitia Chama cha Mapinduzi. Uchaguzi wake kwa kweli kwangu binafsi ni faraja kwa sababu umetufundisha kwamba nguvu ya umma haiwezi kuzuiwa na kitu chochote kile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba nianze kuchangia hoja hizi mbili kwa kuanzia na Hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji na ningependa niende moja kwa moja nizungumzie ubinafsishaji wa mashirika yetu ya umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika moja ya mapungufu makubwa sana ambayo sera hii ya ubinafsishaji imeweka dosari, ni suala la mafao mbalimbali kwa wafanyakazi na watumishi waliokuwa kwenye mashirika haya ya umma. Wakati mwingine kuna mambo ili uyazungumze lazima uwe na kichwa kigumu kidogo au uwe kidogo na ukichaa kichaa ili uweze kuyazungumza barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania toka tumepata uhuru tumepitia awamu tatu na tumepitia kwenye mifumo tofauti ya uchumi. Tulikuwa kwenye mfumo wa ujamaa, ambao ulikuwa na uchumi ambao ulikuwa unasimamiwa na Serikali. Tukajenga mashirika ya umma ambayo kwa kiasi kikubwa ndiyo yalitoa ajira kwa watumishi wengi ambao ni Watanzania. Sasa tumekuja kwenye mfumo huu tulionao wa soko huria ambao tunawajibika kutoka ili sekta binafsi iweze kuchukua mkondo wake. Sasa mimi nasema kwamba Watanzania siyo wajinga kwa sababu ni lazima waelimishwe waelewe tofauti ya mfumo wa zamani huo na mfumo wa sasa hivi. Ni vema tukajua haya mashirika

yalijengwa kwa jasho la Watanzania na Watanzania hawa walijitolea wakaacha starehe zao wakaamua kujenga mashirika hayo. Sasa leo tumeanza kuyabinafsisha haya, kuna yale ambayo kwa kweli niseme tumefanikiwa na kuna mengine ambayo kwa kweli bado ni mgogoro.

Mimi nilitaka nizungumzie kwa mfano kuna Shirika la Vifaa vya Elimu *(Tanzania Elimu Supplies)* shirika hili liliundwa mwaka 1967, kati ya Watanzania kwa msaada wa Serikali ya Sweden. Malengo yalikuwa ni kusaidia kuboresha Sekta ya Elimu kwa maana ya upatikanaji wa vifaa vya elimu ambavyo vingekuwa na nafuu zaidi ya ubora wa hali ya juu kuweza kusukuma maendeleo katika sekta ya elimu. Kuna wafanyakazi pale walijitolea kuacha *bonus* zao ili kuwekeza zaidi kwenye lile shirika. Sasa leo shirika hili linabinafsishwa na linabinafsishwa kwa utaratibu wa ile *voluntary liquidation* lakini sisi tunaelezwa na Serikali kwamba shirika hili limefilisika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, si kweli kwamba limefilisika. Madeni yaliyoko *Tanzania Elimu Supplies* na mali zilizoko *Tanzania Elimu Supplies* bado haziwezi kulifanya shirika hili likawa *declared* kwamba limefilisika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hapo baadaye mimi nakusudia kuleta hoja binafsi ili Bunge liweze kuunda tume, ambayo itapitia malalamiko ya wafanyakazi katika mashirika mbalimbali yaliyobinafsishwa na ambayo yanakusudiwa kubinafsishwa ili tuone kwamba haki inatendeka kwa Watanzania hawa ambao wanaondolewa kwenye haya mashirika. Wakati ukifika nitafanya hivyo na nina hakika Waheshimiwa Wabunge, wenzangu wataniunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kusema kitu kimoja kwamba tunapozungumzia bajeti tunazungumzia makusanyo ya Serikali ya mapato na matumizi ya fedha kwenye miradi na maeneo yaliyokusudiwa. Naomba niseme kwamba katika kundi lolote la binadamu huwezi kuwakosa mafisadi na ndiyo maana hata tukiwa kwenye maeneo ya ibada tuwe Misikitini, tuwe Makanisani bado tunaendelea kuaswa kwamba kuna vitu vizuri vya kufanya na kuna vitu vibaya vya kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi ambayo imesifiwa kwamba imefanywa ya kukusanya mapato kupita kiasi, kuvuka malengo, mimi najiuliza hivi hayo ndiyo yalikuwa makisio halisi kabisa ya ukusanyaji wa mapato hayo au tumekosea sehemu hapo katikati? Kwa hiyo, mimi nasema nawashukuru Watanzania wanaofanya kazi kwenye mamlaka yetu ya mapato kwa kazi nzuri wanayofanya, lakini niseme kwamba bado hili kapu la Serikali bado linavuja. Bado linavuja kwa maana ya kwamba bado tunaweza kukusanya kutoka hapa tulipo tukaenda mbele au mara mbili zaidi. Ukienda kwa nchi ya wenzetu kwa mfano Kenya wanakusanya karibu mara mbili ya hiki tunachokusanya Tanzania. Sasa nasema ukiangalia sisi tuna vyanzo vingi na sasa hivi kuanzia miaka miwili iliyopita sekta ya madini imeanza kuingia kuchangia uchumi wa taifa. Sasa sisi tunalalamika kwamba hatuna fedha, kwa nini tulalamike? *(Makofi)*

Niseme kwamba suala la kukusanya mapato peke yake halitoshi na tukatoa sifa kwa wakusanyaji wa mapato. Lakini mimi nasema wamefanya kazi nzuri. Lakini suala la matumizi ya fedha hizi za Serikali ndiyo nadhani lenye tatizo zaidi. Mimi nilitegemea wakati Waziri wa Fedha, akileta hapa hii hotuba yake angetueleza na baadhi ya maeneo ambayo tunajua kabisa yatahitaji *financing* ya Serikali. *(Makofi)*

Kwa mfano leo tuna ujenzi wa jengo la Benki Kuu pale Dar es Salaam zinatumika *billions of money* kujenga jengo lile. Sasa zimekwishatumika zaidi ya bilioni 75 kama sikosei, Wabunge hawajui kinachoendelea pale. Lakini tunasema hii ndiyo *priority* yetu tunazungumzia hatuna fedha za kupeleka kwenye *feeder roads* huko vijijini, tunazungumzia hakuna fedha za kutengenezea hospitali ambazo ni bora zaidi, lakini kuna maeneo bado tuna-*invest* hivi Watanzania tunahitaji Benki Kuu, iwe ina jengo linalolingana na Benki Kuu ya wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nilitegemea kwamba Bunge lingeelezwa kwamba Serikali ilikuwa na mgogoro pale, kwamba kuna kesi ilikuwa pale kati ya mfanyabiashara mmoja na tuelezwe kwamba hizi fedha zinalipwaje kwa huyo mfanyabiashara ambaye ameshinda kesi, lakini haikuelezwa hapa na hiyo fidia na hayo malipo ni *billions of money* ambayo pia inakwenda huko. Sasa tunasema si kitu kizuri Wabunge wasifahamishwe mambo ya msingi ambayo yanafanyika kwa kutumia fedha za walipa kodi wa nchi hii. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi nategemea kwamba Waziri atatueleza vizuri kwamba haya mambo ya Benki Kuu, yanakuwaje, tungependa tupate taarifa ya ujenzi wa jengo la Benki Kuu na tuelezwe je, utaratibu wa *tender* yaani zabuni ulifuatwa katika ku- *award* hiyo, *tender* ya ujenzi wa Benki Kuu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa naomba sana kwamba vyombo vya habari vitusaidie, suala la kuzungumzia rushwa linaonekana kubezwa. Lakini nasikia baadhi ya waandishi wa habari wasio waaminifu pia, wamekuwa wakificha habari kwa kupatiwa kidogo na hawa wala rushwa. Kwa hiyo na wao ningependa niwageuzie kibao kwamba hawa wachache wataharibu sifa ya taaluma hii ya uandishi wa habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu naona kengele ya kwanza imekwisha nipa tahadhari, mimi nilikuwa nashauri kitu kimoja kwa Waziri wa Fedha, kwamba Waziri wa Fedha aitazame Wizara yake, Waziri wa Fedha aitazame mamlaka ya kukusanya mapato Tanzania na ahakikishe kwamba mamlaka ile inakuwa na sura ya kitaifa. Tuwe na mamlaka ambayo ina sura ya kitaifa, tusiwe na mamlaka ambayo ina sura ambayo inaonyesha kwamba kuna kundi fulani ndilo lenye nafasi ya kupewa pale kwenye hayo mamlaka. Maana kama kuna kazi za kufanya mitambiko tutaitana huko nyumbani mwezi wa kumi na mbili halafu tutazungumza kwamba, bwana umekusanya ngapi na mimi ngapi haya tunazungumza. Kwa hiyo, mimi naliomba hilo aliangalie maana hatuwezi kuweka mkate wa Serikali hii kwenye kundi fulani tu tukasema kwamba linakuwa salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jingine ambalo nilitaka kusema ni kwamba umefika wakati kwa Serikali, kuangalia uwezekano wa kupunguza matumizi kwenye sekta ya utawala na uendeshaji.

Ukitazama Bajeti yetu kwa kweli ahaa! Sasa wananchi wakituuliza sisi tutajibu vipi maana kweli fedha zinazokwenda kwa ajili ya kuboresha maisha ya wananchi wetu kule vijijini zipo lakini si za kutosha. Kwa nini tusijibane sasa hivi tukaamua kuwasaidia hawa wananchi wetu kule vijijini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia kabisa kuna watu wanasema kwamba kiwango cha rushwa kimepungua, lakini nimekwenda kutazama kwenye kitabu namba nne tunapeleka Bajeti ya bilioni 27 kuimarisha kitengo kile. Kama rushwa hii imepungua kwa nini hizo fedha zisiende vijijini kufanya kazi nyingine kama hatuna rushwa na hakuna tatizo hilo?

Kitabu hiki ninacho hapa sijui nimekiweka wapi, kitabu cha nne kwenye Bajeti ya Maendeleo, Ofisi ya Rais, *PCB* wametengewa jumla ya shilingi bilioni 27 na *point something* ku- *build up capacity* yao. Sasa tunasema kama tunapinga hoja hiyo dhana nzima kwamba hilo siyo tatizo sasa la msingi *then is not a priority* tupeleke hizi fedha sehemu nyingine tusaidie wananchi wetu. Lakini kama tunasema kwamba bado tuna tatizo hilo basi mimi nadhani sina tatizo la kusema hizi fedha zinafaa ziende *PCB* zikasaidie hao vijana waweze kufanya kazi nzuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ahaa! Nikushukuru sana, isipokuwa kwa kumalizia kabisa, tungedhani Waziri wa Fedha, anapokuja ku- *wind up* kuna maeneo ambayo tuna mahitaji ya fedha na kuna fedha zimekwenda nyingi kwenye sekta ya utawala.

Mimi nina hospitali pale kwangu tumejenga wananchi wa Mara kwa miaka mingi sana miaka karibu 20 wananchi wamechangia pale lakini inaonekana Serikali haijawa tayari kutusaidia. Kwa hiyo, nilikuwa naomba kwa sababu kuna fedha huko ambazo Waziri anaweza akazikatakata ile hospitali yetu tumejenga ni ya ghorofa 7 akinigawia fedha nitaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. EMMANUEL E. KIPOLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina kushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hoja zilizoko mbele yetu. Nianze kwanza kwa kuwapa pole pia Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda kwa kuondokewa na mzazi wao. Vile vile niwape pole Waheshimiwa Wabunge, wengine wote waliopata matatizo katika kipindi cha kuja kuanza mkutano huu. Naomba kuwapa pole sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niwapatie pongezi wote waliopata mafanikio kabla ya kikao hiki wakiongozwa na Mheshimiwa Danhi Makanga, kupata mafanikio makubwa kabisa ya kurudi kwenye Bunge hili tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, juu ya hoja mbili zilizowasilishwa kwetu hapa mimi niseme kwamba kwa kweli kwa niaba ya wananchi wangu wa Msalala ni hoja nzuri, ni

Bajeti nzuri na kwa kweli niseme mwanzoni kwamba naziunga mkono hoja hizi moja kwa moja. Pamoja na kuziunga mkono moja kwa moja kwa sababu ya uzuri wake na niseme tu labda kama mtu anaendelea kusema hotuba hizi na Bajeti hizi na mipango hii ni mibaya basi huyo ana matatizo yake binafsi.

Kuna machache ambayo ningependa kuyasema hapa kuhusiana na hoja zilizoko mbele yetu. Nianze na suala la Benki ya Maendeleo ya Kilimo. Hili mimi linanipa tabu limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi hapa na kwa mtazamo wa mazungumzo hayo inaonekana kwamba pengine huu ni ukombozi wa matatizo yetu ya kilimo katika nchi hii. Kwa mtazamo wangu na unabaki kuwa wangu sioni kama huu ni ufumbuzi. Kwanza nashangaa sera zetu zinakwendaje, tumesema waziwazi katika sera zetu na ndiyo mwelekeo wetu kwamba tunakwenda kwenye uchumi binafsi, Serikali inauza mabenki yake kama ambavyo tumekwisha kuona, mabenki mengi yameuzwa, kuna benki moja tukaililia kwa nguvu sana isiuzwe lakini baadaye tumekubaliane iuzwe kwa kiasi fulani. Leo tunaanzisha benki nyingine ya maendeleo ya wakulima, mimi inanipa shida. Tunauza benki tuanzishe benki zingine hapo ndiyo sielewi. *(Makofi)*

Kwa mujibu wa sera za uchumi wa soko huria tunasema Serikali inajiondoa katika biashara na ninaposikia benki mimi naelewa ni biashara. Sasa mimi nitapenda kujua kwanza hii benki inaanzishwa kwa ajili ya nani? Ni ya wakulima wakubwa, wakulima wadogo au ma-*middle men* katikati hapa ili waweze ku- *draw* kama anavyosema kaka yangu Derefa? Mimi sielewi inaanzishwa kwa ajili ya nani kwa sababu si sera zetu.

Pengine tuangalie kihistoria tulikotoka. Mara nyingi ukienda kwenye chuo cha udereva huwa tunaambiwa mara nyingi ukiendesha gari yako uangalie unakokwenda na uangalie kwa kutumia vifaa vya kuangalia kule unakotoka, hatuambiwi kuangalia pembeni. Madereva hatuambiwi kuangalia pembeni, unaambiwa angalia mbele na uangalie nyuma kama kuna mtu anakufuata, kuna gari linataka ku-*overtake* na uangalie mbele uone kuna nini. Sasa katika hili tukiangalia nyuma kama ndiyo sisi madereva tunaangalia nyuma kule nyuma tulianzisha Benki ya *CRDB* kwa malengo haya. Benki ya Ushirika na Maendeleo Vijijini, ilileta maendeleo gani vijijini? Wala kijijini kwangu hawakupata kuifahamu mpaka leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi imefunguliwa *CRDB* pale Mjini Kahama wale wenzangu mimi tunakotoka kule Msalala wanaogopa hata kuingia na hawaruhusiwi kuingia mle kimsingi kwa mantiki kwamba hata kile kiwango cha kufungua akaunti kwenye benki ile hakiwawezeshi kuingia mle, wao wanabaki kukimbilia kwenye *National Micro Finance Bank.* Sasa tunaangalia huko haikufanya kitu mpaka tukaiuza mwaka 1996. Tuangalie tulikuwa na benki inaitwa *Tanzania Housing Bank,* benki ile sijui kama ilileta nyumba za kutosha kwenye nchi hii na ikafa. Sasa huko tunaangalia nyuma, *records.* Sasa tunaanzisha nyingine ya kilimo sasa tunaangalia mbele, tukiangalia mbele ndiyo sera zetu zinasema kwamba Serikali iwezeshe watu wafanye biashara binafsi, Serikali iwawezeshe, Serikali iandae mazingira siyo Serikali ifanye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wasiwasi wangu katika uanzishwaji wa hii benki ni huu hapa ufuatao: Kwanza kutakuwa na gharama kubwa sana za kuanzisha benki hii. Benki mpya ni gharama kuianzisha, utahitaji majengo, utahitaji watalaam, utahitaji mambo chungu nzima. Katika hili wasiwasi wangu mwingine mkubwa benki hii lazima Makao Makuu yake yatakuwa Dar es Salaam. Baada ya benki hii kufunguliwa Dar es Salaam, kitachofuata ni kununua yale ambayo kwa mujibu wa Mheshimiwa Dr. Wanyancha, mashangingi ya ma-*DG, MD* ambayo wale wakulima kama ni wale wadogo wadogo ambao ninawazungumzia mimi kule Msalala ni mzigo, ni mzigo kuna wakulima wadogo wadogo tu hatuna wakulima wakubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uelewe tu kwamba wale wakulima wakubwa tulionao kwa sasa hapa nchini milango ya mabenki yote makubwa yaliyopo ipo wazi, wanakwenda kukopa wanavyotaka. Lakini tunayemzungumzia hapa mimi nafikiri ni yule mkulima wa kwangu kule Msalala ambaye juzi tumehangaika hapa, tumeambiwa akopeshwe trekta anafika kwenye sehemu ya kukopeshwa trekta anaambiwa lete hati ya nyumba, hana, hati ya ardhi hana. Lakini wale wakulima wakubwa wakubwa wana hati za nyumba, wana hati za ardhi zao wameshapima maeneo, wanakwenda kwenye mabenki kama Benki za *CRDB* kama Benki za *ABSA* na benki zingine kubwa kubwa, wana uwezo. Sasa hawa tunaowazungumzia ni hawa wadogo wadogo ambao wasiwasi wangu mwingine wa tatu ni kwamba hiyo *net working* ya hiyo benki mpya tunayokwenda kuanzisha sasa hivi ya maendeleo ya kilimo itasambaa mpaka lini mpaka kufika kwa rafiki yangu kule Sikonge? Tunaisambaza sambazaje? Kama kuna benki zina miaka 15 hazijaweza kufika hata kwenye baadhi ya Wilaya, leo hii tunafanya miujuzi gani wa kuipeleka ghafla ghafla ili iweze kutuokoa na hili janga la kilimo kibovu kwenye hii nchi, tunaipelekaje? *I don't see.*

Mheshimiwa Naibu Spika, wasiwasi wangu mwingine kwenye hili ni *manpower* ya hii benki. Mimi nafikiri hapa tunahitaji *a very specialized personnel* kuendesha shughuli hizi za kilimo kidogo kidogo ambao nafikiri hatuna. Tutakuwa tuna hawa watalaam ambao tutawakusanya sijui kutoka wapi ambao ndiyo hawa wanakaa kwenye maofisi Dar es Salaam huko waanze kusema tunamkopesha mkulima sharti ataleta hati ya nyumba, sijui wenyewe hawajui vijijini kuna hati za nyumba au namna gani hawa watalaam wetu! Hivi wanakaa vijijini au huwa wanafika? Au wanapita na yale magari makubwa wamefunga vioo wanapata *air condition* mle ndani hawajui zile nyumba zina hati au hazina? *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Longa longa!

**MHE. EMMANUEL E. KIPOLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nitoe mapendekezo yangu kwenye hili kwa sababu muda ni mfupi, kama kweli Mheshimiwa amepata fedha za kuanzisha hii benki, ni vema hizi pesa zikawawezeshe wakulima wadogo wadogo sawa na sera yetu kwa maana kwamba sasa hivi zipo *community banks* nyingi, ziko *SACCOS* nyingi kule vijijini na hizi zinaendeshwa na wao wenyewe. Bodi *members* ni wao wenyewe wanaojifahamu hawana hati ya nyumba, si *Board Members* hawa wa Dar es Salaam na Dodoma na kwingineko ni hao wenyewe kwenye hizi *Community Banks,* ziko nyingi na zinaonyesha mafanikio makubwa tu. Zipo hata kule

Mbinga kwa ndugu yangu Mheshimiwa Dr. Luoga, kuna *Mbinga Community Bank,* kuna *Mufindi Community Bank.* Tuna *SACCOS* utitiri na zinafanya kazi vizuri na sisi Kahama Mheshimiwa Naibu Spika, nakutangazia na wewe uje ununue hisa tunaanzisha *Kahama Community Bank.* Ninashauri Serikali ichukue hizi fedha izipeleke kule, kwenye *Community Banks* hizi na *SACCOS* hizi ambazo zinaendeshwa na wao wenyewe wakulima wadogo wadogo na wanafahamiana hata itakapofika wakati wa kukopesha wanajua *specific problems* zao wenyewe. Ni kweli tuna *general problems* kwenye nchi hii, lakini matatizo yako Mheshimiwa Naibu Spika, kule Tunduru si sawa na ya kule kwangu Msalala. *SACCOS* yangu ya kule Msalala wanafahamiana matatizo yao ni *Ox plau*, matatizo ni mbolea. Huwezi ukawa na li-*central organ* ambalo unasema litafanya kusambaza pesa kwa watu wote kadri ya mahitaji yao, si kweli. *(Makofi/Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Longa longa!

**MHE. EMANNUEL E. KIPOLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, huo ulikuwa ushauri wangu. Nina lingine moja dogo nimesema bajeti ni nzuri sana. Kuna mambo tu kama haya ya kushauriana na kutoa ushauri kama mawazo. Kuna hili la Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, kama inavyorekebishwa kwenye ukurasa wa 57 wa hotuba ya Mheshimiwa Mramba juu ya mrahaba au mrabaha kwenye madini, mimi hii imenishangaza kwa sababu tumekuwa tukizungumza hapa kwamba tuache mambo ya mrahaba kwenye madini kwa sababu itaigawa nchi hii. Leo kuigawa nchi kumeondoka, sijui kwa sababu haya madini yamepatikana wapi? Ningependa niseme tu kwamba labda tutapewa taarifa haya madini sasa hivi yanachimbwa na nani kwenye nchi hii na yako wapi ambako hakuna kuigawa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashawishika pia kuamini au kuelewa na pengine ufafanuzi utatolewa hapa kwamba pengine kuna *printing omission* hapa katika ile *gypsum,* chokaa, pozolana, labda kuna *omission* pale ya almasi, dhahabu na madini mengine. Nafikiri kuna *omission* labda kama ipo hiyo basi nashukuru itarekebishwa.

Lakini kama siyo *omission* tuambiwe basi huo mgao wa kuigawa nchi umekwenda wapi? Lakini pia kama ni suala la kuigawa nchi, hivi kweli jamani tuzungumze tu kutoka rohoni hii nchi kweli iko *balanced?* Iko *balanced* jamani? Dar es Salaam ni sawa na Kigoma? *(Makofi/Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Hapana.

**MHE. EMANNUEL E. KIPOLE:** Kwa nini mmekataa hata kuja Dodoma kukaa hapa mnataka Dar es Salaam? Jamani nchi haiko *balanced.* Umeme ukikatika Dar es Salaam wanaandika kwenye magazeti, mwananchi wa Bukombe hajawahi kuona hata huo umeme. Inasitikitisha. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sasa hili ngoja niliachie hapo niendelee kwa kusema ifuatavyo; kule ninakotoka mimi tuna mgodi mmoja mkubwa sana. Nasikitika, kimsingi jamani mchango wa sekta ya madini kwenye nchi hii ni mdogo sana 2.9% mwaka 2003, 2.7 mwaka 2002, 2.5 mwaka 2001. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu hizi ni za Benki Kuu, ni ndogo sana. Kwa kweli kwa hali ya migodi ilivyo kwa sasa mimi ningetegemea mchango wa madini kwenye *sector, I mean* kwenye *GDP* kwa ujumla iwe angalau *digits 2.* Siyo *digit 1, digit* ndogo namna hiyo. Tatizo liko wapi? *(Makofi)*

Tatizo tumelitafuta sisi wenyewe kwa kuingia mikataba ya hovyo hovyo. Mikataba tuliyoingia na hawa watu jamani kwa kweli mimi nimepata bahati na ninasema tu hapa wazi nilifanya *appointment* na Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, nikaenda pale ofisini kwake, bahati na yeye akanipiga chenga. Nikamkuta Kamishna wake, tukamwambia tupe basi hata mkataba tuuone, tuelewe. Akasema tumeshawapelekea huko. Mmempelekea nani? Tumempelekea *DC* na *RC.*

Bahati nzuri *DC* wangu nilikuwa naye pale, nikamwuliza ulipelekewa bwana halafu ukatuficha? Akajibu, sijapelekewa na sijauona. Mkuu wa Mkoa tukampigia simu, bwana unao umeuficha? Akasema, aah! Sijapelekewa. *(Kicheko)*

Sasa tukashawishi shawishi hapo, ikawezekana *DC* apewe mkataba na sisi kama Wabunge tukaweza kuuona. Lakini nashauri hapa *squarely* mikataba hii ni vyema ikabadilishwa *at any cost. (Makofi)*

Hakuna kitu, kuna vivutio vya ajabu, ajabu. Kuna vivutio ambavyo havina maana yoyote. Hiyo *three percent* yenyewe sijui ilifikiwaje. Kwa kweli tulifanya vivutuo ambavyo havipo. Mikataba hii tunashauri au ninashauri ibadilishwe *at any cost. (Makofi)*

Hoja inayotolewa na wataalam, wanasheria wetu wa Serikali, Wanasheria wengine wazalendo, wengine siyo wazalendo. Wanasema oh, unajua tukibadilisha mikataba hii tunapoteza *international credibility.*

Mimi hiyo *international credibility* mnayoisema Wanasheria, siielewi, kama watu wangu wanaendelea kuteseka kule na mavumbi, wanaendelea kuumia, *international credibility for what? (Makofi)*

Unamfurahisha mtu wa nje, mtu wako anaumia, *what does it mean?* Mimi kwa kweli hiyo *credibility* yenu watu wangu wanaumia, siikubali. Nimeleta hoja hapa mwaka jana ya vumbi, nikajibiwa hapa, vumbi hilo haina matatizo yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuja na sampuli ya kilo kumi za vumbi, ninaomba unipe ruhusa nijaribu kutimua hapo mbele kwa wale waliosema, kwa dakika moja tu, *one minute. (Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Hiyo ruhusa haitapatikana hapa. *(Kicheko)*

**MHE. EMMANUEL E. KIPOLE:** Vumbi lile ni kero kubwa, leo unaniambia *international credibility,* watu wangu wanaumia! Sisi katika Halmashauri yetu ya

Kahama tukasema kwamba kuna kisheria ya service levy ya 0.3% kwa makampuni yote, *KMCL* wamekataa kulipa.

**NAIBU SPIKA:** Nafikiri kwa sababu umezungumza na watu wamehamasika sana, kengele ya pili imeshalia. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. PROF. JUMA M. MIKIDADI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kabla ya yote nawapa pole Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, pamoja na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kupotelewa na baba yao mpendwa.

Pili, nawapa pole pia wale waliopatwa na maafa kwa Waheshimiwa Wabunge walipokuwa wanakuja Bungeni na tatu nampongeza rafiki yangu, mtani wangu, ndugu yangu Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kurudi Bungeni kwa tiketi ya CCM. Maana yake mtu ukiwa na mzee wako, baba yako anamnyemelea mkeo, sasa ufanyeje, lazima upigane kiume ili yule mkeo ubaki naye. Sasa nampongeza sana Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kuhifadhi mkewe pamoja na kumfukuza baba yake. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii *fat'wa* ninatoa. Mufti wa Bunge, nimeshatoa *fat'wa*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naingia katika hoja ambayo ni hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji pamoja na Waziri wa Fedha. Kusema kweli hizi hotuba mimi naziafiki sana na naunga mkono hoja mapema kabisa. *(Makofi)*

Pili, kwa sababu tumekuwa wazungumzaji baada ya wenzetu wameshaanza. Tutazungumza yale ambayo hayakuzungumzwa kwa sehemu fulani na mengine nitagusia yale ambayo yameshazungumzwa. Nataka nimwulize Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwa kuondoa kodi au kwa kuondoa ushuru wa biashara isiyofikia milioni 20 kwa mwaka. Maana yake ni kwamba kuleta wamachinga au kuleta wale waliokuwa vijijini vijana waje mijini sasa kufanya biashara. Hiyo ndiyo maana yake. Na hawa waliopo wapate *security,* wapate hifadhi sasa ya kuendelea na shughuli zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakuwa ni balaa kubwa, si suala la uzalishaji, bali itakuwa ni balaa. Pengine inawezekana kuwa kuna *interest* hapa za watu, hawa wamachinga wakija watawafanyia biashara zao, watakwepa kodi upande mmoja. Lakini nasema ikiwa kweli tunataka kuwasaidia wananchi katika masuala ya maisha yao kuondoa umaskini, basi kilimo tunachokisema sisi kitawakomboa, sicho hicho ambacho kinazungumzwa mara kwa mara huko Serikalini, hapana. Ni kilimo ambacho ni cha kugeuza maisha ya watu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati fulani nilizungumza hapa, watu wakaniona mimi kama chizi kwamba tupige marufuku jembe la mkono, chikondola na majembe mengine ili sasa tuanzishe ukulima wa kumkomboa mkulima yule aliyekuwa kijijini. Ukizungumzia jembe hili dogo la mkono basi maana yake ni kwamba tayari mtu atazoea, jembe la mkono tu. Sasa ikiwa kilimo ndicho ambacho kinaweza kumkomboa mkulima

maana yake tugeuze kabisa kwanza, kwamba masuala ya kilimo cha kungojea mvua yaishe kabisa, yamalizike hapo hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni marufuku kilimo cha kungojea mvua. Nasema hilo la pili, sio marufuku jembe la mkono tu, marufuku kilimo cha kungojea mvua, kiwe sasa kilimo cha umwagiliaji tu. Mvua ije kama ziada tu. Lakini bahati mbaya sasa, tunazo hekta karibu 29 milioni ambazo zinafaa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji. Lakini tangu mmwaka 2000 mpaka hivi sasa mradi wa umwagiliaji ulipoanza rasmi yaani mpango ulivyoanza sehemu inayoshughulikiwa au ardhi inayoshughulikiwa kwa umwagiliaji ni 0.68 tu ya eneo kubwa lote. Kweli kuna mpango mkubwa, kamambe, mzito, ndiyo sawa, lakini isiwe katika hatua yenyewe tunayokwenda nayo ni hiyo mpango mkubwa, kamambe, hauwezi kutusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hatua hiyo tunayokwenda nayo ina maana ili kuweza kuleta kilimo cha umwagiliaji kinachofaa itatuchukua miaka 182 siyo mwaka 2025 kufuta umaskini hapa. Itatuchukua miaka 182 na miezi mitatu na siku nne ili kufikia lengo hilo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nani atakayekuwa hapa miaka 182 katika muda huo, hayupo. Kwa hiyo, mimi nasema kilimo ambacho sasa hivi ni lazima tukifanye cha umwagiliaji lakini si kilimo cha umwagiliaji tu, tunaweza kuanzisha viwanda vidogo vidogo ambavyo vitatumia malighafi ile, pamba, nadhani viwanda vyetu vyote vya pamba vile vya awali vimekufa, viliuliwa makusudi ili tupeleke marobota nje. Siyo tupeleke pamba iliyotengenezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivyo hivyo ndiyo vimeuliwa viwanda vingine vyote vya korosho hivyo hivyo, Almasi ile *TANCUT* ya Iringa kule kwa Mheshimiwa William Lukuvi. *TANCUT* imeuliwa ili madini yasikatwe hapa nchini, yapelekwe nje, madini yale iwe rahisi kuiba pamoja na ku-*plunder* mali ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa viwanda hivi ndivyo vingekuwa hawa vijana ambao wako mijini vingewavutia kule vijijini kufanya kazi, kwa hiyo, kungekuwa na *influency* sasa ya kutoka mijini kwenda vijijini kufanya kazi, *unemployment* ingekuwa imekufa kabisa, *natural death.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nazungumza juu ya kilimo kwamba jamani hebu angalieni, hata vile viwanda vya kusaidia kilimo kama *UFI* ilikuwa watu wanapata majembe, *ploughs, tazama* kimeuliwa, nani aliyeua kile? Hakipo, ili tuagize majembe nje, aibu gani hii? Ndiyo kazi gani tunaifanya na tunaangalia hivi mambo haya hayahitaji kwenda shuleni kujua kwamba wanatuulia viwanda vyetu ili tulete bidhaa zao kutoka nje ziingie ndani na kwamba malighafi ambayo tunayo hapa hapa nchini ihamishwe ipelekwe kule kwa ajili ya kuwaneemesha watu wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumza hili kwamba kusema kweli kuna haja ya kubadilisha kabisa masuala ya kilimo tena, Waheshimiwa Wabunge nadhani tuazimie sasa tusizungumze kilimo, kilimo, tumezungumza maneno ya siasa tu, siasa ni kilimo,

kilimo cha bega kwa bega, sijui kufa na kupona. Tunabadilisha maneno tu. Tuache haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tukusudie kweli, nasema ni lazima kuanzishwe *cottage industries* huko huko vijijini na kilimo hicho ndicho kitakachokuwa na faida na kitaleta maana ya kumkomboa mkulima, vinginevyo itakuwa tutazungumza hadithi tu kwamba tuna mipango mikubwa, mipana sana, hauwezi ukasaidia huo mpaka hali halisi ibadilike ya wakulima kule kijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili sitaki nigongewe hata kengele ya kwanza, lakini naona nitagongewa. Suala la madini wameshalizungumzia, amelizungumzia Mheshimiwa Emmannuel Kipole hapa, ameacha upole wake leo, vizuri sana. Juu ya mrahaba, sasa mrahaba ikiwa unarudi kwa chokaa, unarudi kwa *gypsum,* nafikiri kama ungekuwa umefutwa, basi dhahabu, almasi nayo irudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu imesharudi basi dhahabu na almasi nao wapewe, wana haki. Hiyo ndiyo kulinganisha, lakini kitu kimoja ambacho kusema kweli ndiyo nataka nimalizie nacho kwamba kuhusu mgodi wa Mwadui, nataka kutoa mfano wa mgodi wa Mwadui ina-*apply* kwa migodi yote.

Kwanza nampongeza Katibu Mkuu ambaye ni mwadilifu wa Wizara ya Nishati na Madini, Ndugu Patrick Rutabanzibwa, kwa ripoti yake iliyoonyesha deni la Serikali linalotokana na mgodi wa Mwadui siyo lile deni tu Serikali inadaiwa bali hata ile asilimia 25 mali ya Serikali haipatikani, hakuna kitu chochote kinachopatikana katika mgodi huo wa Mwadui.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali halisi ya uzalishaji katika mgodi kila tani za mchanga mia moja inayozalishwa inatoa karati 6 za almasi kwa muda wa saa 8 za kazi huzalisha tani 3,200 ambazo hutoa jumla ya karati 192. Hivyo basi, katika muda wa siku moja (saa 24) kazi inayofanywa kwa *shift* tatu hutoa mchanga kiasi cha tani 9,600 ambazo zinatoa karati 576. Lakini pia wakati mwingine huzalishwa zaidi ya hapo na hufikia tani 12,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inamaanisha kwamba uzalishaji wa siku moja tu unatosha kulipia mishahara ya wafanyakazi na Wazungu waliopo pale na kuendesha mgodi. Lakini tunaambiwa kwamba hakuna chochote kinachofanyika, kinachopatikana. Serikali ina deni pale na hiyo asilimia 25 haipati. Kuna mashirika karibu 6 yananufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mashirika 6 yananufaika, sisi hatuna chochote tunachopata. Huu ni mfano mdogo tu wa Mwadui. Lakini ningetoa mifano mingine ya migodi mingine jinsi ambavyo tunadhulumiwa kiasi ambacho kwa kweli inasikitisha. Kuna *DBI, Diamond Trading Company (DT), CUT, TANEX,* mlolongo chungu nzima. Makampuni sita yananufaika lakini sisi hatuna chochote tunachopata, isipokuwa mashimo tu na kufukuzwa watu wetu pamoja na kuanza kuswaga watu. Hii maana yake nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hili nasema liangaliwe na kuna watu wanazungumza, sisi Wabunge tunazungumza na watu wanalizungumza pia kwamba ndege ndogo ndogo zinakwenda katika sehemu zile za machimbo, zinachukua madini na kupeleka nje bila ya *accountability,* bila ya chochote. Mheshimiwa mmoja alilizungumzia. Sasa kwa nini halichunguzwi kwa hasara ya nani? Na kwa faida ya nani? Ina maana pengine kuna watu wananufaika katika mchezo huo. Hatutaki hilo.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge nasema ni lazima sasa kama jambo lolote la kuchunguzwa ikiwa mikataba au nini Bunge ndiyo lihusike, siyo watendaji wenyewe au watu wanaoshughulika na kazi hiyo, hapana. Ni Bunge hili. *(Makofi)*

Kwa sababu tuko hapa kwa niaba ya wananchi. Kwa hiyo, si suala kwamba afisa fulani, sijui mtalaam fulani, mtaalam gani huyo. Hakutufaa wakati hilo jambo linafanywa, atufae sasa hivi katika uchunguzi. Tunataka sisi wenyewe tuhusike katika uchunguzi na kujua kweli jambo hili la haki au siyo la kweli, vinginevyo hamna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuhuma zote za kuchunguza hamna mtu yeyote wa kuzichunguza, isipokuwa ni haki yetu sisi. Kwa hiyo, masuala ya mikataba, mirahaba, Bunge lihusike moja kwa moja, kwa sababu sisi ndiyo tunaosimamia Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. DAMAS P. NAKEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hamasa nyingi kutoka kwa wasemaji wawili waliopita, sasa ni wakati wa kutulia *naturally.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi hii kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja hizi mbili zilizoko mbele yetu, hoja ya Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mramba, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji na nianze kwa kuungana na wenzangu katika kutoa salaam za rambirambi kwa Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kifo cha baba yao mpendwa na Mwenyezi Mungu tunamwomba aiweke roho yake mahali pema, peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nawapa pole Waheshimiwa Wabunge mbalimbali ambao walipata misuko suko wakati wakija katika Mkutano huu wa Bunge. Wengine wamepata ajali, lakini tunashukuru Mwenyezi Mungu amenusuru maisha yao na wako hapa pamoja nasi katika kutimiza wajibu wetu wa kuwawakilisha wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda vile vile nichukue nafasi hii kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa ushindi uliomrejesha Bungeni baada ya kuwa amedhulumiwa nafasi hiyo ya kuwawakilisha wananchi wake na chama chake za zamani. Karibu tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo labda nirejee kwenye hoja ambayo iko mezani. Napenda nirudie kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri walioleta hizo hoja na

kwa kweli kimsingi ni hoja nzuri, imeandaliwa vizuri kama kawaida, lakini tunapowapongeza wanabaki na changamoto ya kutuhakikishia kwamba hayo waliyotuandalia basi yanatekelezwa kadri ambavyo wametuahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kujitahidi kukabiliana na hali ya dharura iliyokuwa imetokea mwaka huu, hali ya njaa iliyotokana na ukame, hata tukalazimika mwezi Februari, 2004 kuja na *Mini-Budget* au *Supplementary Budget* humu Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafuatiliaji wa mambo haya ya ukame, wanatuambia nchi hii hatujawahi kupata ukame, isipokuwa upungufu wa mvua, upungufu wa mvua uwe mdogo au mkubwa lakini hatujawahi kuwa na ukame ambao ungetusababishia hali ambayo tulikabiliana nayo mwaka huu na kwa kweli kama tunataka kufahamu habari ya ukame basi tukumbuke hali iliyotokea Ethiopia, Somalia na Sudan ambapo mvua inakosekana kwa miaka mitatu mfululizo. Kwa hiyo, ninachotaka kusema ni nini, ni kwamba kutokana na hali ya upungufu huo basi kumbe tungeweza kuidhibiti kutokana na mbinu ambazo tungeweza kutumia kwa maana ya mazao ambayo yanastahimili upungufu huo lakini vile vile yanayoweza kustawi kwa mvua chache.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kwa Serikali ni nini? Mimi niseme changamoto ni hiyo ya kujaribu kuzingatia hali ya hewa na vile vile kwa kuwatahadharisha wakulima kwamba sasa mwaka huu hali ya hewa si nzuri, kwa hiyo, tujitahidi kupanda mazao yanayostahimili hali ambayo tunaitazamia. Kwa hiyo, kumbe kuna haja ya Idara ya Hali ya Hewa kuwa makini na kuwa ya kisayansi na kuwa ya kisiku hizi na ya kileo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hiyo mpaka sasa hivi ni ya kutatanisha, hilo ni changamoto kwa Serikali yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo basi ni vizuri Serikali ikapokea changamoto ya kuondokana na aibu ya omba omba. Omba omba ya chakula. Kila mwaka tumezungumza habari ya kilimo, kilimo, kilimo bora. Lakini tunapiga *mark time,* hatusongi mbele. Sasa mimi nafikiri tuhame kutoka kwenye hii *monotony* ya kuzungumzia kilimo bila kupiga hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema mwanzoni Bajeti hii ni Bajeti nzuri na nasema maeneo ambayo tunayapongeza ni pamoja na ongezeko la mapato ya Serikali, makusanyo mazuri ambayo yametokana na jitihada ya Serikali kujaribu kuhakikisha kwamba mapato ya Serikali yanapatikana. Sina hakika kwa wale ambao wana-*challenge* kama malengo yalikuwa yamepangwa vizuri maana yake unaweza ukapanga lengo ambalo ni rahisi kulitekeleza halafu baadaye useme umelivuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi ninaamini kwamba ilikuwa ni nia njema na makusanyo hayo yamevuka malengo ya kweli. Kodi ya *VAT,* kodi ya mapato, ushuru wa Forodha na kadhalika. Ni maeneo ambayo kwa kweli tunaisifu Bajeti hii kwamba wamejitahuidi. Lakini wajitahidi zaidi na zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuongezeka kwa mapato ya Serikali maana yake vile vile ni kuongezeka kwa uwezo wa Serikali katika kutoa huduma kwa wananchi na Serikali yetu tunafahamu sasa hivi haifanyi tena biashara. Suala zima la kujenga uchumi, kufanya biashara, linafanywa kwa kiasi kikubwa zaidi na Sekta binafsi. Kwa hiyo, Serikali ina jukumu la utawala, ulinzi wa amani, amani ya nchi na raia wake na sasa kwa maana hiyo basi, tunaamini uwezo wa Serikali sasa kwa kutokana na mapato kuwa zaidi uwezo wake pia unaongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ina maana kwamba mwaka huu lazima Serikali ifanye vizuri zaidi kuliko walivyofanya mwaka uliotangulia na kwa maana hiyo basi katika eneo la ulinzi na usalama wa wananchi tusingependa tena kusikia habari ya kukithiri kwa ujambazi na ulevi wa gongo. Sasa hivi watu wanasema hata kule vijijini kwamba kwa kweli ulevi wa gongo ni vita ambavyo haviwezekaniki kwa sababu ni mradi wa viongozi kule vijijini. Sasa mradi hauwezi kwisha kwa sababu pale ndiyo wanakopatia mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nasema Serikali iache sasa visingizio vya kusema ushirikiano wa wananchi unahitajika katika suala la kupiga vita ujambazi. Tunaongezea fedha wafanye kazi. Mwaka juzi tuliwaongezea fedha, tuliwapa fedha nyingi, hatujaona *impact* ya fedha zile ambazo tuliwaongezea wakati ule, bado ujambazi unaongezeka na sasa hivi unafanyika hata mchana, *day light robbery.*

Mimi nilifikiri pia wakati umefika wa kupiga vita au wa kupiga marufuku labda, *fire arms* zote. Labda silaha hizo zibaki kwa Jeshi la Wananchi. Lakini hii habari ya kusema kuna bunduki zinamilikiwa kwa halali na kadhalika, hii yote ipigwe marufuku. Hakuna sababu ya mtu kujilinda kama nchi iko salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ulinzi wa nchi tuuachie Jeshi la Wananchi. Kwa hiyo, hii habari ya kujilinda, unajilinda *against what?* Kwa sababu kuna usalama. Sasa tunasema kuna nchi nadhani duniani zimepiga marufuku *fire arms* zote, kwa hiyo, inakuwa ni rahisi ku-*track* wale ambao wana *own illegally.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa leo huwezi kutenganisha au huwezi ku-*distinguish* kati ya yule ambaye ana-*own legally* na yule ambaye ana-*own illegally* na silaha ambazo zinatumika inawezekana ni zile ambazo watu wana-*own legally.* Kwa hiyo, mimi nashauri kwa kweli hili liangaliwe vile vile. Lakini vile vile tumesikia sana kila mara ajali barabarani. Haya yangekuwa mambo katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, lakini niseme Serikali ianze kufanya kazi yake kwa makini zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kidogo habari ya umaskini. Tunaambiwa tathmini ya umaskini katika kuangalia mkakati wetu wa miaka 25 ya kuondoa umaskini inafanyika kila miaka mitatu. Mimi nilifikiri ni vizuri tupunguze muda huo kwa miaka miwili ili kama kuna dosari humo katikati basi kuwe na muda wa kurekebisha mapema kuliko kuchukua muda mrefu zaidi.

Lakini niseme katika eneo hili la kuondoa umaskini kuna mambo ambayo yana-*frustrate* wananchi wetu katika kupiga vita umaskini na nitaje kwa mfano eneo la kilimo. Eneo hili pamoja na kuwa tunahimiza wananchi kufanya kazi kwa bidii lakini upande mwingine wananchi wanakuwa *frustrated* kwa sababu mbalimbali. Kwanza kwa mfano wakulima kwa mfano wa Wilaya yangu ya Babati, hususan Kata moja ya Bonga, wanalima kahawa pale, wakati fulani walipata dawa kutoka kwa *Supplier* mmoja lakini dawa hiyo ikaja kuua kahawa yao. Wamehangaikia tatizo hilo kwa miaka mitano mpaka leo hakuna jibu. *They are frustrated* kwa hiyo, huwezi kusema unahimiza kilimo, huwezi ukasema una-*encourage* kilimo huku unavunja miguu wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano wa pili, ni Kata nyingine, wananchi badala ya kufanya kazi za kilimo kwa bidii, kila siku wanazozana, wanakwenda kwenye kesi za kunyang'anyana ardhi, vipande vya ardhi na mashamba na viongozi wa vijiji. Unakuta kiongozi wa Kata anakuwa ni *part of that problem* inakuwa sehemu ya matatizo hayo. Kwa hiyo, nilifikiri Serikali katika ngazi ya Wilaya ichangamke zaidi na kuona kwamba kwa kweli wananchi hawawi *frustrated* katika suala zima la kilimo katika eneo hilo la kilimo.

Lakini nije upande wa barabara, katika *para* ya 40 sehemu ya 6 inasema Serikali itaendelea na utaratibu wa kutumia fedha za ndani kujenga barabara. Sote tunafahamu kuwa fedha hizo za ndani zimekwishaanza kufanya kazi hiyo kwa barabara za Mwanza - Dar es Salaam - Mtwara yaani hiyo barabara ambayo *is the most celebrated* katika mpango mzima huu wa kutumia fedha za ndani.

Sasa hatujaambiwa mpaka sasa hivi ni barabara ipi inafuata baada ya hiyo barabara ya Mtwara-Dar es Salaam-Mwanza. Ni vizuri tukafahamu katika mpangilio baada ya mradi huo kwisha unafuata mwingine, tufahamu *in advance. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa leo nataka nifahamu kuhusu barabara kuu ya Kaskazini itokayo *Cape Town* - Cairo. Kwa kweli inaaibisha kuona sehemu kidogo sana ya barabara hiyo kutoka Dodoma - Iringa - Minjingu ndio pekee ambayo ni changarawe katika *network* yote hii ambayo nimeitaja. Lakini haizungumzwi kwamba barabara hii itapewa kipaumbele ambacho kinastahili kutokana na *international status* ambayo barabara hiyo inayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapoambiwa fedha za *World Bank,* nina wasiwasi maana yake *we are really deferring implementation* ya kazi ya barabara hiyo. Kwa hiyo, ni vizuri kama kweli kipaumbele kipo kwa maana ya vipaumbele katika sera zetu kutumika kwa fedha hizi za ndani basi barabara hii iwe *the second to the ongoing project now.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri nihimize hilo kama hizi fedha za ndani zipo nielezwe kwa nini zisitumike kujenga barabara hii? Vile vile nashauri utumike mpango ule unaoitwa *Design and Build* ambao haucheleweshi ujenzi wa barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kidogo kuhusu elimu na nishukuru kwa maendeleo makubwa ambayo nchi yetu imepata kutokana na Elimu ya Msingi. Mpango

wa Elimu ya Sekondari (MMES) utakaoanza hivi karibuni hatimaye ulenge elimu hiyo kuwa ya wote mpaka Kidato cha Nne *(Ordinary Level)* kama Elimu ya Msingi. *Ordinary Level* maana yake ni elimu ya kawaida kwa wananchi wetu wote, Elimu ya Msingi haitoshi hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote kwa sababu nilishatoa rambirambi zangu kwa ndugu yetu Dr. Abdallah Kigoda na mdogo wake, Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda. Moja kwa moja nianze kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda nimshukuru Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji, kwa hotuba nzuri ambazo kwa kweli zina kina na mwelekeo unaoonekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nichukue nafasi hii kuwapa pole wale wenzetu waliopata misukosuko mbalimbali wakati wakija hapa Dodoma kama vile dada yetu Mheshimiwa Anne Malecela, Mheshimiwa Estherina Kilasi na Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia dondoo ya Bajeti ya mwaka 2004/2005 katika eneo la sekta za kipaumbele chini ya Mkakati wa Taifa wa Kupunguza Umaskini zitaendelea kupata mgao mkubwa wa asilimia 46 ya matumizi na zimeonyeshwa hapa. Kutokana na michango ya Waheshimiwa Wabunge, ningeomba *priority* zilivyowekwa zibadilike kama sio katika Bajeti hii basi katika Bajeti ijayo. Ningeomba kabisa ile ya kwanza ingekuwa kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama *priority* ya kwanza ingekuwa kilimo nina hakika hata haya maeneo mengine ambayo tunayazungumza ya elimu, afya, maji na kadhalika yangeweza kuhudumiwa kwa sababu nia ni kuondoa umaskini. Maeneo yote haya ambayo tumeyapa kipaumbele kwa kweli tumeyapa kutokana na mikopo. Sasa ili tuweze ku-*sustain* ni lazima tuimarishe kilimo, umaskini upungue na tuweze ku-*manage,* ku-*sustain* hizi *sector* nyingine. Nashauri sana ikiwezekana ifanyike hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije katika uchangiaji ambao napenda kuzungumzia. Nitajielekeza katika maeneo matatu muhimu. Kwanza ni umuhimu wa udhibiti katika uchumi. Pili, uchumi wa kijiografia na mwisho nitazungumzia kidogo sana suala la Bajeti tegemezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza katika suala la udhibiti wa uchumi, nina wasiwasi sana wa yale tunayoamua na mafanikio tunayoyapata bila kuwa na udhibiti na mafanikio haya kwa kweli yote yatapotea. Nitataja maeneo matatu muhimu katika udhibiti ambayo Bunge lako limeweka vyombo vya udhibiti lakini bado ninaamini udhibiti hautoshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuje katika upande wa fedha. *BOT* ndio inayopaswa kudhibiti mwenendo wa fedha au vyombo vya fedha hapa nchini lakini ukiangalia kazi inayofanyika kwa upande fulani ni nzuri lakini kwa upande mwingine sio nzuri. Hebu angalia ni kweli tumefanikiwa katika udhibiti wa mfumuko wa bei lakini mfumuko wa bei bila kumwangalia mlaji wa mwisho hautasaidia, utauona juu lakini chini haufiki. Tatizo la *BOT* au udhaifu wake utauona katika udhibiti wa kushuka kwa thamani ya fedha yetu (shilingi). *(Makofi)*

Leo ukipata dola moja ni shilingi 1,100 hii ina maana kwa mwananchi kwa miaka minne iliyopita atanunua *spare* ya gari lake kwa kutoa kilo mbili za pamba leo ili aweze kupata hiyo *spare* ya gari lake. Hapa hata kama ungemwambia nini katika mfumuko wa bei bado mwananchi huyo hajanufaika kwa sababu itabidi anunue *spare* hii kwa gharama kubwa sana leo kutokana na kushuka kwa thamani ya fedha yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ilikuwa na hadhi ya kuonekana kwamba nguo na vifaa vingine vinapatikana kwa bei nzuri lakini leo hata elimu ni ghali vijana wetu wengi wanakwenda Uganda kusoma kwa sababu kule elimu ni chini. Ukiangalia kwa thamani ya fedha ya nchi yetu utalipa kidogo zaidi Uganda kwa hiyo watu wengi wanakwenda Uganda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tusipoangalia kushuka kwa thamani ya fedha yetu, nina hakika mafanikio tunayoyapata yatakuwa hayasaidii sana na nchi yetu tunavyoingia katika Soko la Afrika Mashariki, *SADC* siamini tutaogeleaje ili tuweze kufanikiwa. Nafikiri Serikali inaliona hili na tunapenda kujua wanachukua hatua gani kupunguza na kuhakikisha kwamba thamani ya shilingi haipungui sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo ambalo halikutajwa hapa katika kupungua kwa thamani ya hela yetu mwaka jana nilisema na kazi hii ni kazi ya Benki Kuu, ni wizi wa fedha za kigeni. Uko wizi mkubwa sana wa fedha za kigeni, zinatoroshwa kiajabu sana. Leo ukienda Afrika ya Kusini sio rahisi kutoa hata dola moja utoke nayo kienyeji leo hapa kwetu hivi sasa ukiniambia nakwenda Ulaya nipe masaa mawili nitachukua dola kiasi chochote ninachotaka kuondoka nacho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huwezi kuongoza nchi katika hali ya namna hiyo. Unafungua uchumi na wewe hicho kitu hunacho unaringia mali ya wenzako. Maana sasa hivi tumeambiwa tuna akiba kubwa ya fedha za kigeni lakini amini, msiniamini, akiba hii sio fedha zetu maana hatujazalisha vya kutosha kupeleka nje. Tutaweza kusema tuna *sustainable economy* kama tuna uwezo wa ku-*export* lakini hela hizi ni za misaada, mikopo tutarudi kule kule tulikotoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1964, 1965, 1970 tulikuwa tunapata misaada na mikopo hii nchi hii tulifanya vitu vya ajabu sana. Tumejenga vitu vingi sana zahanati, shule lakini mwishowe tulishindwa kwa sababu tulishindwa kuji-*sustain* kutokana na kutegemea misaada na mikopo matokeo yake uzalishaji wa ndani haupo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ni lazima Benki Kuu iangalie, ni lazima Serikali iangalie tufanye nini. Yaliyoelezwa katika hotuba ya Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji, ku-*promote* uuzaji bidhaa nchi za nje bado naona ni mambo madogo sana yamezungumzwa. Vimezungumziwa viwanda vya *EBA, AGOA, NIDA* ni viwanda vichache sana ukiangalia msukumo wetu wa kuuza nje hatua hii bado haijafikia mahali ambapo tunaweza kusema baada ya hawa wanaotusaidia wakiondoka tutaweza kumudu uchumi wetu, haiwezekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi zote ambazo zinaendelea *incentives* katika *export* zinatolewa kwa ukubwa sana. Misaada kwa ajili ya *export* iongezwe, watu wanao-*export* wapewe nguvu hii *Export Guarantee* hata watu hawaijui ni watu wachache sana na ni wajanja wale ambao hawana nia nzuri katika nchi hii ndio wanaojua *what is real Export Guarantee* na mwananchi wa kawaida anayezalisha *green peas* zake hana *idea* yoyote ya ku-*export* hiyo *green peas* yake kwenda Ulaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ni watu wachache sana wanajua kwamba maua ni *export* nzuri sana. Ni watu wachache wanaelewa kwamba matunda ni *export* nzuri sana lakini hawa wakulima hawajasaidiwa. Huwezi ukalichukua *apple* la Lushoto ukategemea ulipeleke Marekani lina vidonda 400 watakushangaa, utakaa nalo pale *airport,* hutaweza. Sasa wakulima wanahitaji kusaidiwa kwa kupatiwa madawa, huduma za ugani, mbegu nzuri haya ndio maeneo tunayoweza ku-*export* vizuri sana. Hilo ni eneo moja nilitaka nizungumzie udhibiti wa Benki Kuu katika kuhakikisha kwamba fedha hazitoki ovyo na vile vile kusaidia *exports.*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningependa nizungumzie ni eneo la nishati. Hapa tulishaunda chombo cha kudhibiti eneo hili la nishati na *utilities (EWURA).* Huu ni mwaka wa nne bado hakuna juhudi zozote zinazoonekana kwamba chombo hiki kinaanza, nataka Serikali itamke vipi chombo hiki?

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi hapa *TANESCO* hao ndugu zetu wa *Netgroup Solution* wameongeza bei kwa mlaji na kwa bahati mbaya sana wameongeza bei kwa mlaji mdogo, mwananchi wa kawaida na wamesema watapunguza bei kwa wazalishaji wakuu. Hili lina hatari kubwa sana. Naona Wabunge wengi hawajalizungumzia hili lakini amini, msiamini, *Netgroup Solution,* kwanza mimi siwaungi mkono na namwomba Waziri wa Nishati na Madini watu hawa wasipewe mkataba, wanatudanganya *they are just as good managers as we are,* tupo ma-*manager* wa Tanzania wenye uwezo. Tulichowafanyia hawa ni kuwapa *conditions* nzuri wakaweza ku-*manage TANESCO.* Hayo madeni wanayokusanya mimi siyaoni na kama kweli wangekuwa wanakusanya basi Serikali isingetoa fedha nyingi kiasi hiki kama ruzuku kuhudumia *TANESCO. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kilichofanyika ni kuongeza bei ya mlaji mdogo na kujidai kusimamisha bei ya mlaji mkubwa sasa katika nchi yetu misitu itakwisha. Pia hata huo umeme wa *rural energy* ambao tunaanza watampelekea nani kama hawawezi kununua? Kwa hiyo, kwa sasa hivi *TANESCO* kupitia *Netgroup Solution* wamejitoa kijanja maana wale ni wajanja wamejitoa katika *rural energy* wanasema huko nendeni wenyewe wao tuwape kwenye nundu ili waendelee kula, nasema mkataba usiongezwe hapa nchini tunao ma-*manager* wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ambalo nataka nizungumze kwa kifupi sana ni suala linalohusu uchumi wa kijiografia kwa sababu muda ni mfupi sitaweza kuzungumzia uchumi tegemezi.

Serikali haijazungumza kitu cha kutosha hapa kuhusu reli na bandari. Uchumi wa jiografia katika nchi hii ambapo tunategemea bandari ya Dar es Salaam tuna nchi ambazo haziwezi kupitisha mizigo yao, ni hela zipo. Leo tunafikiria kubinafsisha reli ni kweli tunaweza kubinafsisha lakini ubinafishe kitu ambacho kinaweza kuleta faida kwa huyo atakayechukua, vinginevyo watakaokuja kupenda kuchukua reli hii ni wale matepeli sio watu wa kweli wa kuja kuwekeza. Kitu kinachohitajika kwa upande wa Serikali sasa hivi ni kuwekeza katika reli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi kwa uvumilivu wake. Yeye hatujampa fungu hapa ni kweli tumetoa kwenye barabara lakini tumesahau *ingredient* ya reli.

Mimi ningekuwa na mamlaka ningesema leo twende Benki ya Dunia tukakope tu-*rectify* reli hii tujenge laini ya kwenda na kurudi Kigoma na Mwanza muone uchumi wa nchi utakavyofunguka lakini tunazungumzia tu mambo ya juu juu bila kuangalia kwa undani. Leo mzigo uliopo Zaire, Kongo, Burundi, Uganda ukiupitisha hapa kwa reli inayokwenda njia moja na inayorudi njia ya pili ni mzigo wa kuboresha uchumi wa nchi hii mshangae.

Hakuna anayelifikiria hilo tunaogopa kukopa kwenye Benki tunakopa mikopo sawa tunaweza kukopa kwa ajili ya elimu, afya lakini baada ya hao wanaotukopesha kuondoka tutarudi kule kule maana zahanati tulikuwa nazo tumejengewa na *DANIDA* tumeshindwa kuziendesha kwa sababu hatukuwa na *sustainable economy* na unaweza ku-*sustain economy* kama una vyombo vya ku-*sustain* kiuchumi kama reli na bandari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, reli tunayoichezea leo imejengwa na mkoloni mwaka 1905 mpaka leo bado tunaendelea kuikodisha kama ingekuwa nyumba milango ingevunjika na nini, sasa sisi tunakwenda kuikodisha wakati milango imevunjika, sio busara. Kikubwa huyo anayekuja kukodisha ataondoka na milango, mabati ataondoka nayo, vitasa ataondoka navyo. Mimi nashauri tuwekeze katika reli kwa kweli twende kwenye hiyo mikopo ya *World Bank* tuwekeze kwenye reli tutaifufua bandari ya Dar es Salaam, tutaijenga Zanzibar na nina uhakika nchi itaendelea kwa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali na Waziri wa Fedha hili tumelisahau maana reli tumeizungumzia tu kama jambo la kawaida na wakati tunaibinafsisha. Sasa naiomba Serikali iangalie reli kama muundo mbinu muhimu wa kufufua uchumi wa nchi hii na ninawahakikishia kwa mzigo ulioko katika nchi *landlocked,* tutapata fedha nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. JOHN L. MWAKIPESILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe mwenyewe kwa kunipa nafasi hii ili nami nitoe machache juu ya hoja hizi mbili ambazo ziko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa pole kwa Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na dada yake, Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kufiwa na baba yao mpendwa. Vile vile napenda kutoa pole kwa Waheshimiwa Wabunge waliopata mikasa mbalimbali kama vile ajali za magari na waliovamiwa na majambazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda nimpongeze Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kuingia tena ndani ya Bunge hili kwa kushinda uchaguzi mdogo wa Bariadi kwa kishindo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza kwa dhati Waziri wa Fedha na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, kwa kutoa hotuba nzuri sana ambazo zinaeleweka, zenye mtiririko mzuri wa hoja mbalimbali na hotuba ambazo zimesifiwa sana na wadau wote waliopata nafasi ya kuzungumzia. Pia nachukua nafasi hii kuwapongeza Makatibu Wakuu wa Wizara zote mbili na wataalam wa Wizara hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa moyo wa dhati kabisa, napenda kuwapongeza wafanyakazi wa *TRA* kwa kazi nzuri sana wanayofanya ya kukusanya mapato ya Taifa. Vile vile niipongeze *BOT* kama alivyozungumza Mheshimiwa Henry Shekiffu, wanafanya kazi nzuri ya kusimamia *fiscal policies* za nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niipongeze *PSRC* kwa kazi nzuri ambayo wanafanya. Kubinafsisha mashirika ya umma ni kazi ngumu lakini hatua waliyofikia inatupa moyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nimpongeze sana Mhasibu Mkuu wa Serikali kwa kazi nzuri sana anayoifanya kudhibiti wizi wa fedha za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema wadau wengi wameipongeza sana Bajeti hii wanasema ni Bajeti ya mnyonge na maskini na mimi naipongeza. Lakini ukiitazama Bajeti yenyewe nayo ni maskini kwa hiyo ni Bajeti maskini ambayo inatazamiwa kusaidia maskini na wanyonge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumzie yale ambayo yameonyeshwa katika kitabu cha hotuba cha Waziri wa Fedha ukurasa wa 62 na 63. Ukurasa huo kwa kweli unaonyesha mizania ya mapato na matumizi ya Serikali. Pale tunaelezwa jumla ya mapato ya Serikali kwa mwaka wa fedha ufuatao itakuwa trilioni 3.3. Lakini katika fedha hizo trilioni 1.367 ni mikopo na misaada kutoka nje. Hiyo maana yake ni 41% ya mapato ya Serikali yanatoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitazama upande wa matumizi kati ya fedha hizo ambazo zitakusanywa trilioni 3.3, trilioni 2.239 ni matumizi hiyo ni sawa na 67%. 67% ya fedha zote ambazo zitakusanywa kwa maendeleo ya nchi hii zitakwenda katika matumizi yaani utawala. Sehemu inayobaki kwa maendeleo ni 33% tu lakini katika hizo

33% tunategemea kupata fedha ndani ya nchi 21.4%. Asilimia 78.6 za fedha za maendeleo zitatoka nje, mikopo na misaada. Ndio maana mimi nimeita hii ni bajeti maskini kwa kuwatumikia wananchi maskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kutoa ushauri, kwanza tuchukue fedha zaidi ambazo ziko kwenye *foreign reserves* tukaziweka katika mapato ili tupunguze utegemezi. Tumeambiwa hivi sasa *foreign reserves* zimefikia karibu trilioni 2 lakini fedha ambazo zimechotwa katika *reserves* hizo na kupelekwa kwenye mfumo wa Bajeti ni 10% ya *reserve* hizo. Tumechukua bilioni 231,111 tu ambayo ni 10%. Kama itawezekana ni vizuri kuchukua hizo *reserve* na kuongezea pale 15% - 20% ya *reserves* hizo ambazo tunazo ku-*support* Bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kama ushauri huo utakubalika basi nimwombe Waziri wa Fedha atupe mchanganuo wa *foreign reserves* ambazo tunazo. Inawezekana anazungumza haya hatuna fedha taslimu pale inawezekana ni mikopo kwa sababu ukitazama mauzo ya nje ni kidogo sana. Sasa tupate mchanganuo wa *reserves* hizo kiasi gani ni mauzo yetu ya nje, kiasi gani ni mikopo, kiasi gani ni misaada, kiasi gani ni mapato kutokana na vitega uchumi tulivyonavyo nje ya nchi. Tukipata hilo, basi tunaweza kufikia uamuzi kwamba ni vizuri tuchote kidogo hapo tuongeze mapato ya Taifa na kupunguza utegemezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu wa pili, katika matumizi maalum kuna vita dhidi ya rushwa, kipengele (d) ambacho kimetengewa milioni 857.

Naomba kusema kweli kwamba hizi fedha hakuna haja kuziweka kutumika katika vita hivyo vya rushwa kwa sababu mimi sivioni vita hivyo hata kidogo. Vita ambavyo havina hata *rules of the game,* vita ambavyo havina hata uwanja wa kupigania, vita ambavyo hatuoni hata Askari wanaopigana kwa kweli tungechukua fedha hizo tukazipeleka katika Wizara ya Ujenzi au Elimu zingefanya kazi nzuri zaidi kuliko zilivyowekwa pale. Kwa sababu hivi sasa rushwa inazungumzwa mdomoni tu kila unapojaribu kuzungumzia rushwa unaona sura za wakubwa zinakunjamana, wanakasirika na wanakuambia katuletee ushahidi wa rushwa, nani anakula rushwa. Sisi Wabunge wengine ambao ni jasiri tumeweza kwenda kwenye Mawizara na kuwaeleza wanaokula rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi natoka katika Wilaya ya Kyela. Katika Wilaya ya Kyela tunajenga madaraja *substation bridges* nimejenga madaraja mawili kwa kuyasimamia mimi mwenyewe moja kwa shilingi 16 milioni na lingine kwa shilingi 14 milioni. Lile la kwanza Mheshimiwa Basil Mramba ni shahidi wangu alikuwa Mkuu wa Mkoa pale na tulisaidiana sana kujenga daraja hilo tukalijenga nikapata shilingi milioni 16 tukalijenga. Juzi wamejenga daraja ambalo *information* zote wameficha kwa Mbunge hawakutaka kumweleza Mbunge. Nilipokwenda Wizarani kuwauliza mmepeleka kiasi gani kule wanasema wamepeleka shilingi milioni 129 kwa kidaraja ambacho kinaweza kujengwa kwa shilingi milioni 20. Wananchi wangu Wilayani Kyela wamenieleza wanaokula fedha ni huyu na huyu, nimepeleka majina, hakuna kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri Mkuu kila mwisho wa Bunge hapa anatoa hotuba ndefu sana na kutuomba Wabunge tukifika Majimboni tumsaidie, kazi ya kudhibiti matumizi ya Serikali ni moja ya kazi ya Mbunge kusaidia. Sasa Mbunge afanye nini kudhibiti fedha ambazo zinakwenda Jimboni kwa maendeleo ya wananchi wake? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hizi fedha mlizoweka hapa Mheshimiwa Basil Mramba ziondoe zipeleke Ujenzi, Elimu, Mawasiliano zikafanye kazi kule. Hivi sasa hakuna sehemu yenye wizi wa fedha kama Wizara ya TAMISEMI huko vijijini na ni dhambi kubwa kwetu sisi Wabunge ikiwa tutaogopa kusema hayo kwa sababu wenzetu waliopata vyeo huko juu hawana nafasi kuyaona madhambi yanayofanywa huko vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka niseme hilo kwa sababu lipo moyoni mwangu linaniuma. Fedha nyingi ambazo tunazipata za mikopo, misaada na makusanyo kutokana na kodi zikienda huko zinaliwa na watu hao tunawajua lakini hatupati msaada sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kwa haraka haraka ni ukuaji wa uchumi. Hili suala la ukuaji wa uchumi hakuna tofauti na ukuaji wa mtoto uliyemzaa. Ukizaa mtoto unategemea atakua *uniformly* viungo vyote, huwezi kuzaa mtoto anakuwa kichwa na sauti tu ukasema huyu mtoto anakua na ana afya. Haiwezekani hata kidogo, ni lazima akue viungo vyote ndiyo useme mtoto anakua. Hali kadhalika ukichukua uchumi wa Tanzania, chukua kilimo, wanaposema kilimo kimekuwa kwa asilimia nne mimi sielewi hata kidogo labda sehemu zingine, Kyela hiyo asilimia nne haionekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wanaposema uchumi unakua wakati viwanda vyetu havizalishi kwa sababu ongezeko la bidhaa zinazozalishwa katika viwanda vyetu ni kidogo sana ukilinganisha na bidhaa ambazo tunazitumia katika soko ambazo zaidi ya 90% zinatoka nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukichukua thamani ya shilingi ambayo inaporomoka kila siku, maana yake nini? Maana yake manunuzi yote ambayo yanaingia ndani ya nchi ni ghali na kama mnazo bidhaa chache mnauza nje zinakuwa na bei ya chini kabisa kwa sababu fedha yenu haina thamani. Sasa nikiambiwa leo kwamba *inflation* ya nchi hii imefikia *four percent,* sielewi ndiyo maana nilimpongeza Gavana wa Benki Kuu maana Gavana wa Benki Kuu amekaa mlangoni na begi la fedha anacheza nazo katika soko. Akiona bei za vitu zinapanda juu, anapunguza mzunguko wa fedha katika soko. Akiona bei zinakwenda chini sana anaongeza fedha. Ujazi wa fedha katika uchumi ndiyo mchezo ambao unachezwa hapa, *it is a very dangerous exercise, it is a rope-walking exercise* maana ukitembea kwenye kamba hauna *balance* utaanguka mara moja tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na ninaunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. CHARLES H. KAGONJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana mchana huu kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika Bajeti hizi mbili ambazo zipo mbele yetu. Lakini kabla sijafanya hivyo niruhusu pia kama wenzangu walivyofanya, nitoe pole za dhati kabisa kwa ndugu yangu Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na dada yetu Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kumpoteza baba yao. Lakini pia nitoe pole nyingi kwa Waheshimiwa Wabunge wenzetu ambao wamepata matatizo ya ajali mbalimbali na waliolazwa hospitali wakati wakija Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda nimpongeze ndugu yangu Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kurudi Bungeni hapa kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi, nampongeza sana. Lakini pengine nichukue nafasi ndogo niwapongeze pia wale majemedari wa Chama cha Mapinduzi ambao walikuwa mstari wa mbele katika kumrejesha mwali huyu ndani ya Bunge hili. Namheshimu sana Mzee wetu Mheshimiwa John Samwel Malecela kwa kazi aliyoifanya akiwa kiongozi wa mapambano hayo. Tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wetu wawili, Mheshimiwa Basil Mramba na Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, kwa kazi nzuri ambayo wameifanya ya kutuletea Bajeti hizi ambazo zimeandaliwa vizuri na kwa kweli zinastahili kuungwa mkono. Pia nawapongeza Manaibu Waziri, Makatibu Wakuu na wengine wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mengi yamesemwa hapa na wenzangu lakini na mimi lazima niongeze sauti yangu katika hayo yaliyosemwa. Kwanza kabisa naomba niliseme lile moja ambalo lilisisitizwa sana na Waheshimiwa Wabunge kwamba ni muhimu sana jambo hili lifanyike kwa haraka kuwalipa mishahara walimu wetu wapya wanaoajiriwa. Kwa sababu wanafanyakazi nzuri, kazi ya heshima sana, kazi takatifu kwa Taifa hili, kwa hiyo mishahara yao ipelekwe haraka walipwe bila kuchelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, mimi nilikuwa nauliza benki hii ya mkulima ambayo inaanzishwa hivi itaanza lini, itakuwa wapi, hivi ni lini itaenea nchi yetu yote au itakuwa wapi ili Watanzania waweze kuifikia kwa urahisi. Huko nyuma kama tunavyokumbuka tulishauri sana kwamba benki ya *NMB* ibadilike iwe benki ya wakulima, Serikali ikakataa. Sasa tunaomba maelezo ya kina katika hili kwa sababu ni moja katika mambo ambayo yatamsaidia mkulima kama tuna nia kweli ya kumsaidia mkulima mdogo aondoke pale alipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ninalotaka kusema ni kwamba yapo mambo na malalamiko mengi sana yametolewa hapa Bungeni na Serikali ya watu, kwa niaba ya watu, inatakiwa iyasikilize hayo ambayo wawakilishi wa watu wanayasema.

Mimi naomba kuungana na wenzangu hasa wale ndugu zangu Wasukuma wanaopiga kelele sana kuhusu hili jambo linaloitwa mrabaha. Kwa jinsi ya kauli za Serikali zinavyotuchanganya mimi sioni kwamba kuigawa nchi hii kutatokana na kutoa mrabaha kwa yale maeneo husika. Mimi naona kwamba kauli za Serikali ambazo hazipo sahihi na wazi kwa Watanzania hizi ndizo zinaweza kuigawa nchi. Tunaomba majibu

yatolewe kwa nini maeneo mengine yapewe mrabaha na maeneo mengine yasipewe. Hili ni jambo liwekwe wazi ili nchi yetu na Watanzania wote waweze kuelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine dogo ambalo nilitaka kuchangia ni lile ambalo aliwahi kulichangia rafiki yangu Mheshimiwa Joel Bendera, Mbunge wa Korogwe Mashariki kuhusu yale mashamba ya Mkonge au mashamba ya Katani ambayo hayalimwi, tunayaomba kule Tanga hata kule Morogoro yarudishwe kwa wananchi wafanye hiyo kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kule kwetu Lushoto na hasa katika Jimbo langu la Mlalo kwa wale waliofika kule kila mahali ni sawa na Mji, mgeni huwezi kujua Kijiji wala Kata, Kata ya Mlalo, Mwangoi, Malindi, Shume, Rangwi, Sunga na Mtae yenyewe yote ni Mji, umeshikana hakuna hata sehemu moja ya kupanua mashamba.

Sasa tunaomba tafadhali mashamba haya ambayo hayatumiki watu wameshindwa kuyafanyia kazi tupeni tuungane na ndugu zetu wa Korogwe na Muheza ili tuweze kuyafanyia kazi. Tunafahamu kwamba ndugu zetu wale wa Kigoma na kule Makete na wapi siku hizi hakuna manamba lakini tupo tayari kuifanya hiyo kazi wenyewe sasa, tupeni hayo mashamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nizungumzie suala la kilimo ambalo ni suala kubwa sana. Kwa kweli kwa Tanzania unaweza kupata masikitiko makubwa kama kila mwaka tunaweza kulia njaa. Hakuna mtu yeyote anayetoka kwenye maeneo magumu anayeweza kutuamini tukilia kila siku tuna njaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru sana Ofisi ya Spika na Spika mwenyewe kwa sisi wachache wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, tulipata nafasi ya kwenda kujifunza jinsi Waarabu wa kule jangwani Misri wanavyotumia Mto Nile. Tunamshukuru pia Waziri wa Maji, Mheshimiwa Edward Lowassa na Serikali kwa kuandaa utaratibu huo wa kwenda kujifunza na kuona. Lakini tulichojifunza na kuona sio jinsi tu ya kutumia maji ya Mto Nile, kwa kweli ni jinsi ya kutumia maji katika kuendeleza kilimo na kuzalisha umeme kwa manufaa ya wananchi wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mipango yetu ni mizuri sana kama wenzangu walivyosema lakini sasa naomba tuitoe kwenye makaratasi iende kwenye mashamba. Haiwezekani Waarabu wale jangwani, jangwani hasa, wanazalisha mazao chungu nzima, wanauza kwenye soko la Ulaya, ndani ya Jangwa huwezi kuona kijani kibichi wala hata jani lililokauka lakini kwa kutumia maji wanazalisha na wanasafirisha wanauza Ulaya. Nadhani tuangalie upya sera zetu, tuangalie upya vipaumbele vyetu, lazima kilimo kiwe mstari wa mbele kama walivyosema wenzangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasema huwezi kusema kilimo peke yake kiwe mstari wa mbele bila kuzungumzia maji maana maji na kilimo vinakwenda pamoja. Kweli tukiendelea kulalamika juu ya ukosefu wa chakula na njaa kila wakati ni karibu sawa na kumkufuru Mwenyezi Mungu, haiwezekani. Mito imezunguka nchi, Maziwa yamezunguka nchi hii kila mahali, huko nyuma walikuwa wakisema eti Dodoma ni jangwa, kama umefika jangwani hasa utaona Dodoma ni peponi. Mimi naomba kwa

kweli tubadilishe mtazamo wetu ili tuweze kuendeleza kilimo na kubadilisha nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia Wizara ya Kilimo na Chakula, kama yapo maghala iliyoyauza kwa watu binafsi basi yarudishwe mara moja. Haiwezekani tukasema tunahitaji kilimo na kuwawekea akiba Watanzania halafu maghala yaliyojengwa na Serikali kwa kusimamiwa na Serikali yauzwe tena kwa watu binafsi yawe biashara. Naomba sana maghala hayo yaweze kurudishwa kama yameuzwa na yale mengine ambayo hayajauzwa yaweze kutunzwa vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la mipango. Tuna matatizo makubwa kule Wilayani kwetu, Mikoani hasa kwa hawa Maafisa Mipango. Sina hakika utaratibu wa Wizara hii wa kuwasomesha wanamipango wengi ukoje, labda Waziri atatuambia, tulisikia kwamba Wizara ya Fedha inawasomesha sasa Wahasibu kwa wingi. Lakini Wizara ya Mipango bado hatujajua, tunaomba Maafisa Mipango wenye sifa wapelekwe kule Wilayani. Tunaomba Chuo cha Mipango cha Dodoma kiwasaidie hata wale Watendaji wa Kata waliokuwa wanapigwa msasa kwa muda mfupi waweze kuja hapo na ku-*manage* ile miradi yetu midogo midogo ya kule Vijijini. Tafadhali tunaomba jambo hilo liangaliwe maana ni msingi sana. Unaweza kuwa na pesa nyingi lakini kama huna mipango zitakwenda ovyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme tena moja la Jimbo langu sasa. Wenzangu wamezungumza na mimi sipendi sana kuwa na haya na aibu katika kuyasema mambo haya. Sijui Madiwani walivyotolewa kwenye shughuli za kusimamia zabuni ilikuwa ni kwa sababu zilizosemwa kweli au ilikuwa ni kwa sababu gani, mimi bado sielewi. Kwa sababu mambo yanayofanyika sasa hivi, baadhi ya wenzangu wamesema mmesikia mambo si ya kawaida. Mimi nadhani kuondolewa Waheshimiwa Madiwani katika kusimamia shughuli za zabuni za Halmashauri nadhani zilikuwa zaidi ya sababu zilizotolewa. Nadhani kuna makosa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina barabara yangu moja katika Jimbo langu, barabara ya Mtae kwenda Mnazi, unatoka milimani unateremka. Barabara hii ilipewa ya jumla ya shilingi milioni 89. Juzi Waheshimiwa Madiwani, Kamati ya Ukaguzi ya Miradi ya Halmashauri tulipokwenda kukagua barabara hii haipitiki, karibu nusu ya barabara hii haijatengenezwa. Lakini mkandarasi yule ameshalipwa tayari milioni 85 maana yake kule kwenye Mfuko kumebaki milioni nne. Barabara haipitiki robo ya kazi haijafanyika, ameshalipwa milioni 85, hebu niambie hali hii inaelezeka vipi?

Nimeomba kupata maelezo na vigezo vilivyotumika katika kumlipa mkandarasi wakati barabara ipo katika hali hii, mpaka leo hakuna jibu. Mkurugenzi atamtupia Mhandisi, Mhandisi atamtupia Afisa Mipango basi mambo yanatembea pale. Ahadi ninayopewa ni kwamba tutakutafutia hivyo vigezo Mheshimiwa Mbunge tukuandikie. Wenzangu tulikuwa nao mpaka leo hakuna kigezo hata kimoja kilichokuja, sijui kwa Mhehsimiwa Henry Shekiffu rafiki yangu. Kwa hiyo, hali hii inaletwa na nini? Barabara haitengenezwi, fedha haionekani, ameshalipwa mtu. Habari za pembeni au mitaani zinasema sehemu ya pesa hiyo imerudi Makao Makuu Dodoma, ndiyo habari zinavyosema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, habari hizi sisi Wabunge hatuzipuuzi hata kidogo. Hata ile aliyosemea mwenzangu hapa Mheshimiwa John Mwakipesile, habari ni hiyo hiyo kwamba sehemu ya pesa imerudi kwa wakubwa na tunaiambia Serikali ijue kwamba hawa tunaosema ndiyo wapiga kura wetu hata watumishi wa Serikali kule Wilayani na kwenye Majimbo ni wapiga kura wetu. Wapo wakereketwa, wakizidiwa wanamnong'oneza Mbunge kumetokea nini.

Sasa mimi nataka majibu, Mkandarasi huyu amelipwaje pesa zote kabla ya kumalizika kwa barabara, nimeuliza kwenye Halmashauri yangu sikupata, nimengojea maandishi kutoka kule, sikupata. Sasa Wizara inayohusika iliyowanyima haki Madiwani kwenda kusimamia zabuni hizi na shughuli zake itoe majibu pesa hiyo imekwenda wapi na barabara ile itakwishaje.

Lakini napenda kumwunga mkono mwenzangu aliyesema hapa kwamba kuna mchezo mchafu unachezwa huko kwenye Wizara hiyo. Pesa za watu zinachukuliwa zinarudi, zinaliwa, watu wanafanyia mambo. Tunaomba Serikali ilifuatilie jambo hili ihakikishe pesa hizi kama zimeingia mifukoni mwa watu, basi lazima wawajibike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, ni suala la rushwa, sipendi kulisema sana lakini kwa kweli ni vizuri lisemwe. Ni vizuri lisemwe ili tuwasaidie wenzetu wale waliojitumbukiza watoke. Rushwa ni kitu hatari, rushwa ni hatari kubwa na tunasikia wapo watu wanakula rushwa.

Sasa jamani mambo haya ni magumu na adhabu ya rushwa ipo hapa hapa duniani, moto wa rushwa upo hapa hapa wala haungoji uende *Jahanam,* ni humu humu. Kwa mfano, sasa hivi mnaona mambo yanayotokea kwa mzee wetu mstaafu hapo Kenya. Alitakiwa sasa awe anapumzika, amefanya kazi ya watu kwa miaka mingi, lakini sasa ana hoja za kujibu. Mimi nawasaidia wale ambao wamejiingiza, jamani ndugu zangu tokeni, tunataka Chama chetu kiwe safi, Serikali yetu iwe safi, Watanzania waiheshimu Serikali na Chama chake mpaka mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii kwa leo ili nizungumzie katika hotuba mbili ambazo ziko mbele yetu hapa. Lakini kwanza kabla ya kuchangia ningetoa pole kwa msiba uliwafikia Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, nampa pongezi sahibu yangu Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa ushindi mkubwa alioupata. Tangu juzi hapa kuna baadhi wamekuwa wakimtisha Mheshimiwa Makanga kwa kumwambia kwamba kama amekimbia huko kwa kufukuzwa, Chama na CCM kitamfukuza.

Sasa mimi nasema tu CCM hata ikimfukuza yeye na wengine inawafukuza lakini kwa mujibu wa kanuni zake za Chama si kwa ubabe wa mtu mmoja. Kwa hiyo, mimi

natoa nasaha na wasia wangu kwa Mheshimiwa Danhi Makanga kwamba, Mheshimiwa Makanga wakikushtua wewe usishtuke, nani awezae kupitisha lake, ikiwa wana lao, Mola ana yake. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi naanza kwa kuunga mkono hotuba hii na nasema kwamba hotuba zote mbili si mbaya, lakini ninachopenda kuthubutu kusema ni kwamba si kila kizuri hakina hila. Pia sifikirii kwamba kwa sababu Misahafu ile miwili ni mizuri basi hakuna utendaji mbovu ndani ya Misahafu ile miwili. Kwa sababu tuna *Bible* kwa wenzetu Wakristo na tuna Misahafu kwa Waislam, lakini juu ya yote hayo madhambi makubwa yanafanywa na Waislam na madhambi makubwa yanafanywa na Wakristo. Kwa hiyo, mimi nina imani hotuba hizi mbili zinataka usimamizi na uadilifu mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hakuna hata mzungumzaji mmoja aliyezungumza ndani ya Bunge hili aliyekuwa hakuzungumzia suala la upotevu wa mamilioni ya pesa, rushwa ndani ya Serikali, katika Idara na katika Mashirika. Sasa mimi nasema nitamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu siku ya Jumamosi baada ya uzinduzi wa Sera ya Uwezeshaji, nina msaidizi wangu humu ndani, naamini katika waganga wakuu ndani ya Bunge hili ni mimi na Mheshimiwa Omar Mwenda. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi nitamwomba Waziri Mkuu aturuhusu mimi na Mheshimiwa Omar Mwenda, baada ya uzinduzi ule tuje pale mbele, tunakuja na chetezo chetu na mkaa unawaka moto, huu hapa ubani, tutaufukiza. Ubani huu tutaufukiza, nitampa Mheshimiwa Basil Mramba na wasaidizi wake wawili Manaibu Waziri waweke ubani huu mle na kitabu cha *Al-badri* ni hiki hapa

*(Hapa Mheshimiwa Mbunge alionyesha vielelezo husika)*

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, tutasoma *Al-badri* mimi na Mheshimiwa Omar Mwenda kwa sababu mambo yameshakithiri, kama hawakubali maneno ya Wabunge sasa tutatumia uchawi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kitabu hiki Mawaziri waliokuwa wanakula rushwa, Makatibu Wakuu na wengineo watapukutika kama senene. Haitofika mwaka 2005, nakula yamini ndani ya Bunge hili. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nazungumza wasiwasi wangu juu ya Bajeti ambayo ipo mbele yetu. Bajeti hii inataka usimamizi mzuri lakini wasiwasi wangu mkubwa ni kwamba kabla ya kufika Juni, 2005, Waziri wa Fedha ataleta *Mini-Budget* hapa kutokana na hali ya umeme unavyopanda bei na hali ya mafuta sasa hivi shilingi mia tisa kwa Dar es Salaam. Sifikirii hata siku moja kama tutakuwa na uwezo kweli wa kuhitimisha mpaka mwezi Juni mwakani bila kuleta *Mini-Budget* hapa. Naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha atueleze atatumia busara gani na njia gani hata tuweze kufika huko. Hali ni mbaya sana ingawa Bajeti ni nzuri lakini hali ni mbaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine cha tatu ambacho nitachangia ni huo uaminifu na rushwa ndani ya Wizara zetu. Hakuna chuo hata kimoja kinachofundisha uaminifu

katika ulimwengu. Tumesoma kuanzia Zanzibar, Tanzania Bara mpaka Uchina hatujaona chuo kinachofundisha watu uaminifu na kila mtu akisoma sana ndiyo anajua kuiba zaidi, bora wale waliokuwa hawakusoma, wale wa darasa la pili au la tatu hawajui kuiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tafadhali naomba nikueleze juu ya mtu mwaminifu anakuwa vipi. Kuna bwana mmoja alipewa mke wa kaka yake ampeleke safari. Wakati wapo njiani usiku ukaingia, ikawa hakuna njia yoyote lazima walale mahali, wakaomba chumba, wakapata chumba kimoja. Wakalala chumba kimoja lakini bahati mbaya kukawa na kitanda ambacho ni *double decker,* yaani cha juu na cha chini. Yule bwana kwa sababu mwenyewe anavyojidai ana maradhi ya sukari akalala chini kwa sababu kila wakati mwenye maradhi ya sukari anakwenda chooni. Yule bibi akalala juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tazama jinsi uaminifu ndani ya ulimwengu huu ulivyofikia, saa nane za usiku yule bibi juu kule akaona anaguswa guswa, kakamatwa. Akastuka, kugeuka anamwona shemeji yake, akamwambia shemeji mbona hivyo? Akamwambia ahaa, nimeanguka mie, kaanguka kutoka chini kapanda juu. *(Kicheko)*

Sasa ndiyo walivyo hawa watendaji wetu wa Serikali. Lakini bahati nzuri yule kaka mtu mwenye mke akatafuta kila njia ya kumsomea *Al-badri* yule bwana afe kabisa. Kwa hiyo, nasema na Mawaziri hawa ambao sio waaminifu bora wafe kabisa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka kuzungumzia ni suala la biashara ndogo ndogo hasa kwa vijana na akinamama wanaotoka Zanzibar, wanateswa pale bandarini Dar es Salaam. Wote tunaelewa kwamba ushuru wa Zanzibar na ushuru wa Tanzania Bara ni ule ule. Cha kushangaza zaidi kwamba akinamama wale na vijana wale wananunua viguo vyao kuja kuuza Dar es Salaam, wanafika pale wanapekuliwa mpaka utashangaa, halafu wanatozwa pesa risiti hazitambuliki.

Kwa hiyo naomba baada ya Bajeti hii tena nasema na nataka *Hansard* hii iwekwe, tutakwenda Zanzibar mimi, Waziri Basil Mramba, Naibu Waziri wake Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatibu na Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. Festus Limbu. Lakini tutakaporejea nitamchukulia kanzu Mheshimiwa Basil Mramba avae na tarubushi ili asijulikane kama yeye Waziri. Mheshimiwa Dr. Festus Limbu nitamvalisha seruni na fulana ile wanayochezea Msewe kule Pemba na Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatibu, yeye nitampa baibui avae. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wakipita pale nataka wajionee wenyewe au si hivyo watoe tamko siku ya Ijumaa hapa kwamba wakomeshwe wale wanaowatesa wenzao pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi suala la *TRA* sina tatizo na ukweli tukitaka tusitake kazi nzuri wamefanya na wanaendelea kufanya na kama mimi ningekuwa na uwezo basi ningesema kila mwaka wanastahili kuzawadiwa zawadi maalum kwa kazi nzuri wanayoifanya. Matatizo madogo madogo hayakosi, lakini tulikotoka tuangalie tulikuwa tukifika wapi, leo tuko mbali sana, tunapaa, kwa hiyo tuwape moyo ndugu zetu

wafanye kazi nzuri, waendelee na watunzwe bwana. Mheshimiwa Basil Mramba naomba uwatunze hawa watu wako.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka kuchangia ni kuhusu mambo yetu ya Muungano. Wazee wetu walivyounganisha nchi hizi waliunganisha kwa roho safi na kunjufu kabisa na wale watu wa Zanzibar na Watanganyika hawakuwa na tofauti yoyote. Lakini imani yao ilikuwa kwamba kadri tunavyokwenda upande wowote ambao utakuwa unatetereka kwa uchumi wake upande mmoja usaidie. Leo hapa Marehemu Abeid Karume kama angefufuka akaja hapa akasikia na akaona mambo ya Zanzibar basi angesikitika sana.

Mheshimiwa Waziri wa Fedha naomba aende Zanzibar, aone maduka ya Zanzibar, aone hali duni ya Wazanzibar, akaone hali duni ya Serikali ya Zanzibar kutokana na uchumi wake. Leo kwa sababu wanapata *percent* yao ile hatuwaangalii tunasahau kwamba upande wa pili tunastahili kuwasaidia. Mheshimiwa Henry Shekiffu pale amesema na Zanzibar tungeijenga lakini sasa tunakaa kimya kwa sababu na wao wana mapato yao. Naomba tuachie hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi labda niwapongeze taasisi ambazo zipo chini ya Wizara ya Fedha ikiwemo *BOT, TRA, NBC* na baadhi ya benki. Wanasaidia sana, taasisi zote hizo pakitokea mambo yoyote lakini cha kusikitisha ningeomba kumkumbusha Mheshimiwa Basil Mramba.

Mimi mwenyewe binafsi mwaka jana kwa heshima na taadhima nimemletea barua nikazungumza naye akamwita msaidizi wake kwa sababu Zanzibar ilikuwa inaandaa mashindano ya mpira *under 19* ya *East and Central Africa,* Serikali ilikuwa haina pesa tulikuwa tunatafuta michango. Mheshimiwa Waziri wa Fedha aliniahidi na akawaambia watu wake lakini nathubutu kumwambia hapa kwamba hakuna hata senti moja iliyotolewa na taasisi yake na akaniambia kwamba madhali *BOT* ipo Zanzibar nitaamuru mpewe, madhali *NBC* ipo Zanzibar nitaamuru mpewe na madhali *TRA* ipo Zanzibar nitaamuru.

Nawapongeza sana Waziri Mkuu hana taasisi yoyote lakini ameniletea wafanyabiashara wamechangia *millions and millions.* Vile vile nathubutu kusema mbele ya Bunge lako Tukufu, katika Mawaziri ambao nimewaalika na nimewapa barua Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya alikuwa hayupo, yuko Ulaya taasisi zake zote zimechangia *over thirty million.* Leo ikawa Mawasiliano ikaweza kuchangia Zanzibar *thirty million,* Wizara ya Fedha isichangie hata senti tano, inasikitisha na *Al-badri* tutasoma. Mwisho vile vile nampongeza Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nazungumzia suala la kilimo ambalo limezungumzwa na watu wengi. Inasikitisha na ni aibu kwa Tanzania hii iliyokuwa kila ukipita mahali ni *green* kabisa, leo kilimo hatukiwezi. Tumeshindwa na Mascut, Mascut wameipindua Serikali yao mwaka 1971 walikuwa hawana umeme, hawana Chuo Kikuu, hawana shule za sekondari. Sasa hivi wana Vyuo Vikuu kemkem na ukienda wanasafirisha matunda kupeleka nje, kwao ni jangwa tupu.

Mwaka jana nimedanganywa na Mheshimiwa mmoja hapa ndani upande wa mbele pale, ameniambia kwamba tunafanya utafiti wa Tende. Sasa namwambia Waziri wa Kilimo na Chakula, kama anataka mtafiti mimi ni mtafiti wa mambo ya Tende. Tende Tanzania hata wapae mbinguni haiwezi kuja ikawa Tende, kwa sababu Tende inazaliwa wakati wa baridi, inapea na kuiva wakati wa joto na joto lazima lisipungue nyuzi joto baina ya 48 na 50. Leo niambie utafanya miujiza gani Tanzania upate joto hilo. Nimekuja na ushahidi huu hapa. Tende hii hapa hii ndiyo Tende naomba niwaonyeshe.

*(Hapa Mheshimiwa Haroub Said Masoud alionyesha Tende kwa Waheshimiwa Wabunge)*

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, Tende inakuwa hivi na hii ndiyo inayoiva kwenye nyuzi joto 50. Tusijidanganye, kama pesa za utafiti wapelekewe wakulima kule Kyela na kwingineko ili wakalime. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulime mazao ambayo Tanzania yanastawi, mahindi yanastawi, mtama unastawi, mpunga unastawi na maharage yanastawi. Tumesema tunataka kufanya utafiti wa Tende tutapoteza fedha za watu bure tunakwenda Sudan kutafuta Tende. *(Makofi)*

Kingine ambalo ningeomba labda nichangie ni kuhusu habari ya pensheni. Tumefurahi kuona kwamba wale waliopata mkupuo kuanzia mwezi Januari mwakani kwa mujibu wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri wataanza kulipwa. Lakini mimi sioni sababu watu wamestahimili miaka na miaka tumepiga kelele hapa tangu mwaka 1995, leo kama kweli ni uungwana wa Serikali mimi sifikiri kama kuna sababu gani ya kufika mwezi Januari mwakani wameishapata moyo wengine waliokaribia kufa wameanza kufufuka, leo tunasema wasubiri mpaka mwezi Januari, mwakani.

Tunaomba Mheshimiwa Basil Mramba na nitalia kwa kuomba nataka uhakikishe kwamba pensheni zinalipwa kuanzia mwezi Julai, 2004 kama utafika mwezi Januari, 2005 walipwe marupurupu yao ya nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine la mwisho kabisa ambalo napenda kukumbushia baadhi ya Wizara ningeomba Mheshimiwa Basil Mramba akaziangalia. Tulipokuwa tukijadili Makadirio ya Wizara ya Kazi na Maendeleo ya Vijana na Michezo kwenye Kamati inasikitisha, Ustawi wa Jamii wakati tunamhoji mtu wa Hazina aliyekuja pale unaziona fedha hizo walizopangiwa na idadi ya watu kwenye vituo, watu wazima wenye ukomaa na watoto yatima unajua wako wangapi?

Nilipowaambia wafanye *calculation* naona hata haya kuzitaja mbele ya Bunge hili. Kila mtu mmoja alikuwa amepangiwa shilingi 132/= kwa siku, mtoto wangu mimi Shem hachukui hata siku moja wala hakuna mtoto hata mmoja anayekubali kwenda shule akachukua shilingi 130/=. Leo mzee wa Mungu unamuweka pale kwenye kituo hana mikono wala miguu, watoto yatima pale unategemea kuwapangia fedha shilingi 132/=!

Mheshimiwa Basil Mramba, tafadhali, tafadhali, tafadhali, fanya kila uwezalo hilo ulitamke rasmi Bungeni hapa na useme utaongeza kiasi gani cha fedha katika kifungu kile. Wizara ile inaonewa kwa nini kwa sababu Wizara ile ina matatizo matupu maskini ya Mungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naona kengele baada ya nusu dakika nitagongewa. Nashukuru sana na mimi naunga mkono hoja hii, lakini *Al-badri* Jumamosi ipo pale pale. Ahsanteni. *(Makofi)*

**MHE. OMAR MJAKA ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi nataka niungane na wenzangu kumpa pole Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na familia yake, pamoja na Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, kwa kufiwa na mtoto wake.

Vile vile nataka nitoe pongezi zangu za dhati kwa Waheshimiwa Mawaziri hawa wawili pamoja na watendaji wao wote kwa ujumla. Bajeti yao iko wazi sana na kwa kweli kama wataifanyia kazi itaweza kuleta mabadiliko makubwa katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niungane na michango yote ya Waheshimiwa Wabunge waliochangia na niwatake Waheshimiwa Mawaziri hawa wawili na watendaji wao waifanyie kazi. Bahati nzuri Mheshimiwa Rais wetu kila anapohutubia Taifa anatueleza athari na faida za utandawazi. Kwa hiyo, ni imani yangu kwamba watachukua changamoto kwa ajili ya kuifanyia kazi na si vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza kuchangia mimi namuunga mkono sana Mheshimiwa Basil Mramba, amefanya kazi kubwa sana ambayo kwa kweli imeonekana kwa Taifa hili.

Mimi ni shahidi wa macho yangu kabisa. Mimi mwaka 1977 nilipokuwa na miaka 16 nikiwa na timu ya Taifa ya Zanzibar nilikuwepo hapa Dodoma. Tulicheza mechi tatu, pamoja na *CDA,* tukacheza na timu ya Mpwapwa na timu moja ya Makutupora, hali ya Dodoma mwaka 1977 siyo iliyopo leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kusingekuwepo na mabadiliko Waheshimiwa Wabunge kutoka Zanzibar tungekuwa tunakuja na biashara ya khanga na vitu vingine kuliko hata shughuli za Bunge. Kwa hiyo, mabadiliko makubwa sana yametokea katika Taifa hili. Kwa hiyo, nataka niunge mkono kwa kazi kubwa iliyofanywa na Serikali katika miaka hii ya hivi karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile hii ni ishara Waheshimiwa Mawaziri hawa waenda mbio sana wananchi wanachotaka ni maendeleo. Tulifanya makosa nyuma huko, tukaingia katika vita katika Bara la Afrika ambavyo sivyo vya kwetu. Bahati mbaya mwaka 1978 na 1979 tukaingia katika vita na Iddi Amini. Lakini lingine kubwa ni kwamba tumeanza kuujenga uchumi kuanzia mwaka 1984 ambapo tuna miaka 20 ni kosa kuilinganisha nchi yetu na Marekani ambayo iko zaidi ya miaka 200. Kwa

hiyo, hii ni ishara kwamba viongozi wetu hawa na Serikali Kuu ifanye kazi ya ziada wananchi wanachotaka ni maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda ukurasa wa 37 katika hotuba ya Waziri wa Fedha amesema kwamba: "Serikali imedhamiria kuendelea kusimamia vyema nidhamu katika matumizi ya fedha za umma."

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni *commitment* ambayo Mheshimiwa Waziri wa Fedha umeji-*commit* kwa umma. Tunachokuomba itakuwa ni aibu kukuta kwenye gazeti la kesho kwamba kuna bilioni 3 zimepotea katika Wizara fulani.

Tunaomba hapa kama ulivyoahidi usimamie fedha za umma. Tumesikia hapa masuala ya madaraja fedha zimekuwa zikienda kwa uzembe sana. Wananchi wanategemea maendeleo. Kwa hiyo, naiomba Wizara yako na watendaji wote suala hili mlione kwamba mapana kabisa. Wananchi wamechoka kulumbana wanachotaka ni maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 40 nataka niipongeza sana Serikali kwa kuongeza bajeti katika vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama. Hakuna maendeleo kama hakuna usalama katika nchi. Katiba ya nchi na sheria za nchi, usalama wa raia na mali zao inategemea vyombo hivi tusijidanganye.

Kwa hiyo, kama kuna watu wanaona labda vyombo hivi havifanyi kazi siyo kweli. Hivi vyombo vinafanya kazi, na sote ni mashahidi kwamba kuna vijana wetu wako Ngara wamekaa katika mipaka ya nchi tatu kule Uganda, Burundi na Rwanda wakati tunaendesha Bunge hapa na tunaendesha uchumi. Kuna vijana wetu wanafanya kazi katika mipaka ya nchi za Uganda, Burundi na Rwanda, kwa hiyo hapa umefanya jambo la halali na lazima tuimarishe ulinzi wa Taifa hili bila ulinzi na bila usalama hatuna maendeleo katika Taifa hili. Tunaiona Kongo leo ilivyo, Somalia haipo kabisa, Iraq iliyokuwa nchi tajiri ikitajirika dunia hii iko wapi sasa hivi Iraq. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini moja lingine ambalo nataka nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwamba kuna suala la majanga ya moto hakuliingiza hapa. Sasa hivi janga la moto nchini ni moja katika majanga makubwa ya uhalifu katika nchi yetu. Kwa hiyo, kulikuwa na uhalali kuiweka katika hotuba yako siyo uiache kwenye Wizara kwa sababu tuione Serikali Kuu inasemaje vipi kuhusu majanga ya moto katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kuna hali ya ugaidi duniani. Majanga ya moto yatakuwepo tu kutokana na hali ya uchumi duniani na matukio mbalimbali. Kwa hiyo, mimi nataka Mheshimiwa Waziri aliingize hapa kwenye ujambazi, uhalifu, masuala ya uchaguzi pamoja na majanga ya moto. Kwa sababu tulishuhudia tarehe 22 Januari, 2004 moto wa Ubungo ulivyotokea, tarehe 1 Aprili, 2004 Arusha katika jengo la *AICC.* Moto uliotokea tena Ikulu tarehe 13 Aprili, 2004 na vile vile Arusha katika kituo cha mabasi tarehe 14 Aprili, 2004. Kwa hiyo janga la moto ni janga la Kitaifa.

Kwa hiyo, maandalizi makubwa yanatakiwa yafanywe na Serikali Kuu, kwa hiyo, hapa aliweke katika kifungu hiki hapa cha Ulinzi na Usalama wa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeliingiza hili kwa sababu mengi yalichangiwa. Kwa sababu majanga ya moto sasa hivi yataongezeka huko mbele na kwa kutumia nafasi hii nataka niiombe Wizara ya Fedha inunue magari kwa ajili ya viwanja vya ndege. Narudia naiomba Serikali inunue magari kwenye Bajeti hii kwa ajili ya zimamoto katika viwanja vya ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina sababu tano kuu zilizonisababisha kwa nini niiombe Serikali. Ya kwanza, inasema kutua kwa ndege katika viwanja inategemea hali ya zimamoto ilivyo, kama gari moja tu litapata ajali ina maana ndege za *KLM* haziwezi kutua. Nafikiri tunalifahamu ni Shirika kubwa linaendesha usafiri katika nchi yetu.

Lakini ya pili, nasema wakati wa kuzima moto *Ubungo, Airport* walikwenda na gari lao moja, lakini baadaye waliliondoa kurudi uwanjani kwa sababu ndege ya *KLM* ilikuwa inakaribia kutua. Baada ya *KLM* kuruka walirudi Ubungo kuendelea kuzima moto. Ya tatu, ilibidi waache Ubungo warudi *Airport* kwa sababu ni matatizo makubwa ya Kimataifa ambayo nchi yetu inaweza kuyapata kama itatokea ajali katika uwanja wa ndege na ikiwa gari la zimamoto halitakukwepo. Lakini ya nne, kwa kuwa majanga ya moto mengine ni ya Kitaifa hayakwepeki ambapo pia kazi ya kuuzima moto inahitaji amri na kuwa katika eneo la tukio. Kwa hiyo, yanahitajika magari ya ziada. Lakini la mwisho la tano, ili zimamoto na uokoaji uweze kufanya kazi zake vizuri inahitajika kuwa na magari matano.

Mheshimiwa Naibu Spika, nayazungumza haya kwa uwazi kabisa. Naiomba sana Serikali isiiachie Wizara inayohusika ilichukue yenyewe hili janga. Tunaiona sasa hivi Iraq inavyolipuliwa na milipuko tofauti ya moto na wakati tunakwenda kwenye uchumi mkubwa yatatokea katika Taifa letu. Kwa hiyo, lazima tujiandae katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niipongeza tena Serikali katika ukurasa wa 39 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha inasema: "Bajeti imeendelea kutenga asilimia 4.5 ya mapato yatokanayo na misaada *(grants)* isiyo ya miradi kwa ajili ya Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar SMZ. Utaratibu huu utaendelea hadi hapo mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha *(Joint Finance Commission)* yatakapopatikana."

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi haya mapendekezo tangu mwaka 1964 mpaka leo mwaka 2004 yatapatikana lini na mnatwambia nini Zanzibar *serious* kabisa? Hivi Mheshimiwa Waziri wa Fedha katika suala hili hakuna sheria inayokupa uwezo Ijumaa utakapojumuisha ukaongeza hii *point* tano angalau zikafikia asilimia 5. Halafu ukaonyesha njia kwa nini? Zanzibar hatuna uchumi, bajeti ya Zanzibar mara hii itakuwa na upungufu wa asilimia 5 kuliko Bajeti ya mwaka jana mtatusaidia vipi katika maendeleo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama *TRA* inakusanya fedha mpaka Pemba inafika huko, hivi hata hawa Wazanzibar kwa nini hamuwahesabu walioko huku Bara wanafanya biashara hizi fedha zao zote mkatusaidia sisi kule Zanzibar wakati ni Tanzania moja. Hili suala nalizungumza kwa uchungu Mheshimiwa Rais Amani Karume hana muda wa kubishana na watu siyo kwamba labda hawezi kusema mambo ya siasa, huwezi ukasema ndani mwako hakuna kitu, ameichukua nchi katika hali mbaya nyote mnajua. Mishahara ilikuwa hakuna Zanzibar, migogoro mitupu ya kisiasa. Baraza la Mawaziri mnakaa vipi kama hamtufikirii sisi Zanzibar?

Kwa hiyo, naiomba Serikali ikae itufikirie juu ya asilimia 4.5 iondoke tuko kwenye karne ya 21, hii mlikubaliana kwenye karne ya 20. Tunahitaji maendeleo Zanzibar siyo lingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikimnukuu Mheshimiwa Rais wetu Benjamin William Mkapa katika mkutano wake aliofanya hapa Bungeni kwa Waheshimiwa Wabunge, alisema: "Napenda nianze kwa kurejea kwenye muhtasari nilioutoa kuhusu sura kuu ya mwelekeo wa miezi 20 ijayo." Alitoa sura tano, mimi nitanukuu moja na alisema. "Kwanza kuongeza kasi, kubadili mtazamo wa watumishi wa umma kwenye Serikali Kuu na Serikali za Mitaa ili wajue kuwa kazi yao ya msingi sasa ni kuwasaidia na kuwaendeleza wananchi." Mimi Serikali kufuta kodi sishangai kwa sababu tayari Mheshimiwa Rais alishalizungumza hili jambo. Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwasaidia wananchi mimi naipongeza sana Wizara ya Fedha kwa kufuta hizi kodi ni kweli kabisa. Kwa kweli lazima Waheshimiwa Wabunge tukubaliane wananchi wetu wako katika hali mbaya na sisi tunazungumza na wananchi wengi na wengi wameridhika na bajeti hii. Watatushangaa kama hatutoiunga mkono Bajeti hii. Wanakiri kwamba kweli zamani tulikuwa tukiwaibia fedha zao, ndiyo wanatwambia. Lakini sasa tunawashukuru mmetuondolea hili. Kwa sababu maskini ya Mungu wengine walikuwa hawana uwezo wa kupata shilingi 500, alipe kodi gani? Mwaka jana Serikali ilionyesha njia na mara hii imeonyesha njia, kwamba kuanzia milioni 20 mtu ataanza kudai kodi. Naipongeza sana Serikali imekwenda sambamba na kauli hii ambayo Mheshimiwa Rais aliitoa hapa Bungeni kwa Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikirudi kwenye Wizara ya Mipango na Ubinafsishaji katika ukurasa wa 58 inasema: "Sera na msimamo wa Serikali ni kudumisha ushirikiano mzuri wa kidemokrasia uliopo kati yetu na nchi karibu zote duniani. Pamoja na ngazi hizi za Kimataifa na Mashirika mbalimbali kwa manufaa yetu sote."

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali. Haya ndiyo yaliipa nchi yetu kuwa karibu na Mataifa yote makubwa ya dunia tuna uhusiano mzuri bila kutuathiri yote Marekani, Urusi, Ujerumani, Ufaransa, Uingereza na mengine mengi yote. Mataifa haya yanafanya kazi ndani ya nchi yetu na Mashirika yao bila kutuathiri na sisi tunaitawala nchi nzima bila matatizo ya migongano na Mataifa makubwa. Tuyaombe kupitia Bunge hili kwamba bado tunayategemea kutusaidia kuendesha Taifa letu la Tanzania kwa mafanikio makubwa.

Lingine ambalo nataka nilizungumze nilisikia kwamba Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, alimtuma Waziri wake mmoja Pemba juu ya Bandari ya Mkoani tunaomba yale maagizo yafanyiwe kazi. Tunachotaka ni maendeleo hatutaki kingine sisi Pemba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine naiomba Serikali juu ya bandari yetu ya Wesha ishughulikiwe mara moja. Kwa bahati nzuri Mheshimiwa Spika, amefika, kwa bahati nzuri Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, amefika na kwa bahati nzuri Balozi wa Japan alifika na wengine wengi.

Mwisho, naiomba Serikali kwa dhati kabisa Mheshimiwa John Magufuli hayupo, lakini mwaka 2001 nilimwomba ombi langu. Nina barabara zangu tatu za vitongoji, zenye kilometa 24 naiomba Serikali kwa mafanikio makubwa kabisa inisaidie tuweze kuleta maendeleo makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, namtakia mafanikio mema Mheshimiwa Waziri wa Fedha na naitakia mafanikio mazuri Serikali. Naomba sana Waheshimiwa Wabunge tuunge mkono Serikali kwa nguvu zote na kwa mafanikio makubwa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SHAIBU AHMADA AMEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii na mimi niweze kuchangia kwenye hotuba mbili hizi za Waheshimiwa Mawaziri wetu, Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji. Hotuba hizi ni nzuri sana na huenda zikaleta mustakabali mzuri kama zitatumiwa kikamilifu na kusimamiwa vilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nitaungana na wenzangu na mimi kuwapa mkono wa pole Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kufiwa na baba yao mzazi Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile na mimi nampongeza Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa ushindi wake alioupata katika uchaguzi mdogo kule kwenye Jimbo la Bariadi Mashariki hivi karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi sasa naomba kuchangia waliochukua pensheni kwa mkupuo. Waliochukua Pensheni ya mkupuo Waheshimiwa Wabunge wote kila mmoja ilikuwa ni kilio chake kuona ni lini itafanikiwa na leo imefanikiwa lakini tunaambiwa bado mambo yanatayarishwa yatakuwa mwezi Januari, 2005. Tunaomba sote hao waliochukua pensheni ya mkupuo wangelipwa fedha sasa hivi kama hazitapatikana mwezi Julai, 2004 basi japo mwezi Septemba, 2004 walipwe. Kama malipo hayo hayatapatikana basi wale watu watakuwa wamekata tamaa na watakuwa na hali mbaya sana. Maana desturi ya Mswahili ukishamuahidi kitu na akishapata fununu basi pale pale anaanza kukopa, sasa hao wote waliochukua mafao yao kwa mkupuo inaonyesha wazi kwamba sasa hivi walishakopa fedha nyingi sana.

Kwa hiyo, kama Serikali itawalipa itakuwa imefanya jambo la maana sana. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri Basil Mramba, hili suala alishughulikie ili watu wetu nao wapate kujumuika na wale wanaopata pensheni zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nitazungumzia kuhusu mambo ya Muungano. Kwanza, nampongeza Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, kwa hotuba aliyoitoa katika kilele cha sherehe ya miaka 40 ya Muungano wetu. Sherehe ile ilifanikiwa sana kule Mjini Zanzibar, sherehe ile ilikata midomo yote kwa wale wote waliokuwa wanatazama Muungano wetu kwa jicho la husuda. Sasa hivi Zanzibar kidomodomo cha kuvunjika Muungano hakuna, Muungano sasa hivi unaonyesha wazi unanawiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ile aliyoitoa Mheshimiwa Rais kwa kuchukua vigezo vya waasisi wetu wa nchi hii, alichukua kigezo cha Mheshimiwa Marehemu Thabiti Kombo, alichukua kigezo cha Marehemu Abeid Amani Karume na alichukua kigezo cha muasisi wetu Marehemu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, kwa hiyo, ilikuwa ni hotuba tosha kwa wale watu wote waliokuwa na matatizo juu ya Muungano wetu. Kwa hiyo, sasa hivi imekuwa safi kuhusu Muungano kule Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mambo mengi yanayofanywa kwa Serikali ya Zanzibar hasa hususan kwa majengo. Hivi juzi tumeona Mheshimiwa Spika, mwenyewe amekuja kuweka jiwe la msingi katika Ofisi ndogo ya Bunge kule Zanzibar. Halafu na sasa hivi Ofisi ya *BOT* sasa hivi kazi inaendelea kama kawaida na Ofisi ya Makamu wa Rais pamoja na nyumba yake ya kuishi pia sasa hivi watu wanaitayarisha kwa kujenga na Taasisi ya Viumbe Bahari vilevile sasa hivi wanajenga. Kwa hiyo, tunaipongeza sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa shughuli zao wanazofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *TASAF*. *TASAF* tunajua sote kama ni mkombozi wa Tanzania. *TASAF* sasa hivi imeenea kule Zanzibar katika Mikoa yote mitano, lakini matatizo madogo madogo yapo. Hivi sasa fedha zimemalizika wanavyosema wenyewe wataalam na *Project* nyingi sasa hivi zina ngoja fedha ili kumaliziwa. Kuna umaskini wa kukithiri katika sehemu nyingine bado *Project* hizo za *TASAF* hazijafika, kwa hiyo tunaomba wahusika watumalizie zile *Project* zilizopo halafu watuletee fedha tushughulikie sehemu zingine zilizokuwa duni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nitawapongeza baadhi ya Waheshimiwa Mawaziri wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutembelea Zanzibar, wa kwanza, nitampongeza Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, juzi alikwenda Zanzibar amekifagilia Chama chetu cha CCM vizuri sana. Tunamshukuru sana kwa kwenda pale kutoa msaada wa mabati 200 kwa jengo la CCM la Mkoa. Tunamshukuru vile vile kwa Majimbo yote aliyoyatembelea na kutoa msaada katika Majimbo yale. Tunawaomba viongozi wengine Waheshimiwa Mawaziri wafuate mfano wake ili na wao waende Zanzibar kututembelea. Zanzibar ni moja katika sehemu ya Tanzania kwa hiyo na wao waende kule Visiwani kufanya kazi kama aliyoifanya mwenzao ili wapate kutatua matatizo mbalimbali katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, mimi nasema naunga mkono hoja hii mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ALI MACHANO MUSSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi karibu ya mwisho ili niweze kuchangia katika hotuba hizi mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabla sijaanza kuchangia katika hotuba hizi na mimi nichukue nafasi hii ya kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Manaibu wake, Makatibu Wakuu na Maafisa wote wa ngazi zote kwa kufanikisha Bajeti yetu hii. *(Makofi)*

Lakini pia nichukue nafasi hii kutoa mkono wa pole kwa Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kuondokewa na mzazi wao, nafikiri niseme kwamba wenyewe wanajua kwamba kila nafsi itaonja mauti, kwa hiyo, waone kwamba ni jambo la lazima na inafaa tumshukuru Mwenyezi Mungu tu na tumwombee marehemu kwa Mwenyezi Mungu malazi mema. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nafikiri nisisahau kuwaunga mkono wenzangu wote ambao wamewapongeza wale wenzetu ambao wamechaguliwa katika kipindi cha hivi karibuni katika nafasi mbalimbali. Kama Mheshimiwa Getrude Mongella, mama yetu, Mheshimiwa mwenzetu kutuwakilisha katika Bunge la Afrika na vile vile kuonekana kwamba tunao akinamama ambao wanafaa kuongoza na kuchaguliwa kuwa Rais wa Bunge la Afrika kwa mara ya mwanzo kabisa. Kwa hiyo nampongeza sana. *(Makofi)*

Lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mheshimiwa Arcado Ntagazwa kwa kuchaguliwa kwake naye. Lakini kwa sababu muda haukidhi kwa kifupi niseme kwamba mwenzetu Mheshimiwa Danhi Makanga amejua sasa pa kuelekea. Kwa hiyo, naye nimpongeze kwa hatua yake safi na niseme sasa huko ndiko uliko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nafikiri niende katika hotuba zetu hizi hasa hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha ambayo sitaki kuichangia sana kwa sababu mambo mengi wenzangu wamenifilisi na hatutakiwi turudie rudie maneno ambayo yameishazungumzwa. Sasa nichague yale mambo ambayo yanaonekana kwamba labda hayajazungumzwa. Lakini niseme tu kwanza naunga mkono hoja hii mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini baada ya kuunga mkono hoja hii, kuna mambo madogo madogo ambayo nataka na mimi niyatilie mkazo niseme kwamba yaangaliwe. Lakini pia nishukuru nisisahau kwamba nafasi ile ya kuona kwamba wale wenzetu ambao walikwishakukata tamaa ya kulipwa pensheni zao ambao walichukua mafao yao kwa mkupuo niseme kwamba Mheshimiwa Waziri wa Fedha amefanya jambo la maana kuwarejeshea watu malipo kwa sababu kwa kweli walikuwa na hali mbaya sana na pengine wasingelipiga kura mwakani, lakini kwa sababu wengine wangekuwa marehemu, lakini kwa sababu tu watapata pensheni hizo labda tutaendelea kuwa nao katika dunia, Mwenyezi Mungu awajalie tuwe nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hilo, katika Bajeti yetu hii kuna nafasi moja ambayo Mheshimiwa Waziri wa Fedha ameizungumza katika ukurasa wa 40 ambapo alikuwa anazungumzia vikosi vyetu vya ulinzi. Kuna fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya kuimarisha vikosi vyetu vya ulinzi na usalama na pia kutatua matatizo ya uchaguzi katika kipindi kijacho, kwa kweli hili sina utata na nasema kwamba ni jambo jema. Kwa sababu ni lazima uchaguzi tutaufanya na kwa sababu tutaufanya uchaguzi kuna matatizo ambayo yanaweza yakajitokeza, kwa hiyo kutengwa kwa fedha hizi ni suala la msingi. *(Makofi)*

Lakini jambo ambalo nataka kulisemea na nafikiri itakuwa ndiyo mada yangu muhimu ambayo imenifanya niombe kuchangia. Fedha zinazotengwa kwa ajili ya vikosi vyetu vya ulinzi na usalama tungejaribu sana katika kuzigawa tukaangalia kwamba nafasi hii tunaigawa katika hali ya kuona kwamba vikosi vyetu vinalingana. Maana ya kusema hivi ni kwa sababu ndugu zetu hasa wa Jeshi la Polisi wanafanya kazi sawasawa na wenzao wa vikosi vingine. Lakini wamekuwa na malalamiko makubwa kwamba hali ya maisha yao ni duni na kazi wanayoifanya ni kubwa kama wanayoifanya wenzao, lakini utofauti wao katika hali ya maisha inakuwa tofauti sana.

Sasa Mheshimiwa Waziri wa Fedha ningeomba fedha hizi zitakapotolewa kama zimekosekana kwa mwaka huu, lakini katika kipindi kijacho uone namna gani ya kuweza kuwasaidia Jeshi la Polisi ili liwe katika hali ya kukidhi mahitaji yao ya kimaisha na pia ili wafanye kazi yao vizuri katika kipindi cha uchaguzi. Kama utaangalia sana Askari Polisi mishahara yao inatofautiana sana na vikosi vingine. Sitaki kusema kwamba wanapokea mshahara wa kiasi gani na vikosi vingine vinapokea mshahara kiasi gani na wanapata posho kiasi gani na vikosi vingine vinapata posho kiasi gani. Haya ni mambo ambayo yanahitaji kwamba yazungumzwe katika hali ya ukimya kimya.

Kwa hiyo, kama ni ya kuzungumzia kiukimya Mheshimiwa Waziri katika mafungu haya naomba tuangalie Askari Polisi manung'uniko yamekuwa makubwa. Kwa kila anayesimama hapa anaomba pembejeo, anataka kuondoa umaskini. Mimi naungana na wale wote Waheshimiwa Wabunge ambao wametoa hoja hizo au wametoa maoni yao.

Lakini wenzetu maaskari hawana pembejeo. Pembejeo zao ni kwamba kila wakati wavae *uniform* waende kazini. Kama wanakwenda kazini lakini hali yao mbaya wanasababisha wakati mwingine kuweza kuleta mambo ambayo hayaelekei katika shughuli zao za kazi na matokeo yao wana-*harass* wapiga kura wetu. Sasa kwa hilo ningependelea sana likaangaliwa kwa uzito kabisa kuona kwamba tunaangalia, tukikosa katika Bajeti hii, Bajeti zijazo tuone kwamba tunafikiria kuwalinganisha karibu na vikosi vingine. Hii inaweza ikatusaidia katika tatizo lile ambalo linatokea hivi sasa la kila wakati kusikia kwamba kuna ujambazi unatokea lakini maaskari hawaonekani njiani.

Mimi nafikiri askari wanaonekana sana hapa ni *Traffic* ambao kwa sababu wana nafasi ya kukaa barabarani kunyoosha mkono wakiondoka pale hali zao zinaonekana mambo poa. Kwa hiyo, kama ni hilo basi ebu tuwasaidie na wale wengine. Lakini pia nisiishie hapo tu. Kuna nafasi moja ambayo nafikiri wakati wa bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani itafaa tuizungumzie. Tuangalie katika hali ya maslahi yao hata katika

hali ya malazi. Ningependa kumshtua *IGP* ni kwamba katika fedha hizi kama watapewa kuna maaskari pale Polisi Ufundi wanalala katika nyumba ambazo hazistahili kwa kweli. Nyumba ambayo naikumbuka maaskari ni nyumba ya bati ambayo imejengwa *full suit* yaani juu bati na chini bati. Lakini nyumba hiyo imejengwa mwaka 1979 nusu katika nyumba hiyo imeshaanguka na nusu bado wanakaa maaskari. *(Makofi)*

Sasa ningependa Mheshimiwa Waziri wa Fedha utakapowapa fedha hizi basi uone huruma na uone kwamba maaskari wale wafanyiwe maarifa waepukane na ajali ambayo inaweza ikajitokeza. Nafikiri hapo imefika na inaeleweka ninachokizungumza ni nini katika suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudi katika nafasi nyingine ya kuzungumzia suala ambalo mwenzangu amelizungumzia la 4.5% ambayo inapata Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Suala hili limekuwa linazungumzwa sana na sisi kwa sababu tunawakilisha wananchi tunapata malalamiko makubwa na uchungu ambao wanaouona wananchi. Lakini hawastahili wao kufika hapa tunachotakiwa sisi wananchi tunaofika hapa tulizungumzie. Kama walivyosema wenzangu, muda umekuwa mrefu wa 4.5%. Lakini tunachotakiwa sisi tuseme ni kwamba kama muda ni mrefu kila kitu kinafaa kuzungumzwa, kinazungumzika.

Mimi ningependelea Tume ya Fedha ambayo imeundwa ikae na kufikiria tena angalau ipendekeze 5.5% kwa muda huu angalau kukidhi hali ya aibu ambayo inatokeza katika shughuli za Zanzibar. Hatuwezi tukachambua kwamba Zanzibar kuna matatizo gani, Tanzania Bara kuna matatizo gani? Kipindi kifupi tu tueleze kwamba matatizo yaliyopo kule na misaada ambayo inayotolewa na mikopo basi tufikirie kwamba ndugu yako unapoona aibu inampata ni vizuri wewe mdogo wake au kaka yake kumsaidia. Kwa hiyo, nafikiri kuna baadhi ya mambo ambayo yanayozungumzika tukae tuyazungumze kabla kipindi hakijarefuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa muda uliokuwa umebakia haukidhi haja, mengine tuyaweke tuzungumze kesho. Lakini bado nisisitize kwamba katika Bajeti hii mimi naunga mkono na niseme kwamba ni njema na inafaa. Lakini kuna watu bado wanaendelea kuibeza sijui niwaite wapinzani au nani. Mimi niseme tu kuwa katika dunia atakayetengeneza kitu chochote ambacho hakitakuwa na dosari hata moja hayupo. Atakayetengeneza mambo ambayo yatakuwa yamekamilika ni Mwenyezi Mungu tu. Kwa hiyo, Waheshimiwa Mawaziri na maafisa wengine kazi waliyoifanya kubwa na lazima tuithamini. Kwa hiyo, hatuna budi kusema kwamba tuiunge mkono hotuba hii na tuone kwamba ina mafanikio kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, muda uliobaki hautoshi kwa mchangiaji mwingine kwa hiyo, kufikia hapo sasa naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.36 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi, Tarehe 17 Juni, 2004 Saa Tatu Asubuhi)*